**OORODHA YA WAJUMBE WA BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR**

**MHE. PANDU AMEIR KIFICHO - SPIKA**

| | |
|---|---|
| 1. Mhe. Ali Abdalla Ali | Naibu Spika/Jimbo la Mfenesini. |
| 2. Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa | Mwenyekiti wa Baraza Jimbo la Kikwajuni. |
| 3. Mhe. Mgeni Hassan Juma | Mwenyekiti wa Baraza/ Nafasi za Wanawake. |
| 4. Mhe. Balozi Seif Ali Iddi | MBM/Makamu wa Pili wa Rais/Kiongozi wa Shughuli za Serikali/Kuteuliwa na Rais. |
| 5. Mhe. Dr. Mwinyihaji Makame Mwadini | MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Ikulu na Utawala Bora/ Jimbo la Dimani. |
| 6. Mhe. Omar Yussuf Mzee | MBM/Waziri wa Fedha/ Kuteuliwa na Rais. |
| 7. Mhe. Haji Omar Kheri | MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ/JimbolaTumbatu |
| 8. Mhe. Fatma Abdulhabib Fereji | MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais/Kuteuliwa na Rais. |
| 9. Mhe. Mohammed Aboud Mohammed | MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais/ Kuteuliwa na Rais. |
| 10.Mhe. Abubakar Khamis Bakary | MBM/Waziri wa Katiba na Sheria/Jimbo la Mgogoni. |
| 11. Mhe. Rashid Seif Suleiman | MBM/ Waziri wa Afya/Jimbo la Ziwani. |
| 12.Mhe. Ramadhan Abdalla Shaaban | MBM/Waziri wa Ardhi, Maakazi, Maji na Nishati/ Kuteuliwa na Rais. |

| | |
|---|---|
| 13.Mhe. Juma Duni Haji | MBM/Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano/Kuteuliwa na Rais. |
| 14.Mhe. Zainab Omar Mohammed | MBM/Waziri wa Uwezeshaji, Ustawi wa Jamii, Vijana, Wanawake na Watoto/Kuteuliwa na Rais. |
| 15.Mhe. Abdillah Jihad Hassan | MBM/Waziri wa Mifugo na Uvuvi/Jimbo la Magogoni. |
| 16.Mhe. Ali Juma Shamuhuna | MBM/Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Jimbo la Donge. |
| 17.Mhe Dr. Sira Ubwa Mamboya | MBM/Waziri wa Kilimo na Maliasili/Kuteuliwa na Rais. |
| 18.Mhe. Nassor Ahmed Mazrui | MBM/Waziri wa Biashara,Viwanda na Masoko/Jimbo la Mtoni. |
| 19.Mhe. Said Ali Mbarouk | MBM/Waziri wa Habari, Utamaduni Utalii na Michezo/Jimbo la Gando. |
| 20.Mhe. Haroun Ali Suleiman | MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi Ya Rais, Kazi na Utumishi wa Umma/Jimbo la Makunduchi. |
| 21.Mhe. Haji Faki Shaali | MBM/ Waziri Asiekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Mkanyageni. |
| 22.Mhe. Machano Othman Said | MBM/Waziri Asiekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Chumbuni. |
| 23. Mhe. Shawana Bukheit Hassan | MBM/Waziri Asiekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Dole. |
| 24. Mhe. Issa Haji Ussi (Gavu) | Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano/Jimbo la Chwaka. |

| | |
|---|---|
| 25. Mhe. Zahra Ali Hamad | Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Nafasi za Wanawake. |
| 26.Mhe.Mahmoud Thabit Kombo | Naibu Waziri wa Afya/ Jimbo la Kiembesamaki |
| 27.Mhe. Bihindi Hamad Khamis | Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni,Utalii na Michezo/ Nafasi za Wanawake. |
| 28.Mhe. Haji Mwadini Makame | Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati/ Jimbo la Nungwi. |
| 29.Mhe. Thuwaybah Edington Kissasi | Naibu Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko/Jimbo la Fuoni. |
| 30.Mhe. Mohammed Said Mohammed | Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi/Jimbo la Mpendae. |
| 31.Mhe. Mtumwa Kheir Mbarak | Naibu Waziri wa Kilimo na Maliasili/Nafasi za Wanawake |
| 32.Mhe. Said Hassan Said | Mwanasheria Mkuu. |
| 33.Mhe. Abdalla Juma Abdalla | Jimbo la Chonga |
| 34.Mhe. Abdalla Moh'd Ali | Jimbo la Mkoani |
| 35.Mhe. Abdi Mosi Kombo | Jimbo la Matemwe |
| 36.Mhe. Ali Mzee Ali | Kuteuliwa na Rais |
| 37.Mhe. Ali Salum Haji | Jimbo la Kwahani |
| 38.Mhe. Amina Iddi Mabrouk | Nafasi za Wanawake |
| 39.Mhe. Asaa Othman Hamad | Jimbo la Wete |
| 40.Mhe. Asha Abdu Haji | Nafasi za Wanawake |
| 41.Mhe. Asha Bakari Makame | Nafasi za Wanawake |
| 42.Mhe. Ashura Sharif Ali | Nafasi za Wanawake |

| | |
|---|---|
| 43.Mhe. Bikame Yussuf Hamad | Nafasi za Wanawake |
| 44.Mhe. Farida Amour Mohammed | Nafasi za Wanawake |
| 45.Mhe. Fatma Mbarouk Said | Jimbo la Amani |
| 46.Mhe. Hamad Masoud Hamad | Jimbo la Ole |
| 47.Mhe. Hamza Hassan Juma | Jimbo la Kwamtipura |
| 48.Mhe. Hassan Hamad Omar | Jimbo la Kojani |
| 49.Mhe. Hija Hassan Hija | Jimbo la Kiwani |
| 50.Mhe. Hussein Ibrahim Makungu | Jimbo la Bububu |
| 51.Mhe. Ismail Jussa Ladhu | Jimbo la Mji Mkongwe |
| 52.Mhe. Jaku Hashim Ayoub | Jimbo la Muyuni |
| 53.Mhe. Kazija Khamis Kona | Nafasi za Wanawake |
| 54.Mhe. Makame Mshimba Mbarouk | Jimbo la Kitope |
| 55.Mhe. Marina Joel Thomas | Kuteuliwa na Rais |
| 56.Mhe. Mbarouk Wadi Mussa (Mtando) | Jimbo la Mkwajuni |
| 57.Mhe. Mlinde Mabrouk Juma | Jimbo la Bumbwini |
| 58.Mhe. Mohammed Haji Khalid | Jimbo la Mtambile |
| 59.Mhe. Mohamedraza Hassanali Mohamedali | Jimbo la Uzini |
| 60.Mhe. Mohammed Mbwana Hamadi | Jimbo la Chambani |
| 61.Mhe. Mussa Ali Hassan | Jimbo la Koani |
| 62.Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa | Nafasi za Wanawake |
| 63.Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi | Nafasi za Wanawake |
| 64.Mhe. Nassor Salim Ali | Jimbo la Rahaleo |

| | |
|---|---|
| 65.Mhe. Omar Ali Shehe | Jimbo la Chake-Chake |
| 66.Mhe. Panya Ali Abdalla | Nafasi za Wanawake |
| 67.Mhe. Rufai Said Rufai | Jimbo la Tumbe |
| 68.Mhe. Raya Suleiman Hamad | Nafasi za Wanawake |
| 69.Mhe. Saleh Nassor Juma | Jimbo la Wawi |
| 70.Mhe. Salim Abdalla Hamad | Jimbo la Mtambwe |
| 71.Mhe. Salma Mohammed Ali | Nafasi za Wanawake |
| 72.Mhe. Salma Mussa Bilali | Nafasi za Wanawake |
| 73.Mhe. Shadya Mohamed Suleiman | Nafasi za Wanawake |
| 74.Mhe. Shamsi Vuai Nahodha | Jimbo la Mwanakwerekwe |
| 75.Mhe. Subeit Khamis Faki | Jimbo la Micheweni |
| 76.Mhe. Suleiman Hemed Khamis | Jimbo la Konde |
| 77.Mhe. Suleiman Othman Nyanga | Jimbo la Jang'ombe |
| 78.Mhe. Ussi Jecha Simai | Jimbo la Chaani |
| 79.Mhe. Viwe Khamis Abdalla | Nafasi za Wanawake |
| 80.Mhe. Wanu Hafidh Ameir | Nafasi za Wanawake |

**Ndugu Yahya Khamis Hamad** **Katibu wa Baraza la Wawakilishi**

## BARAZA LA NANE LA WAWAKILISHI

## MKUTANO WA ISHIRINI

### Kikao cha Ishirini na Moja - Tarehe 12 Juni, 2015

*(Kikao kilianza Saa 3.00 Asubuhi)*

### DUA

*Mhe.Mwenyekiti, (Mgeni Hassan Juma) alisoma Dua*

### HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:

**Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo:** Mhe. Mwenyekiti naomba kuwasilisha Mezani Hotuba ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Habari Utamaduni, Utalii na Michezo kw mwaka 2015/2016. Nomba kuwasilisha.

**Mhe. Mwenyekiti wa Kamati ya Mifugo, Utalii, Uwezeshaji na Habari.** Mhe. Mwenyekiti naomba kuwasilisha Hotuba ya Maoni ya Kamati ya Mifugo, Utalii, Uwezeshaji na Habari kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo kwa Mwka 2015/2016. Mheshimiwa naomba kuwasilisha.

### MASWALI NA MAJIBU

### Nam. 40

### Mpango wa Ujenzi wa Kituo cha Sober House

**Mhe. Jaku Hashim Ayoub (Kny.Wanu Hafidh Ameir):** Aliuliza**:**

Katika Kikao cha Pili cha tarehe 22/10/2014 Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais wakati akijibu suala Nam. 34 la Mhe. Saleh Nassor Juma alikiri kuwa bajeti inayopata Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais kwa ajili ya ruzuku za *Sober Houses* ni kidogo kuweza kuhudumia ipasavyo nyumba hizo kutokana na idadi ya nyumba za *Sober Houses* kukuwa na kufikia nyumba 12 Unguja na Pemba.  Kwa kuwa Serikali kupitia Ofisi hii ya Makamu wa Kwanza wa Rais ilikua ina mpango wa kujenga *"Rehabilitation Centre"* ambapo vijana

hawa wote wangepata huduma ambazo wanastahiki kupata katika kituo hicho kimoja ili kupunguza gharama za uendeshaji, lakini pia sambamba na kuwa na utaratibu mzuri wa huduma hizi kwa vijana.

(a) Je, nia lengo na dhamira ya Serikali kujenga "*Rehabitation Centre*" imefikia wapi.

(b) Kwa kuwa nyumba zilizopo hivi sasa zinaratibiwa na watu tofauti kwa nini Serikali haianzishi utaratibu wa kua na mratibu mmoja tu ambae atakuwa ndie Msimamizi Mkuu wa shughuli zote za *Sober Houses* Unguja na Pemba.

**Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais - Alijibu:**

Mhe. Mwenyekiti, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 40 lenye kifungu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Serikali bado inayo dhamira ya kujenga Kituo cha Tiba na Marekebisho ya Tabia "*Rehabilitation Centre*" ambapo kwa mwaka wa fedha 2014 – 2015 uliidhinisha kutumiwa Tshs. 1,400,000,000/= kwa ajili ya ujenzi wa msingi wa jengo la ghorofa mbili na kukamilika ghorofa ya chini *"ground floor"* hadi sasa hatua iliyofikia ni kukamilika kwa msingi na uwekaji wa jamvi.

Naomba nitoe taarifa kwa Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako tukufu Mhe. Mwenyekiti kwamba kwa hivi sasa bajeti hii yote imepatikana Ofisi yangu jana imepokea shilingi 1,150,000,000 kw ajili ya kumaliza ujenzi wa *ground floor ya Rehabilitation Centre.*

(b) Tume ya Kitaifa ya Kuratibu na Udhibiti wa Dawa za Kulevya, ndiyo Msimamizi Mkuu wa masuala yote yanayohusu dawa za kulevya katika kupambana na kutoa huduma za walengwa waliopata matatizo ya dawa za kulevya kwa ajili ya kupata nafuu na kurekebisha tabia.

Kwa hivi sasa nyumba za upatikanaji nafuu (*Sober Houses*) nazo zinaratibiwa na Tume ya Kitaifa ya Kuratibu Udhibiti wa Dawa za Kulevya chini ya Mkurugenzi Mtendaji wa Tume. Huduma hizo zinasimamiwa kwa karibu na Mratibu wa Kitengo cha Taarifa, Kinga, Tiba na Marekebisho ya Tabia kwa watumiaji wa Dawa za Kulevya. Kwa sababu hizo, nyumba zinazofunguliwa na mtu binafsi au Asasi hutakiwa kuomba ruhusa na kupata kibali kwa Tume kupitia mratibu, ambae

husimamia shughuli zote za nyumba kufuatana na mwongozo uliowekwa na Tume.

**Mhe. Shadya Mohammed Suleiman:** Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti kwa kuweza kunipatia na mimi nafasi hii ya kuweza kumuuliza Mhe. Waziri suala moja la nyongeza kama ifuatavyo:

Kwanza nimpongeze Mhe. Waziri kwa kuweza kupata pesa hizo ili ziweze zimsaidie katika nyumba hizo za vijana wetu. Mhe. Waziri kama tunavyofahamu vijana wetu nyumba hizi zinawasaidia sana kutoka kwenye dimbwi la utumiaji wa madawa ya kulevya.

Je, Mhe. Waziri Wizara yako ina utaratibu gani wa kuona kuwa nyumba iliyopo Mbuyuni Wilaya ya Mkoani inafaidika na msaada huo ili vijana wetu wasihangaike katika suala zima la ulipaji wa kodi hii.

**Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais:** Naomba nimkumbushe tu Mhe. Muwakilishi kwamba utaratibu wa Tume ya kudhibiti na uratibu wa dawa za kulevya ni kuweza kuzipatia *Sober house* hizi kila moja shilingi milioni 1,800,000/= kwa mwaka. Fedha hiyo sio kubwa na matumizi ya fedha hii inategemea *Sober house* yenyewe imeweka kipaumbele kipi katika kuzitumia fedha hizo, wengi wa *sober house* nyengine ambazo tunazo huzitumia fedha hizi katika kulipa kodi au pango la nyumba hizo. Sasa kwa kesi ya Mbuyuni *Sober house* ambayo ipo Mbuyuni katika Wilaya ya Mkoani itabidi tuifuatilie tuione kesi yake ikoje. Lakini nasikitika sana kwamba Ofisi kwa sasa haitakuwa na uwezo wa kuwalipia kodi hiyo kwani haina bajeti hiyo.

**Mhe. Nassor Ali Salim:** Ahsante Mhe. Mwenyekiti na mimi kunipa nafasi ya kuuliza suala moja la nyongeza.

Mhe. Mwenyekiti, mbali na majibu mazuri ya Mhe. Waziri na amekiri katika majibu yake kwamba *sober houses* ambazo nyumba hizi zinakaa waathirika wa madawa ya kulevya wamekuwa wakipata ruzuku kama alivyoeleza. Je, Wizara imefanya mikakati gani au mipango gani ya kuwasomesha na kuwapa elimu ya kutosha wasimamizi wakuu wa nyumba hizo, ili kuweza kuzitumia hizo pesa ipasavyo, vile vile kutoa elimu ambayo itaweza kuwajenga vizuri vijana wetu walio katika nyumba hizo.

**Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais:** Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais kupitia Tume ya kuratibu na Udhibiti wa dawa za kulevya kwanza imeandaa muongozo maalum ambao nyumba hizi tunazoziita *sober houses* lazima zifuate vigezo ambavyo vimo katika muongozo huo. Ndani ya

muongozo huo inaelezewa haja ya kuweza kuwa na watu, ambao wanaweza kusimamia matumizi ya fedha vyema, lakini Tume nayo inaandaa mafunzo katika nyakati tofauti kuwakusanya pamoja wale ambao wanashughulika na masuala ya fedha na viongozi wa *sober houses* hizi huwapa mafunzo mbali mbali yakiwemo namna bora ya kutumia fedha.

Kwa fedha hii ya 1,800,000/= naomba niwahakikishie wajumbe kwamba hii matumizi yake yanaratibiwa na Ofisi yenyewe na Tume yenyewe kwamba *sober houses* au nyumba hii ya kupata nafuu inaleta maombi yake ya jinsi gani inataka kuzitumia fedha zile, ndio hapo basi baada ya kuthibitishwa na Tume ndio fedha hizo zinalipwa, ili kuhakikisha kwamba matumizi ya fedha hiyo ndogo inapata faida kubwa katika nyumba hizo.

Vile vile kama nilivyoeleza mafunzo mbali mbali huwa yanapelekwa katika *sober houses* hizi, vijana waliopo kwenye *sober houses* hizi wanapatiwa mafunzo ya kompyuta, mafunzo ya ujasiriamali vile vile na katika baadhi ya *sober houses* wameweza kusaidiwa vifaa kutoka *UNDP* kwa kuweza kujisaidia na hasa kuhakikisha kwamba wanapotoka ndani ya *sober houses* zile wanaweza kujitegemea, ili wasirudi katika vijiwe na kuweza kurejea katika hali ile ya kutumia madawa ya kulevya.

**Mhe. Makame Mshimba Mbarouk:** Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri naomba kumuuliza Mhe. Waziri suala moja la nyongeza.

Kwa kuwa wewe Mhe. Waziri ni mjasiri wa kutokomeza madawa ya kulevya kwa vijana, Wizara yako ilikuwa na mpango mzuri kabisa wa kuweka *centre* ya kujenga nyumba ili vijana hawa wapate mafunzo mazuri na kuondokana na madawa ya kulevya. Je, Mheshimiwa mpango huo bado upo.

**Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais:** Mhe. Mwenyekiti, ni bahati mbaya sana kwamba Mheshimiwa Mshimba kidogo alichelewa kuingia ndani ya ukumbi kwa sababu hilo suala mama la jibu hili lilikuwa linahusiana na kituo hicho, lakini kwa faida yake ni kwamba azma ya Serikali ya kujenga kituo hiki ipo, ujenzi umeanza kama mlivyoona katika picha ya kitabu changu cha bajeti na nimetoa taarifa kwamba jana Ofisi imeingiziwa shs.1,150,000,000/= ili kukamilisha bajeti iliyoahidiwa ya shs. 1,400,000,000/= kwa sababu niliporipoti hapa wakati wa bajeti mpaka mwezi wa Machi tulikuwa tumeingiziwa milioni 250. Kwa hivyo nina furaha na nashukuru sana kwamba Serikali imeshaingiza fedha hizo na ujenzi wa kituo hicho utaendelea hadi kumalizia na *ground floor* kwa sababu ni jengo kubwa sana.

**Mhe. Menyekiti:** Mhe. Jaku naomba tufuate utaratibu wewe sio Mhe. Salehe sijakuita, simama kwanza halafu ndio nikuite jina lako kwa niaba ya Mhe. Saleh sawa.

**Mhe. Jaku Hashim Ayoub:** Hewalla Mhe. Mwnyekiti.

**Mhe. Mwenyekiti**: Na huo ndio utaratibu, endelea.

**Nam. 52**

**Uwepo wa Darasa la Michezo Uwanja wa Gombani**

**Mhe. Jaku Hashim Ayoub. (Kny.Saleh Nassor Juma): -** Aliuliza**:**

Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, kwa muongozo wako na mimi nimekubali kuteleza si kuanguka kwa heshima kabisa. Kwanza nichukue fursa hii kuipongeza Serikali kwa jitihada ilizochukua kuhusu uwanja wa *Mao* baada ya miaka mingi kutoufanyia matengenezo na hivi sasa tumeanza kuushuhudia. Kwa hivyo niipongeze Serikali kwa jitihada hizi na hasa kutokana na mpira wa miguu kukosa sehemu nyingi kufanya mazoezi uwanja ule sasa unaonekana kuwa makini.

**Mhe. Mwenyekiti:** Mhe. Jaku uliza kwa niaba.

**Mhe. Jaku Hashim Ayoub**: Baada ya hapo Mhe. Mwenyekiti, naomba Serikali itoe jawabu la suali namba 52.

Katika kuimarisha michezo ya ndani (*Indoor games*) Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imeamua kujenga ukumbi wa mazoezi ya Judo katika eneo la Gombani karibu na Uwanja wa mpira wa miguu uliyopo Gombani.

Kwa kuwa tangu Serikali kujenga ukumbi ule hadi leo hii haionekani kufanya bidii yoyote katika kuimarisha mchezo huo kisiwani Pemba, kwani darasa la mchezo huo lililopo katika ukumbi huo halina walimu wa kutosha, wenye uwezo pamoja na ukosefu mkubwa wa vifaa vya michezo.

Je, ni kwa kiasi gani Serikali kupitia Wizara husika inatambua uwepo wa darasa la mchezo huo katika ukumbi huo wa Gombani.

**Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo -** Alijibu**:**

Mhe. Mwenyekiti, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 52 kama ifuatavyo:-

Mhe. Mwenyekiti, Wizara ya Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo inafahamu kuwepo kwa darasa la mchezo wa Judo kwenye ukumbi wa mazoezi uliojengwa hivi karibuni kwenye eneo la Uwanja wa Gombani Pemba. Kutokana na kufahamu kuwepo kwa darasa hilo, Wizara inatafautiana na mawazo ya Mheshimiwa Muwakilishi, sio kweli kwamba michezo yote hapa nchini inaimarishwa kwa vyama vinavyohusika na michezo hiyo.

Mchezo wa Judo nao unasimamiwa na Chama cha Judo cha Zanzibar na ndicho kilichomkabidhi Ndugu Khalfan Ali Ussi kuwa Mkuu na Mwalimu wa kituo hicho cha Gombani Pemba. Mwalimu Khalfan ana ujuzi wa kutosha wa mchezo huo na amefunzwa na Mwalimu Mkuu wa Zanzibar Shimahoka akiwa ni Rais wa heshima wa judo Zanzibar.

Mhe. Mwenyekiti, mkufunzi huyo amepata mafunzo mbali mbali na ziara mbali mbali za nje, ndani ya nchi yetu.

**Mhe. Jaku Hashim Ayoub:** Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri naomba kuuliza suala moja la nyongeza.

Mhe. Naibu Waziri alipokuwa akijibu suala la msingi alisema Wizara inatofautiana mawazo na Mheshimiwa Muwakilishi; je, Wizara inasaidia vipi mchezo huo wa judo katika kiwanja cha Gombani na avitaje vitu walivyosaidia kama ni Wizara, ili wanamichezo hao wa judo wa Gombani wapate kujua kama Wizara imepata kutoa msaada kiasi gani au vifaa gani.

**Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo:** Mhe. kwenye suali langu la msingi nimetofautiana na Mheshimiwa Muwakilishi aliyeuliza suali, kwa sababu amesema kuwa jengo la judo ni mwalimu gani ambae anafundisha, nimemtaja Bwana Khalfan na pia nimemtaja Rais wa Judi Zanzibar bwana Shimahoka, na pia vifaa ambavyo vimekabidhiwa kwenye mafunzo haya Mhe. Rais Mwenyewe wa judo anayetoka *Japan*, ndiye aliyeshirikiana na Wizara kuweza kushirikiana na wanajudo walioko Pemba na waliopo Unguja, kwa kuweza kushirikiana na kuweza kutoa vifaa mbali mbali, pahali popote pale panapokuwa na mashindano haya ya ndani na nje ya nchi.

**Mhe. Nassor Salim Ali:** Mhe. Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri naomba kuuliza suala moja la nyongeza.

Mhe. Mwenyekiti, mchezo huu wa judo ni mchezo ambao umekuwa ukiinuka siku hadi siku katika Visiwa vyetu vya Zanzibar au katika nchi yetu ya Zanzibar na Tanzania kwa ujumla, na mchezo huu umekuwa ni kivutio sana kwa vijana wetu

wa Zanzibar. Suali langu ni kwamba Serikali kupitia Wizara husika imekuwa ikisaidia vipi kutoa mafunzo ya nje ya nchi kwa wakufunzi wengine mbali na mkufuzi mkuu wa mchezo huo wa judo, ambae katika maelezo yake Mhe. Naibu Waziri alisema kwamba anatoka *Japan*, lakini ninavyofahamu Mkufunzi huyu ni Mtanzania na Raia wa Tanzania; ni vijana wangapi wamepata mafunzo nje ya nchi ili kuendeleza mchezo huu Zanzibar.

**Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo:** Mhe. Nakushukuru sana kwa kuweza kuniuliza suala hilo. Mhe. Mwakilishi ukiwa ni muasisi wa ZFA na ni mdau wa michezo Mheshimiwa, nakuhakikishia mbele yako ni kuwa hawa vijana wetu wa judo wanakwenda sehemu mbali mbali na tunapata nishani mpaka za dhahabu. Kwa sababu hayo yote wanayoyapata ni mafunzo tosha. Kwa sababu kupata nishani ni kuwa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa kushirikiana na Wizara pamoja na wakufunzi wetu, hili ndilo suali tosha ambalo vijana wetu wanafaidika na mafunzo hayo.

**Mhe. Mwenyekiti:** Mhe. Jazira unataka nini naona umesimama, swali umeshapata moja au hujaridhika na majibu.

**Mhe. Nassor Salim Ali:** Mheshimiwa kidogo nataka kuweka *hansard* sawa kwa ruhusa yako. Katika maelezo yake amesema kwamba... nashukuru kwa kuweza kunipamba zaidi kwamba ni mwana michezo. Lakini katika maelezo yake amesema kwamba ni muasisi, maana muasisi wa ZFA kidogo naona aweke *hansard* sawa hapo. Mimi nilikuwa ni kiongozi tu wa ZFA lakini sio muasisi wa ZFA.

**Mhe. Mwenyekiti:** Mhe. Naibu Waziri rekebisha anasema yeye ni kiongozi, sio muasisi.

**Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo:** Mhe. Mwakilishi hata kama sio muasisi lakini ulikuwemo kwenye ZFA, ulikuwa unaiongoza na umahiri wako ndio ulionipa kusema ni muasisi.

**Mhe. Salim Abdalla Hamad:** Mhe. Mwenyekiti, nashukuru sana na mimi asubuhi hii kupata kuuliza swali la mwisho la nyongeza katika suala hili. Katika maelezo yake mwenye kuuliza swali hili mama alieleza kuwa darasa la mchezo huo yaani huo mchezo wa judo liliopo katika ukumbi huo halina walimu wa kutosha wenye uwezo pamoja na ukosefu mkubwa wa vifaa vya michezo.

Tumepata majibu kuwa yupo mwalimu anayeitwa Ndugu Khalfan na tumepata taarifa kuwa kuna vifaa vimegaiwa, lakini kwa mujibu wa suala hili je, huyu mwalimu mmoja anatosheleza na hivi vifaa vinatosheleza kwa shughuli hiyo

**Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo:** Mhe. Mwenyekiti, mwalimu huyu nilimtaja tu lakini kuna walimu wengine wanatoka Mkoa wa Kaskazini Pemba na Mkoa wa Kusini Pemba. Mpaka Wilaya ya Micheweni walimu wapo na wanashirikiana pamoja kwa hali na mali, ili kuendeleza mafunzo haya.

Mhe. Mwakilishi kuhusu vifaa kama nilivyoeleza Wizara pamoja na Rais wa Judo Zanzibar kwa kushirikiana na Ubalozi wa Japan vifaa hivi ndio wanaoleta na kuwapa vijana wetu ili kuweza kufanya mazoezi.

## HOJA ZA SERIKALI

### Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Bajeti ya Wizara ya Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati Kwa Mwaka 2015/16

*(Majadiliano yanaendelea)*

**Mhe. Marina Joel Thomas Kny (Mwenyekiti wa Kamati ya Mawasiliano na Ujenzi):** Ahsante Mhe. Mwenyekiti, kwa niaba ya Mwenyekiti wa Kamati ya Mawasiliano na Ujenzi naomba kusoma hotuba ya maoni ya Kamati ya Mawasiliano na Ujenzi ya Baraza la Wawakilishi kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Bajeti ya Wizara ya Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati kwa mwaka 2015/16.

Mhe. Mwenyekiti, awali ya yote napenda kuchukua nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu, ambae ametuwezesha sisi kukutana hapa katika Baraza lako tukufu tukiwa katika hali ya uzima na afya njema.

Pia, ningependa kwa heshima na taadhima nikushukuru wewe binafsi kwa kunipa nafasi ya kusimama mbele ya chombo hiki muhimu cha wananchi kueleza kwa muhtasari maoni ya Kamati ya Mawasiliano na Ujenzi kuhusiana na makadirio ya bajeti ya Wizara ya Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati kwa mwaka wa fedha 2015/2016.

Mhe. Mwenyekiti, napenda kuchukua nafasi hii kuwapa pole wananchi wote walioathirika na mvua za masika zilizonyesha. Kama wote tunavyojua kuna wananchi wa maeneo mbali mbali wameathirika na mvua ikiwa miongoni mwao walipoteza uhai, kuharibiwa na nyumba zao na kadhalika. Tunamuomba Mwenyezi Mungu atupe subira kwa wakati huu mgumu na waliopoteza uhai Mwenyezi Mungu awaweke mahali pema peponi, Amina.

Mhe. Mwenyekiti, napenda pia kuishukuru serikali kupitia kitengo chake cha maafa kwa kusaidiana na wananchi wazalendo katika kutoa misaada mbali mbali kwa wananchi walioathirika na kadhia hii. Kamati inawaomba viongozi wa serikali wakiwemo Wawakilishi, Wabunge, Masheha na Madiwani kusimamia vizuri misaada inayopatikana ili kuhakikisha wananchi wote waliothirika wanapata neema hiyo.

Mhe. Mwenyekiti, kazi ya kupitia makadirio ya bajeti ya Wizara ya Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati ni nzito ambayo inalenga kuleta maendeleo katika nchi yetu. Isingewezekana kama tusingepata mashirikiano yako ya dhati pamoja na Wajumbe wangu wa Kamati wakisaidiana na makatibu wawili ambao kwa heshima naomba uwatambue kwa majina kama ifuatavyo:-

| | | | |
|---|---|---|---|
| 1. | Mhe. Mahmoud Mohammed Mussa | - | Mwenyekiti |
| 2. | Mhe. Panya Ali Abdalla | - | M/ Mwenyekiti |
| 3. | Mhe. Mohammed Haji Khalid | - | Mjumbe |
| 4. | Mhe. Marina Joel Thomas | - | Mjumbe |
| 5. | Mhe. Ismail Jussa Ladhu | - | Mjumbe |
| 6. | Mhe. Salma Mohammed Ali | - | Mjumbe |
| 7. | Mhe. Hussein Ibrahim Makungu | - | Mjumbe |
| 8. | Ndg. Saad Othman Saad | - | Katibu |
| 9. | Ndg. Maryam Rashid Ali | - | Katibu |

Mhe. Mwenyekiti, Kamati ya Mawasiliano na Ujenzi ya Baraza la Wawakilishi, ilipata fursa ya kulifikiria kwa kulifanyia uchambuzi wa kina fungu la makadirio ya Bajeti ya Wizara Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati kama ambavyo imeelezwa katika kanuni ya 96 (1) ya Kanuni za Baraza la Wawakilishi Toleo la 2012.

Mhe. Mwenyekiti, Wizara ya Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati ni moja ya Wizara muhimu katika nchi kutokana na ukweli kwamba inasimamia Sekta muhimu ya rasilimali muhimu ya Ardhi, Makaazi ya wananchi, na huduma muhimu katika maisha ya binaadamu ya Maji na Nishati katika nchi yetu.

Mhe. Mwenyekiti, kwa ujumla Kamati yangu ilipitia na kujadili kwa kina makadirio ya Bajeti ya Wizara ya Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati na hatimae kutoa maoni yenye lengo la kuimarisha utendaji wa Wizara hiyo. Tathmini ya ujumla ya Kamati hii kuhusiana na makadirio hayo ni kama ifuatavyo:-

Mhe. Mwenyekiti, **s**erikali imeamua kufanya mageuzi ya bajeti ikiwa ni sehemu ya mageuzi ya utawala na udhibiti wa fedha za umma. Mageuzi hayo ni kutoka mfumo wa sasa unaotumia vifungu *(line item)* kwenda katika mfumo unaotumia program *( Programme Based Budget)* ambao unaangalia zaidi matokeo ya

utekelezaji wa shughuli za Wizara. Inategemewa kuwa kuingia katika mageuzi hayo ya mfumo wa bajeti inaleta uwiano mzuri na kurahisisha utoaji wa huduma kwa jamii.

Mhe. Mwenyekiti, naomba kuwasilisha muelekeo wa bajeti yenye programu ya Wizara ya Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati kwa mwaka wa Fedha 2015/2016. Wizara ya Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati ina jumla ya Programu kuu nne ambazo ni:

Programme 1: Mipango, Sera na Utawala wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati;
Programme 2: Usimamizi na Upangaji wa matumizi ya ardhi;
Programme 3: Uhifadhi wa Mji Mkongwe, uratibu na usimamizi wa shughuli za ujenzi na nyumba za Serikali; na
Programme 4: Usimamizi wa huduma za uzalishaji na usambazaji wa Nishati na Maji.

## HALI YA MAKADIRIO YA MAPATO

Mhe. Mwenyekiti, kwa kuanzia na ufafanuzi wa tathmini ya jumla iliyofanywa na Kamati yangu kuwa makadirio ya mapato ya Wizara ya Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati ni kwa mwaka wa fedha 2015/2016, Makadirio ya mapato yamezidi ambayo ni 4,799,625,000 ukilinganisha na yale ya mwaka wa fedha wa 2014/2015 ambapo yalikuwa ni 4,416,900,000 hii ni dalili kwamba wizara imejipanga kuiongezea zaidi mapato serikali, hatua ambayo Kamati yangu inaipongeza.

Kamati inaamini hili limetokana na ukweli kwamba, lengo la mwaka 2014/2015 halikufikiwa kwa vile vyanzo vingi vya mapato vinavyotegemewa na Wizara hii havikuwa katika hali nzuri. Mfano wa vyanzo ni kama vile viwanda vya kuzalisha kokoto na viwanda vya useremala (Pemba), mauzo ya nyumba za serikali na kodi za nyumba za serikali ambazo kwa muda mrefu zilikuwa hazijafanyiwa mapitio. Hivyo basi, tunaamini kwamba kwa kuwa vyanzo hivi vimeshafanyiwa mapitio pamoja na mategemeo ya kuanzishwa kwa Shirika la Nyumba mapato yataongezeka na lengo la serikali litafikiwa kama lilivyowekwa.

Hivyo, Kamati inaishauri Wizara kuviboresha vyanzo hivi vyengine ili viweze kuzalisha zaidi, pamoja kulipatia ufumbuzi suala la madeni makubwa wanayodaiwa wananchi na Taasisi za Serikali ambao wamekodi nyumba za serikali, ambao ulipaji wake sio wa kuridhisha.

## HALI YA MAKADIRIO YA MATUMIZI YA KAZI ZA KAWAIDA

Mhe. Mwenyekiti, wizara pia imeonekana kupunguza makadirio ya matumizi ya kazi za kawaida, ingawa ni kwa asilimia ndogo ambapo kwa mwaka wa fedha 2014/2015 ilikuwa ni shilingi 7,760,100,000 ambayo ni kubwa ukilinganisha na makadirio ya mwaka wa fedha 2015/2016 ambayo ni shilingi 7,198,900,000. Matumizi haya ni kama asilimia 20 ya fedha ya matumizi ya Wizara ya Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati.

Mhe. Mwenyekiti, samahani kidogo naona bora niwatambulishe wageni wetu waliofika hapa na nafahamu kwamba watakuwa wana dharura nyengine nisiwaweke muda mrefu ili waweze kwenda kufanya shughuli zao.

Waheshimiwa Wajumbe tumepata wageni wa Mhe. Haji Omar Kheir (Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Idara Maalum).

- Hawa ni Wakurugenzi, Mameya na Watendaji wa Majiji na Manispaa za Tanzania;
- Jumla yao ni 30;
- Wanaongozwa na Mwenyekiti wao ambaye pia ni Meya wa Mji wa Zanzibar- Mstahiki Khatib Abrahman Khatibu, Pamoja na Meya wa Tanga Mstahiki Omar Uledi; na
- Wapo Hapa Zanzibar kwa ajili ya Mkutano wao Mkuu wa Majiji ya Tanzania (TACINE).

Naomba Waheshimiwa wageni wote naomba msimame muwasalimie Wajume wa Baraza la Wawakilishi.(Makofi)

Asante sana, karibuni Zanzibar karibuni katika Baraza la Wawakilishi.
Mheshimiwa tuendelee.

## HALI YA MAKADIRIO YA MATUMIZI YA KAZI ZA MAENDELEO

Mhe. Mwenyekiti, katika eneo la makadirio ya matumizi ya kazi za maendeleo kwa mchango wa wafadhili yamepungua sana na haina tofauti kubwa ukilinganisha na mwaka wa fedha 2014/2015 ambapo ni shilingi 26,831,030,000 na mwaka huu wa fedha 2015/2016 ambapo ni shilingi 28,750.560,000 kwa Miradi mbali mbali ya Wizara.

Mhe. Mwenyekiti, kupatikana kwa fedha hizi ni faraja kubwa kwani matumizi mazuri ya fedha hizi yataweza kuleta matumaini mapya kwa ile miradi ambayo kipindi kilichopita haikufanyika kwa ufanisi mkubwa. Ni imani yetu kwamba juhudi za makusudi zitachukuliwa na Wizara katika kuisimamia miradi hiyo ili iendelee kuleta tija kwa wananchi wetu.

Mhe. Mwenyekiti, dhima ya Wizara hii ni kubwa mno, kwa ustawi wa wananchi wetu. Sote tungependa wananchi wetu waishi kwenye nyumba nzuri na zinazoendelea kutunzwa. Tunatarajia sana nyumba zetu zitaendelea kuwa katika hali nzuri kwa kukarabatiwa mara kwa mara, nalo hili liwape moyo wapangaji wetu, hivyo tunaiomba Wizara izingatie kwa upana wake suala la kuzikarabati nyumba za Kengeja na Mtemani.

Mhe. Mwenyekiti, sasa kwa ruhusa yako naomba nijielekeze katika kuchambua programu ambazo zimepangiwa katika Wizara hii kama ifuatavyo:

**PROGRAMU YA UHIFADHI WA MJI MKONGWE, URATIBU NA USIMAMIZI WA UJENZI NA NYUMBA ZA SERIKALI**

Mhe. Mwenyekiti, programu hii inasimamiwa na Idara ya Ujenzi, Idara ya Nyumba na Maendeleo ya Makaazi na Mamlaka ya Uhifadhi na Uendelezaji wa Mji Mkongwe. Madhumuni ya programu hii ni kuhakikisha upatikanaji wa makaazi bora na yenye gharama nafuu kwa wananchi wote pamoja na kulinda na kuhifadhi Mji Mkongwe kama urithi wa kihistoria, programu hii imepangiwa TZS 1,117,901,000.

Mhe. Mwenyekiti, programu hii inatekeleza lengo la MKUZA II la kuwa na makaazi bora ya kutosheleza na endelevu na kushajihisha michezo, kuendeleza, kulinda na kuhifadhi urithi wa kihistoria na utamaduni wa asili, aidha programu hii imegawanyika katika programu ndogo ndogo kama ifuatavyo:

**URATIBU NA USIMAMIZI WA SHUGHULI ZA UJENZI NA NYUMBA ZA SERIKALI**

Mhe. Mwenyekiti, Kamati yangu kwa kipindi kirefu ilikuwa inapigia kelele kuhusu ukarabati wa nyumba za Kengeja na Mtemani zilizopo Pemba. Nyumba hizi ziko katika hali mbaya na wakati wowote zaweza kuja kuleta maafa ya kuanguka, nyumba hizi pia ni miongoni mwa nyumba za serikali ambazo Idara ya Nyumba na Makaazi inategemea kuwa ni chimbuko lake la mapato.

Mhe. Mwenyekiti, katika programu iliyotajwa hapo juu kifungu 003 cha matengenezao ya nyumba za serikali, Idara ya Nyumba imepangiwa shilingi 20,566,000 ambapo haziwezi kukidhi kwa ukarabati wa matengenezo madogo yanayozikabili nyumba za Serikali. Wizara ya Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati kwa muda mrefu imeomba kiasi cha shilingi 200,000,000 kwa ajili ya ukarabati wa nyumba ya Kengeja kwa hatua ya kuezeka ambapo hadi tunamaliza bajeti ya 2014/ 2015 bado Wizara haijapatiwa.

Mhe. Mwenyekiti, Kamati inaishauri serikali kuweka utaratibu wa kuzitengeneza Nyumba zake zilozopo Mazizini ili zipate kutumika kwa kuwaweka Viongozi Wakuu, kwani Serikali inatumia fedha nyingi kuwakodia Viongozi hao nyumba. Wakati zingetumika Nyumba hizo za Serikali ingesaidia kuongeza mapato katika Idara ya Nyumba na kuzifufua nyumba hizo ili kuepusha kuanguka au kufanyika ukarabati mkubwa.

Mhe. Mwenyekiti, Kamati inaipongeza serikali kwa uamuzi wa kuzishughulikia Nyumba zipatazo 26 zilizo katika hali mbaya ya kuangauka Mji Mkongwe, nyumba hizo ni miongoni mwa nyumba karibu 300 za serikali zinazomilikiwa na Idara ya Nyumba. Serikali imeamua kukodisha nyumba nane kwa wawekezaji kwa mfumo wa PPP, kuuza nyumba mbili ili angalau Idara ipate fedha za kuweza kukarabati nyumba 15 zilizobaki. Vile vile Kamati inaishauri Kamati iliyoundwa ya Mawaziri kushughulikia jumba la *treni (Chawl building)* kuharakisha kuwapa elimu wafanyabiashara waliomo ndani ya Jengo ili wahame na kuepusha maafa yanayoweza kutokea na ili ukarabati mkubwa uweze kufanyika.

Mhe. Mwenyekiti, Kamati inaisisitiza serikali kuweka utaratibu wa kuchukua madeni ya Wizara ambayo yanashindikana kulipika ili kuweza kutatuwa matatizo mbali mbali. Baadhi ya madeni hayo ni malipo ya Wajumbe wa Bodi ya Udhibiti wa Kodi za Nyumba ili tupate kuwatia moyo wafanyakazi katika kipindi kinachokuja.

**Uhifadhi na Uendelezaji wa Mji Mkongwe**

Mhe. Mwenyekiti, dhumuni la programu ndogo hii ni kuuhifadhi na kuuendeleza Mji Mkongwe wa Zanzibar kiutamaduni na kihistoria ambapo matokeo ya muda mfupi *(output)* yanayotarajiwa katika utekelazaji wake ni uhifadhi na Uendelezaji wa Mji Mkongwe na usimamizi wa maeneo ya wazi ndani ya Mji Mkongwe.

Mhe. Mwenyekiti, Kamati inaishauri Serikali kuangalia uwezekano wa kulikarabati jengo la Bait el Ajab kwa gharama zake wenyewe ili kuuhifadhi urithi wetu kwa maeneo ya Mji Mkongwe. Takribani imekuwa karibu miaka miwili tangu kupata ahadi kutoka Serikali ya Oman na kuja kwa mtaalamu kukagua ramani na kutoa mapendekezo ya kitaalamu. Mamlaka ya Mji mkongwe imekuwa ikitoa gharama za ujenzi mara kwa mara bila ya matumaini ya kupata ufadhili huo huku gharama hizo zikiongezeka kutokana na muda.

Mhe. Mwenyekiti, Kamati inaishauri Wizara ya Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati wakati wa ujenzi wa ukuta wa ukingo wa bahari ya Mizingani kuangalia mvungu ulioko chini ya barabara ambao unasemekana unakwenda mpaka Skuli ya Forordhani usije baadae kuleta athari kubwa kwa barabara hiyo, wakati hivi sasa nguzo za jengo la *People's Palace* zimeshaanza kupinda.

Mhe. Mwenyekiti, Kamati inaitaka Wizara ya Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati kuingilia kati suala la jengo la Abdul Hamid ambalo limewekewa mwega kwa muda mrefu na kibali cha ujenzi kimetolewa tangu mwaka 2006. Jengo liko katika hali mbaya na liko katika njia kuu ya kuelekea Forodhani hivyo kuogopa kutokea madhara ambayo yanaweza kuepukika.

**PROGRAMU YA USIMAMIZI WA HUDUMA ZA UZALISHAJI NA USAMBAZAJI WA NISHATI NA MAJI**

Mhe. Mwenyekiti, programu hii inasimamiwa na Idara ya Nishati na Madini, Mamlaka ya Kudhibiti Huduma za Maji na Nishati (ZURA), Shirika la Umeme na Mamlaka ya Maji ambayo madhumuni yake ni kuhakikisha kuwepo kwa upatikanaji wa Huduma za Nishati na Maji inayotosheleza mahitaji ya watu, programu hii imetengewa TZS 2,814,638,000. Programu hii inatekeleza lengo la MKUZA II la kuwa na mazingira bora ya ukuaji uchumi na kustawisha ukuaji wa uchumi uliyo endelevu na unaozingatia umaskini uliokithiri pamoja na lengo la kuimarisha huduma za maji na usafi wa mazingira.

**MAMLAKA YA MAJI**

Mhe. Mwenyekiti, Kamati inaishauri Mamlaka ya Maji ijipange vizuri kuweka data za wateja wao vizuri ili iweze kuongeza makusanyo ya mapato yanayotokana na huduma ya ugawaji wa maji. Hili linatokana na matunda ya mafunzo yaliyopatikana ya Mradi wa kuijengea uwezo Mamlaka ya Maji unaofadhiliwa na Serikali ya Japan kupitia Shirika la Kimataifa la Misaada la JICA.

**SHIRIKA LA UMEME**

Mhe. Mwenyekiti, Kamati imeishauri Shirika la umeme kufanya *reform* ya wafanyakazi ili Shirika liweze kufanyakazi kwa faida na kuleta mapato kwa Serikali, aidha Kamati inashauri Shirika la Umeme kufuta na kutowapatia wafanyakazi wake unit za 150 za bure kwa kila mfanyakazi, bali watafute utaratibu wa kuwalipa posho ili posho hiyo watumie kununua umeme huo ili kuongeza mapato ya Shirika.

**IDARA YA NISHATI**

Mhe. Mwenyekiti, Kamati inaishauri Wizara ya Ardhi kuruhusu wawekezaji kujenga *Depots* na *facilities* nyengine ili kuondosha uhaba wa mafuta nchini ili kutatua tatizo la uagizaji na uhifadhi wa mafuta. Kipindi kilichopita nchi yetu imekumbwa na tatizo la uhaba wa mafuta katika sheli zetu zilizopo zikiwemo

*United Petroleum, GAPCO* na BP (*PUMA*) na kusababisha usumbufu kwa wananchi wetu.

Mhe. Mwenyekiti,  Sababu ya msingi ni uwezo mdogo wa uhifadhi wa mafuta hayo kwenye Depot zetu zilizopo Mtoni ambapo hulazimika kununua mafuta kwa kiwango kidogo kulingana na mahitaji. Uwezo tulionao hivi sasa ni ujazo wa Petroli *cubic* mita 150,000, *Diesel cubic* mita 75,000 na mafuta ya taa cubic mita 30,000. Tunaiomba Serikali kuzidi kutilia mkazo uwepo wa *Depot* kubwa na zaidi kuangalia uwekezaji wa wazalendo katika hili.

**HITIMISHO**

Mhe. Mwenyekiti,  napenda nichukue fursa hii kuipongeza Wizara, akiwemo Waziri, Naibu Waziri pamoja na Watendaji wake wote wa ngazi ya juu na chini kwa mashirikiano yao waliyotupa katika kipindi chote cha kazi. Ni imani yangu kwamba mashirikiano haya yataimarisha ili kuleta ufanisi na kuweza kufikia lengo la kuleta maendeleo katika jamii na nchi yao kwa ujumla.

Mhe. Mwenyekiti,  mwisho kabisa nakushukuru wewe binafsi pamoja na Wajumbe wote wa Baraza lako tukufu kwa kunisikiliza kwa makini wakati nikitoa maoni ya Kamati ya Mawasiliano na Ujenzi kuhusiana na Bajeti ya Wizara ya Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati. Aidha napenda kuwaomba Wajumbe wa Baraza lako kuichangia na hatimae kuipitisha bajeti hii.

Mhe. Mwenyekiti,  Kamati inaliomba Baraza lako tukufu liidhinishe jumla ya Shilingi Bilioni 4,799,625,000  kukusanywa na Wizara hii. Pia Shilingi Bilioni 7,198,900,000 kutumiwa kwa ajili ya kazi za kawaida na Shilingi Bilioni 28,750,560,587 kwa kazi za maendeleo. Kamati inaamini kwamba kupatikana kwa fedha hizo Wizara itaweza kutekeleza kazi, majukumu na malengo waliyojipangia kwa kipindi cha mwaka 2015/2016.

Mhe. Mwenyekiti, kwa vile huenda ikawa ni mara yangu ya mwisho kwa kipindi kusimama hapa mbele ya Baraza lako Tukufu natumia fursa hii kumshukuru Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dr. Ali Mohammed Shein kwa kuniamini na kuniteua kuwa Mjumbe wa Baraza la Wawakilishi. Vile vile natoa shukurani zangu za dhati kwake kwa mashirikiano kwangu kwa kipindi cha miaka 3 ambacho nimekitumikia kuwa Mjumbe wa Baraza la Wawakilishi.

Aidha napanda kuwashukuru wajumbe wote wa Baraza hili na kuambia kuwa miaka 3 ambayo nimetumika pamoja katika utendaji wetu wa kazi ni mwingi katika maisha ya binaadamu na mengi yametokea katika mazingira tofauti. Mimi ni binaadamu ninaomba tusameheane.

Mhe. Mwenyekiti, kwa niaba ya Wajumbe wa Kamati ya Mawasiliano na Ujenzi naunga mkono hoja hii ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati kwa mwaka wa fedha 2015/2016.

Mhe. Mwenyekiti, naomba kuwasilisha.

**Mhe. Mwenyekiti:** Ahsante sana Mhe. Marina kwa niaba ya Mwenyekiti wa Mawasiliano na Ujenzi. Waheshimiwa majadiliano yanaendelea nina wachangiaji wawili tu kwa hivyo yule ambaye yuko tayari kuchangia alete jina lake ili niweze kumuweka katika *list* ya wachangiaji, sawa tunaanza na Mhe. Makame Mshimba.

**Mhe. Makame Mshimba Mbarouk:** *Bismillahi Rahmani Rahiim*, leo Mhe. Mwenyekiti, nimetanguliza jina la Mwenyezi Mungu kwa kutoa baraka zote katika wizara hii na hasa Mhe. Waziri ni mtu ambaye yuko karibu kule kwao Mchangani kwa masharifu lazima kidogo atie fatha ya wazee awarehemu, ili bajeti yake iweze kupita vizuri sana.

Mhe. Mwenyekiti, furaha yangu anaijua Mwenyezi Mungu na leo hii ninaanzia na hotuba ya Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati. Kabla sijaanza wazee wamenituma na wazee ni wazee mara nyingi sana mzee akilia basi ujue kuna jambo. Wazee wameshalia sana kwa hivyo wamenituma mtoto wao wamenambia na wewe usilie na mimi nikasema silii, lakini ujumbe nitaufikisha kwa Mhe. Waziri maana pale walipokuwa wakilia na mimi nilikuwa natoka machozi, hata sijafika humu kwenye jengo. Lakini nikasema basi na mimi nitakuwa silii nitajikaza na leo nimejikaza sana na hasa nilivyoanzia kwa jina kubwa la Mwenyezi Mungu, kuiombea shufaa wizara hii.

Mhe. Mwenyekiti, tuna kilio cha Mahkama ya Ardhi, naanzia hapo. Mheshimiwa kuna ma-*assessors,* hawa hawapati zile haki zao kwa mujibu wa utaratibu uliokwekwa. Lakini kuna fununu za hapa na pale kwa sababu ni radio kifua hawajui wengine wanasema huenda ma-*assessors* mara hii Mahkamani wakaondoshwa, wanasema hivyo watu lakini mimi sidhani kama hicho kitakuwepo kwa sababu tukisema kuwa tunatafuta njia ya kusaidiana baina ya majaji na wazee basi ukiwaondoa hawa ma-*assessors* tuseme haki inapotea, hilo moja.

La pili, hivyo vijisenti maana yake vijisenti havyendi na wakati, kupunguza uongozi si chini ya miezi sita sasa hivi pesa zao hawajapewa, lakini la kusikitisha zaidi sasa hivi wamewekwa mbali sio mbali kwa kuwa wanashindwa utekelezaji. Hapana mbali kutokana na ile *pay* yenyewe hawapewi. Kwa hivyo sio mbali kiasi cha kusema mbali. Ninamuomba sana Mhe. Waziri ajitahidi na hawa wazee, ili kuweza kufanikisha hili lengo la wazee wetu kuwasaidia pale walipwe pesa kwa

*time*. Tena basi ukiangalia, sijui pesa yenyewe kiasi gani, sijui kama inafika shilingi 1500 kwa siku. Sijui kiasi gani.

Mhe. Waziri utakuja kunisaidia kuwa wanalipwa kwa kiasi gani kwa kila wanapokaa pale, halafu tuangalie lile pato lenyewe halafu leo likawa linalimbikizwa, sijui utaratibu huu tatizo liko wapi.

Tatizo kuwa fungu lenyewe la wizara dogo, tatizo kuwa pesa hamtiliwi kwa wakati na Wizara ya Fedha, tatizo sijui linakuwepo wapi lakini *inshaalaahu wataala* mimi ninafikiria tuone jinsi gani Mheshimiwa kilio hiki kikubwa sana. Wanakopa mpaka wanajisikia vibaya wazee wetu.

Usione wakija kule mahkamani wana mikoba ile ukafikiriwa, muna pesa au muna vyakula hapana, ile ni moja katika tabia zetu, wazee wetu wanatumia asilia ile mikoba kuja nayo mle katika ofisi zao, lakini haimaanishi kama mkoba ule Mheshimiwa wakirudi unajaa hapana. Mimi naomba sana Mheshimiwa tuweze kufanikisha hali halisi.

Mhe. Mwenyekiti, kipindi cha nyuma niliacha tatizo la gari sijui mara hii gari imepatikana na kwa kweli huyu Mwenyekiti anafanya kazi kwa mazingira magumu sana. Naomba Mheshimiwa tumsaidie na yeye kijana wetu mzuri pamoja na majaji wake. Kwa kweli sasa hivi raha iliyoje kesi zinakwenda murwa kabisa, zinakwenda kwa wakati.
Mheshimiwa hili suala nikupongeze sana kufanya mabadiliko pahali na kutengeneza jambo na ndio ilivyo lazima ufanya mabadiliko ili iendane vizuri. Mhe. Mwenyekiti, *alhamdu lillahi* kesi zinaenda vizuri hatujasikia non'gono hapa na pale mpaka sasa hivi na Mungu awazidishie awape kila jambo la kheri kutokana na utekelezaji wao mzuri. Hiyo ninawaambia siwaviki koti bure, nawavika koti kutokana na utendaji wao mzuri. Kwa hivyo hilo moja.

Mhe. Mwenyekiti, nataka niseme kitu kimoja na hili suala nimeshasema siku nyingi sana. Mhe. Waziri naomba sana ni vizuri kwa mtu yeyote, kiongozi yeyote kuacha pahali jina likawa zuri na kusema kumbukumbu hii fulani alianzisha na ikaweza kufanikisha vizuri. Mji wa Zanzibar sasa hivi hatunao na mimi nachangia Mheshimiwa ukiutengeneza na mimi mmoja katika *supporters* nitakuwa ndie niliyefanya hivyo.

Mhe. Mwenyekiti, nilisema sasa hivi tutafute eneo liendane na mazingira ya mji; mji tuliokuwa nao *Stone Town* ndio utakuwa huo huo, bado mipango miji hawajatuelekeza. Maana yake tuseme ukweli ulivyo tunataka mji uendane na jina la mji. Leo mtu akitoka nje akija hapa anaoneshwa ile ile *Stone Town* tuliyorithi. Sasa kwa ukweli hali halisi ilivyo hebu leo umeshatembea sana, juzi tu ulikuwepo

nje, nitoe mfano Ohio. Mimi nilienda Ujerumani, kila sehemu unayoiona wenyewe wanasema shamba, mimi nasema mjini. Lakini sisi leo kwetu kimazingira ukenda shamba unakubali shamba, lakini wenzetu hiyo shamba mimi nasema hapa shamba kumbe si shamba ni mji kutokana na yale mazingira ya *plan* zao walivyojipanga vizuri sana.

Kwa hivyo Mheshimiwa naomba sana kilio hiki Mheshimiwa naomba uje uniambie umeshatenga eneo zuri ambalo linaweza kusema kuwa sasa mji wa Zanzibar utakuwepo hapa wenye mambo yote, tena sio nyumba ndogo tunataka ma-*skyscrapers* makubwa. Naomba sana hilo utusaidie sana.

Mhe. Mwenyekiti, kuna ujanja unafanyika siku hizi; mimi nataka nikwambie na hilo si lazima uje kunijibu niite kisiri nikufahamishe. Sheria inasema ardhi mkodishaji ni wewe Wizara ya Ardhi. Lakini kuna watu wanakodisha ardhi kinyume na utaratibu. tunakosa mapato mengi sana, hili usilifumbie macho. Hili njoo unitafute kwa wakati wako, nitakuonesha. Ni hatari kubwa Mheshimiwa, unakosa mapato ndio maana tunashindwa hata ma-*assessors* kuwalipa fedha kwa sababu huna kitu.

Kwa hivyo naomba sana hili suala ambalo bado watu wanakiuka sheria na kufanya sheria wanavyotaka wenyewe. Ninakujua wewe Mheshimiwa hutomfumbia mtu macho hilo suala ambalo hali halisi iliyopo.

Mhe. Naibu Spika, kwanza nimpongeze sana Mkurugenzi wa Mipango Miji, ana lengo zuri la kutaka kuweka mji wa Zanzibar kwenye *plan,* sina ubishi nae. Kauli yake anakwambia haombi msaada kusaidiwa, anafanya kazi kama wajibu wake, hilo mimi nakubaliana nae wala sina tatizo nalo na ndio vizuri kabisa. Kwa sababu haiyumkiniki wewe ukamuombe msaada yule wakati yeye tayari ana taaluma iliyokuwa nzuri ya kufanikisha lile jambo alilopewa.

Tatizo liko moja tu niombe sana Mheshimiwa tunachelewa na sababu nilichogundua wana wafanyakazi 4 tu Zanzibar nzima. Hilo kosa sio kosa kwa kuwa umekosa sheria hapana. Kosa kuwa hatoweza kufanya kazi kwa *time,* watu wanavamia maeneo. Watu wanafanya nini tutakuja kumlaumu bure mipango miji na wengi najua humu watamlaumu, ninaamini hivyo.
Msimlaumu, ana watu wachache sana. Watu hao wazunguke mji huu peke yake Unguja ni *cost* kweli, pengine sijui hata hilo fungu lenyewe kama lina-*play* vizuri. Kwa kweli Mheshimiwa vitendea kazi bado ni duni sana na ndio sababu anachelewa. Sasa anapochelewa ndio watu wanapokuja kujenga vile wanavyotaka wao, hatimae Mheshimiwa huwezi kuja ukavunja.

Kwa sababu leo watu wanajenga kwenye mabonde ya mpunga, kwenye maji, mapitio ya maji, hatari tupu mafuriko kabisa. Vile vile tuwaombee hao unajua sasa hivi tunazaa tusiseme uongo tunazaa sana *population* inazidi kukua. Ningeomba sana hawa ndugu zetu waliopata mafuriko ya maji juzi juzi, hebu watafutie eneo uwaondoe kule na uwapeleke kule juu, kwa sababu watu wengi wamepata athari kubwa sana na Serikali ndio muhimili wa kuweza kufanya kitu hiki.

Ninawaombea sana Mheshimiwa na wale wanaojenga katika mabonde ya mpunga, njia za maji waondoeni mara moja kwa njia nzuri na za busara, kwa unyenyekevu watafutieni eneo ambalo lililokuwa mbadala.

Kwa sababu uzazi hatuwezi kuuzuia kwani sehemu nyengine zinakua giza, mtu hana lolote la kufanya inabidi uzae tu kwa sababu hupati hata sehemu ya kwenda kuangalia televisheni. Kwa hivyo naomba sana hili suala tuweze kufanikisha. Vyengine vyovyote tutakuja mzuilia mafungu bure maskini ya Mungu, tutamuonea. Kwa hilo naomba sana Mheshimiwa. Huwezi kama mipango miji haijapanga kama upimaji, upimaji ni mtu ambaye anakuja dakika za mwisho, hiyo ndio dhana yenyewe. Nahusudu sana Mheshimiwa na suala hili nimpongeze sana naibu wangu aliyekuwa Mwenyekiti wa Mawasiliano na Uchukuzi Maalim Rashid alilisema sana neno hili, leo tizama faida yake hii hapa. Alisema vile vitu viwe tofauti, naam yule pale Mheshimiwa unaona raha hiyo sasa anafurahi kuona kuna Mkurugenzi wa Mipango Miji. Kuna Mkurugenzi wa Upimaji, kuna Mkurugenzi wa Usajili wa Ardhi alilisema yeye. Lakini kwa bahati mbaya ameshaondoka huko amepanda daraja nyengine. Hivyo ndio inavyotakiwa. Sasa na mimi naomba sana Mheshimiwa kutokana na hii wajumbe kumbe wakitembelea kwenye Kamati wanakuwa wanasema jambo lilokuwa la msingi sana.

Kwa hiyo, mimi naomba sana Mheshimiwa kuwa tusimuweke Mkurugenzi wa Upimaji bali aweze kutekeleza kazi yake vizuri huyu, apike amletee huyu na huyu amalize mwenyewe Januari amalize kazi yake. Hii ndio raha iliyoje, haina tatizo wala upinzani kabisa hata wewe mwenyewe unajisikia raha kutokana na utekelezaji ulivyo. Kwa hivyo, naomba sana na ninaona raha zaidi huyu Mkurugenzi ni mbishi sana upimaji. Ni kweli, ni mbishi hawezi ovyo ovyo akasema kuwa basi mimi nitavamia tu nitapima tu, hapana hilo nampa sifa yake. Sifa yake mtu apewe kabisa, ameondoa matatizo mengi mengi tu. Nimshukuru sana Mwenyezi Mungu ampe kila la kheri, ampe na mengine yenye kheri na yeye.

Mheshimiwa watu wako hatuna la kuwapa Baraza la Wawakilishi, hatuwezi kuwatunza tukawapa fedha, lakini waombee dua yenye kheri ni sawa sawa na thamani ya pesa.

Dua ukimuombea binadamu mwenzako yeyote basi ni sawa sawa na umempa fedha nyingi za kuweza kujikimu katika maisha yake, tusidharau dua nzuri. Dua zinapokelewa na Malaika na sisi wengine masharifu tukitoa dua basi hailali asubuhi Mwenyezi anaipokea, ile neema anakuja kuileta pale. Kwa hivyo, mheshimiwa ningependa sana kwamba niwashukuru nao hao kutokana na hali halisi inavyojitokeza katika utendaji wao wa kazi.

Mhe. Mwenyekiti, niende katika Idara ya Nyumba, tulipitisha sheria hapa lakini juzi nilisikia kwenye nyumba hii ya treni nikaambiwa kuwa *ZSSF* ndio inayoshughulikia sehemu ya ujengaji. Nikaja nikajiuliza *ZSSF* kawa *contractor* hapa kidogo sijafahamu vizuri. Lakini nikajiuliza huyu *ZSSF* anahusiana na nini na jumba lile, mfadhili mwenyewe wa kulijenga halafu mkakatibiana.

Je, huyu muhusika ambaye tuliyempigia kura zote hapa ameshirikishwa? Ndio maana tukasema kuwa jamani hizi sheria tunavyozitoa hapa tuwaachie wenyewe fursa, tuwape wenyewe meno. Sasa sijui ikoje kwa sababu mpaka leo naona shirika hili tulililoliunda hapa la nyumba naona bado sijafamu, kwa sababu sasa hivi nilitegemea mimi tayari hawa wataniambia wana mabilioni ya fedha, na hasa nataka nijue hivi sasa hivi nyumba ngapi wanamiliki wao. Hilo la kwanza.

La pili wana benki gani ambayo tayari wameshirikiana nayo katika utendaji wao wa kazi. Mimi nina shirika kubwa sana la kuweza kufanikisha wakakubaliana hawa, wakajenga nyumba zenye mkopo nafuu. Itakuwa tumesaidia sana hilo suala, tena sana kabisa watakwenda vizuri na mipango miji, watakwenda vizuri na msajili, unaona utamu huo. Sasa hiyo ningeomba sana tuwape haki zao kwa mujibu wa sheria zetu.

Mhe. Mwenyekiti, nimekumbuka kitu hapa kwa Mhe. Waziri nataka nikiseme, tuna wazee wetu pale walipima viwanja wale Halmashauri pale kwa Gube. Hawa wazee walitoa pesa siku nyingi sana, lakini kwa kuwa tuna utaratibu wa sheria kukatoka barua kwenye mipango miji kwa kuzuiliwa wale watu wasijenge. Sipigi kelele mimi wala silalamiki kwa sababu anayeanzisha anaanzisha jambo kwa nia nzuri, lakini baadae kwa sababu kila mtu ana akili yake humu ndani, unaweza mtu kidogo akakosoa. Lakini je, *ethics* yake iko wapi. Hasara zake ni kubwa kwa sababu tayari wale watu wameshatoa fedha hawajui masikini wazee wangu wale. Wao wanachokimbilia kupata maslahi kwa sababu leo chumba kimoja kina *population* ya watu chungunzima; baba humo, mama yumo, mtoto yumo. Sasa wale ndio waliona watafute eneo la kuweza kujikimu.

Kwa hiyo, Mhe. Waziri naomba sana tuwasaidie kwa huruma, kwa unyenyekevu unaostahiki kama haiwezekani pale tuwatafutie sehemu nyengine inayostahiki kuweza kuwapa, kwa sababu ni muda mkubwa na fedha zao zishakuwepo

zingekuwa zinazalisha tu sasa hivi. Wana milioni mia mbili, kwa sababu ni muda mrefu sana.

Mhe. Mwenyekiti, jengine nimeleta barua mezani kwako wale wafadhili sasa hivi wako tayari, pesa ziko mkononi wanataka kujenga eneo nililokwambia la skuli ya kusomesha *nursing, orderly, medical*. Hao watu tayari, lile eneo sasa naomba unikabidhi wananchi wangu wa Jimbo la Kitope waweze kusoma masuala ya *nurse* tutatibu wenyewe tumeamua.
Hawa watu tayari tenda zipo ndio maendeleo yenyewe, nikijenga mimi hilo nikikaa nyumbani kama sikupata kura itakuwa jina nimeweka, nani kama si Mshimba, hiyo si mchezo. Sasa naomba sana hawa watu wako tayari tukimaliza bajeti hapa mimi naamini hawa wataipitisha tu hawana wasi wasi wowote, rasha rasha zitakuwepo hili jambo la kawaida. Binadamu unaweza ukavaa koti ukasahau ukosi nje ukautoa, hiyo imo wala usipate tabu nayo, hiyo imo.

Mimi naamini kwa kuwa watu wote wanahitaji ardhi humu sidhani kama watu watakupigia buti hapa, hata siku moja sidhani. Piga buti uone kama utapata kiwanja. Kwa hiyo, hili suala wala usiwe na hofu nalo naamini litafanyiwa kazi kwa vizuri. Kwa hivyo, mimi naomba sana wale watu sasa hivi wako tayari.

Mhe. Mwenyekiti, jengine tusaidie vijana wako tunataka kutengeneza kiwanja cha *International* sasa hivi, kiwanja cha mfano hakuna Kaskazini “A” wala Mjini; hiki kiwanja babu kubwa, itakuwa ni cha pili kutoka huko Ulaya.

Mheshimiwa sifa hiyo unayo hilo wala usije ukanijibu lakini naomba sana tuharakishe kipindi kimeingia cha lala salama wananchi wanataka kufanya, dingi wangu nisaidie tufike pahali pazuri sana kwa uwezo wa Mwenyezi Mungu.

Mhe. Mwenyekiti, niingie ukurasa wa 19 Mamlaka ya Hifadhi ya Mji Mkongwe. Nimefurahi sana, nilikuwemo mimi wakati ule kila siku tunasema tutajenga, tutajenga. Leo nimepita pale nimeona mabati yameshaanza kuzungushwa ukuta ule unataka kujenga na iendane na ile ramani itakuwa sasa hivi *Alhamdulillah*, ile hali halisi ya Mji Mkongwe, unafurahisha.

Mheshimiwa nimefurahi sana kumbe tukiwezeshwa tunaweza, hilo mimi nafurahi sana mheshimiwa na nimpe pole sana Mkurugenzi wangu wa Mji Mkongwe, lakini anajitahidi sana huko katika *UNESCO*, na Mwenyezi Mungu atamuwezesha.

Mhe. Mwenyekiti, kuna jumba moja kubwa sana linatuharibia Mji Mkongwe, jumba lile lina nanga, sasa mimi huwa najiuliza hili boti au nyumba. Mheshimiwa utakuta *partitions* maana yake utacheka mawe, hilo kwa kweli halileti taswira nzuri, litauwa kama ndio *supporter* yenyewe. Naomba sana lile tulitafutie njia ya

kuliondoa haraka sana. Kwa hivyo, mheshimiwa ujenzi wa ukingo wa ukuta wa bahari nimekubaliana nao, naomba sana ujitahidi sana kwa sababu ni kipindi kilichokuwa kizuri sasa hivi cha kutangaza sera yetu ya Chama cha Mapinduzi.

Mhe. Mwenyekiti, niende katika masuala ya Mamlaka ya Maji (*ZAWA*). Niwapongeze sana haki ya mtu mpe, hawa wanajitahidi sana kutafuta maji, lakini pole pole nawaambia mwisho wataitoboa ardhi yetu ya Zanzibar yote.
Maana ya kusema hivi ni kwamba tayari visima vingi wameshavichimba Mamlaka ya Maji kwa kweli inafanya kazi vizuri sana. Sasa hivi ile dhana ya kukaa kwenye kiti watu wakazunguruka hivi kama pia, hawa watu wanaondokana kabisa wanakwenda *field* sasa hivi. Wanaangalia wapi kila siku wanatoa hapo, wanatoboa hapo *wallahi* kwa kuonesha ushahidi hii jadweli si ya uongo.

Mimi ni mdau wao mmoja mkubwa sana. Na mdau wao kwa sababu nahitaji mahitaji kutoka kwao, sasa ushahidi tosha nikifanyiwa mimi ninaona na wenzangu wanafanyiwa. Kwa hivyo, niseme ukweli jadweli hii inasema kweli nimpongeze sana Mhe. Waziri kwa utekelezaji wa watu wake nambari *one,* wanakwenda vizuri sana.

Mhe. Mwenyekiti, kisima kimechimbwa, tenki limetengenezwa *wallahi* kama hili lakini tofauti na hili, hili tenki zuri sana mimi sijapata kuona nilidhani ni kutoka Japan kumbe naambiwa ndani ya Zanzibar. Zamani tukitumia madubwana yale ya *calcium.*

Mabati wameondokana nayo kwa sababu matumbo yanakuwa tunapata matatizo kutokana na hayo, hilo nawashukuru sana. Tizama kitu kilivyotulia hapa *wallahi* huwezi amini ni raha iliyoje. Sasa mimi niwapongeze sana, waendelee na ustadi huu.

Kwa hivyo, ninawaomba sana tujitahidi tuwatengenezee kisima chetu kile pale watusambazie mabomba, ili wananchi waondokane na tatizo la maji.

Mhe. Mwenyekiti, halafu ukiwaita tu *faster* hicho kitu sifa moja nyengine nataka nikwambie, ukikusanya *meeting* na wananchi hawa wanakuja hawaringi, huyo Mkurugenzi wao ukija pale utasema kama ndio Mshimba hatambulikani kuwa nani mkubwa kutokana na alivyoji-*act,* hiyo *acting* yake inasaidia na ndio maana unapata sifa kwa watu kutokana na *acting* yake. Pamoja na Wakurugenzi wengine, Mkurugenzi Fedha, Mkurugenzi wa Utaalamu wote wanafanya kazi kwa *teamwork*, Mkurugenzi wa Biashara na kitu kizuri ukifanya kazi kwa *teamwork* basi kinaleta faraja.

Kwa hivyo, naomba mtufanyie *faster* kwa sababu hiyo hapo Ramadhani, leo tutawaambia nini wananchi, kule wananchi wote wa Kiwengwa wote hawana maji, maji yao wanayokunywa si mazuri. Ramadhani hiyo hapo naomba sana tuwatafutie miundombinu ya hali ya juu haraka sana, pahali popote nenda au tandaza mabomba, wananchi waweze kufanya kitu. Tena Ramadhani mwezi mtukufu sana, na haya maji ndio unapata thawabu kubwa kila tone unapata thawabu.

Usione ajabu ukaambiwa huyo Mhe. Mshimba anakwenda zake peponi, kumbe nimejitahidi kwa suala la maji, kuwaondoshea wananchi dhiki, ukweli ndio huo kwani Makka unafikiria mbali, Makka mambo kama haya ukisaidia umeshahiji tusihangaike jamani watu wanaitafuta Makka. Anzia hapa sasa, watengenezee watu neema, nenda zako ukachukua nyengine kwa Mwenyezi Mungu huko Makka. Sasa hiyo ndio namna yenyewe, kwa hivyo mimi niseme kwamba nimefurahi sana na waendelee kutusaidia, na ziara yao ya Jumamosi wasiisahau waendelee kwenda kwenye ziara yao.

Mhe. Mwenyekiti, ukurasa wa 30 Idara ya Nishati na Madini, hapa nilisema mimi na niliomba dua usiku wake Mkurugenzi akatangaziwa, lakini bado hatujawawezesha vizuri.

Ningeomba sana Mhe. Waziri wa Fedha na hawa wakakaa kitu kimoja au mipango ya kupanga ile kodi ya fedha wakaachiwa, hawa kwa sababu tayari tushakuwa na idara maalum. Sijui Waziri wa Fedha anaona busara ipi zaidi, lakini najua yeye ni mtaalamu zaidi ataona bora niwaachie yeye hana uchoyo huo, yeye la msingi mumkusanyie mapato mumpelekee tu na yakifika kule mwenyewe anayaziba vizuri hayavuji. Hiyo ndio sifa yake. Mapato hayavuji kwake, atakayesema yanavujisha mimi nasema wewe tangu humpendi huyo hata siku moja, niseme ukweli.

Kwa  hivyo, mimi naomba sana hii wizara bado hatujaitendea haki, kuna mambo mengi ya uchimbaji wa mafuta, ya usimamizi wa mafuta lakini yeye katika upangaji tu wa bei hahusiki. Sasa na hili tumuachieni mwenyewe apange kila kitu, na ndio maana awe na *power*. Hawa watu tizama wanavyotuchezea mafuta, mara utasikia hakuna, awafungie mara moja watu kama hawa. Wanafanya uzembe, mafuta yatakuwa hayaji *quality*. Lakini ninachotaka kukwambia sasa hivi kuna wawekezaji wamepata maeneo, kuna mwekezaji mmoja ni Mkurugenzi wa *Vigor* amepata eneo zuri la *deep sea*, hebu tukae nae huyo, serikali isihangaike ili waweze kulitengeneza hili suala.

Kwa kweli amejitahidi sana kijana Taufik, eneo zuri tu, tumwambie tatizo lako liko wapi anachukua mafuta sasa hivi, ile itakuwa ni *centre* ya *East Africa deport* kubwa. Bei zitapungua, na yatakuwa ya *quality*, kwa nini tusimpe *power*.

Tunahangaika, tunakwenda kule Mombasa tunapanga *queue,* ile *queue* Mombasa hata ukiunganisha mpaka Zanzibar meli zinaweza zikafika kwa *queue* ile. Lakini leo hapa hapa anakwenda mtu pale ananyonya mafuta anatoka anakwenda ku-*supply* kwengine hata.

Mheshimiwa kwa kweli ni suala ambalo linafurahisha sana, mimi naamini hata ukimuona Mhe. Mazrui anatikisa kichwa hapo ujue hili suala kalifahamu na ni kweli kwa sababu ni mwekezaji ambaye aliyekuwa ni kijana nambari *one* katika nchi hii.

Tuwapeni wazalendo kwa sababu mzalendo unayempa miradi kama ile, zile fedha zinakuwa zinakaa pale pale nchini tofauti na watu wengine. Watu wengine wanakwenda kutumia kwao lakini mzalendo pesa zile tunazipata wenyewe hapa. Kwa hiyo sioni tatizo nitasikitika sana nitapokaa nje huko sijaingia Barazani, lakini nikirudi sikubaliani nalo suala hili kwa sababu wazalendo sasa hivi tuwape nafasi ya mbele kabisa na wakitaka waniwezeshe.

Kwa mfano, nirudi kwenye Mji Mkongwe kidogo alikuwa na sehemu aliomba siku nyingi sana na *wallahi* sehemu ile pale *Africa House* angepewa ingekuwa *half London,* usingekubali kama ile ni Zanzibar ndani ya ramani, panataka kuwekwa vizuri na ile sijui mpaka lini na imefikia wapi.

Mkurugenzi wangu wa mambo ya mji hana tatizo alikubali, lakini inavyoonesha mpaka leo kuna tatizo fulani. Tuwapeni hawa watu jamani wanataka kuigeuza Zanzibar iwe ya uwekezaji wa uhalisia, mimi naamini tusaidiane kutokana na hali ya shughuli hizo.

Mhe. Mwenyekiti, niingie Shirika la Umeme, nakaribia kumalizia. Hapa ndio kwenye roho. Mimi nafikiria Mhe. Waziri sijui unapokuwa kabla hujachaguliwa, nakuona unaoteshwa ata sijui kwa sababu umechaguliwa kuwa waziri, lakini niseme umechagua na wachezaji kwa sababu wewe niseme ni kiungo pale namba 8. Namba 8 anapandisha na anashusha na anachagua wepi *player* wa kuweza huyu unamkisia, huyu nikimpa pasi fulani atakuwa mzuri na huyu nikimpa *short* kuna na *long*. Hiyo moja umeangalia, ili kuweza kufanikisha.

Mhe. Mwenyekiti, nimeanzia wizara yako kote kuzuri sasa tunaingia hapa kwa mfungaji *ZECO,* ni mfungaji magoli kabisa maana kama huna umeme hujawa, umeme ni muhimu. Niondoke namba 6 pale alikuwa mtu wa maji…

**Mhe. Mwenyekiti:** Mheshimiwa una dakika tano ya kumalizia.

**Mhe. Makame Mshimba Mbarouk:** Dakika tano zinanitosha ndio namalizia sasa hivi hapa.

Mhe. Waziri nikupongezeni kwanza kwa suala moja kubwa sana la kuwasaidia wanyonge kwa kuwapatia umeme wa mkopo, *wallahi* umeota ndoto pale Mhe. Waziri, umeota ndoto pale kubwa sana wewe hujui mpaka Msikitini huko unaombewa dua tu, kutokana na lile jambo lipo, kwa sababu mnyonge anataka kutajirika kwa kupata umeme. Lakini unavyomuona wewe mnyonge yule hauwezi ukamfika, umemwambia njoo ukope sasa.

Halafu meneja wako anafanya kazi nzuri, pamoja na timu yake si mchezo. Kila panapotakiwa umeme wanapeleka umeme, wanapeleka nguzo, wanafanya kazi kwa pamoja. Yale majungu yamekwisha sasa hivi.

Mhe. Waziri nikushukuru sana na endelea hivyo hivyo tukushukuru umetusaidia, viongozi wengi humu kuwasaidia nguzo kuwapelekea kwenye majumba yao kwa njia hiyo ya mkopo, ungekuwa hujafanya hivyo tungeumia sana. Kwa hivyo, nikushukuru sana endelea na jitihada hizo. Namuomba sana meneja aendelee, afunge magoli tushinde kwenye ligi kuu, namuomba sana amalizie hilo.

Sasa namalizia, kabla sijasahau nimpe pongezi kubwa sana katibu wangu. Katibu wangu ndiye *over roll* wa wizara hii, huyu ni *centre half* wake ambaye ana-*cover* nyuma, anazuia kusitokee tatizo.

Mkurugenzi huyu pamoja na rangi yake aliyokuwanayo hana majivuno, hana maringo, tizama sasa kazi nzuri anayoifanya Mhe. Waziri kwa sababu wanakubaliana na katibu wake wanazungumza vizuri, wanapanga vizuri, wanakosoana kistaarabu na wanafika pahali wanakubaliana.

Mhe. Waziri nimpongeze sana kwa katibu huyu aliyekuwanaye, mtu mwenye hekima, busara, mimi namjua sio jana na leo ni zamani sana, tena huyu nimekabidhiwa na Mhe. Waziri wa Fedha wakati huo Mhe. Amina Salum Ali, alinikabidhi fanya naye kazi huyu na ni kweli nimeona matunda yake. Alikuwa anatusaidia kwenye jimbo letu la Kwahani kipindi kile na akitupa wahai mzuri wa kustawisha utendaji wa kazi.

Mhe. Mwenyekiti, nimeona na yeye nimpe nafasi yake, nimpongeze sana sana azidi kutumia nafasi yake vizuri kwa kumsaidia Mhe. Waziri. Hiyo nimeona nimgaiye yeye *special* kwa kumpa pongezi.

Vizuri zaidi makatibu wengi baadhi yao ukiwapigia simu wanaringa hata mawaziri wengine hawapokei simu, sisemi uongo niseme ukweli mtu hajui kitu gani,

hapokei simu. Jamani tukipiga simu hatuombi pesa kwao, pengine kuna kitu tunataka tusawazishe.

Yeye mpigie simu yuko Ulaya atakutumia *message* ndugu yangu niko pahala fulani, huu ni moja ya utendaji mzuri unafanikisha, sijui kwa nini wakurugenzi wengine hawapokei simu ukweli tuseme. Sijui kwa sababu gani, hatukuombeni pesa kuna kitu tunataka tufanyiwe marekebisho. Sasa mimi nimsifu kwa hilo kwa simu yuko *faster*, yeye hajali nani, haulizi kapigiwa na nani anaitikia.

Kwa hivyo, mimi hilo nisimpunguzie madaraka yake, nimpe haki na *Inshaallah* Mwenyezi Mungu atamjaalia hata akitaka jimbo la Kitope naweza nikampa, hamna tatizo lolote.

Mhe. Mwenyekiti, sasa nataka kuunga mkono, Mhe. Waziri na yeye namsifu sana kwa utendaji wake na umahiri wake, ukarimu na ukimwa wake na *Inshaallah* Mwenyezi Mungu na yeye atamjaalia kila la kheri, atampa lenye kheri na kumuepushia la shari na *Inshaallah* kwa Mwenyezi Mungu tutakuwa pamoja penye uhai na uzima.

Naiunga mkono, naomba sana waheshimiwa wenzangu sikushawishini lakini panapo kasoro turekebishe na tuweze kuipitisha siku ya Jumatatu kwa vizuri kabisa, mchangie kwa wingi sana ili Jumatatu tuipitishe.

Mhe. Mwenyekiti, naunga mkono kwa asilimia mia moja. Ahsante sana.

**Mhe. Jaku Hashim Ayoub:** Mhe. Mwenyekiti baada ya kumshukuru Mwenyezi Mungu aliyeniwezesha kusimama hapa na kuweza kupumua kwa pumzi zake alizoniazima. Naweza kushukuru kusema *Alhamdulillah*.

Mhe. Mwenyekiti, Wajumbe sote humu tuko sawa hakuna mkubwa wala mdogo, tafauti yetu ni umri tu, katika maamuzi ya kiti chako yanapohitajika maamuzi yanastahiki uyapime na utolee maamuzi.

Baada ya hapo Mhe. Mwenyekiti, niendelee kumshukuru Rais wa Zanzibar Dkt. Ali Mohammed Shein kwa jitihada anazozichukua kwa wananchi wake wa visiwa hivi vya Unguja na Pemba, ikiwa mambo mengi tu amefanya na akiwa msikivu.

Vile vile nichukue fursa hii kumpongeza Makamu wa Kwanza wa Rais, Maalim Seif Sharif Hamad kwa jitihada zake vile vile. Nitakuwa sijamfanyia haki kiongozi wetu wa ndani humu Mhe. Balozi Seif Ali Idd kwa jitihada anazozichukua na anavyomshauri Mhe. Rais kwa majukumu.

Pia niungane na Mhe. Makame Mshimba kwa kummwagia sifa katibu wa wizara hii Ali Khalil Mirza, naweza kusema katika makatibu wanaoweza kushindana yeye na katibu wa Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais, Dokta Omar Dadi Shajak nafikiri wanashindana kwa utendaji hawa, wanastahili sifa kwa hali ya juu.

Katika makatibu ambao wanapiga kazi; hawajali usiku, hakuna mchana, hakuna Jumamosi, hakuna Jumapili utamkuta katibu mpaka Jumamosi pale gari yake iko chini anapiga kazi, jinsi wizara ilivyokuwa ngumu, wizara nzito kabisa hii.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nitoe masikitiko yangu sana kwa Mhe. Waziri, kuna msemo unasema "Utakachokipanda ndicho utakachokivuna", kama utapanda shokishoki huwezi kuja kuvuna doriani. Mhe. Waziri nilikuwa nikipiga kelele sana kuhusu simu yake kuwa haipatikani, unapompigia hapokei sijui tatizo liko wapi.

Sisi Mheshimiwa asifikiri kama tunahitaji kiwanja au nyumba, kuna mahitaji mengine muhimu jimboni apokee simu halafu amwambie tu mtu kiutuo kuna tatizo gani, aipokee baadae mtu amjibu baada ya siku tatu au nne. Katibu Mkuu wake yuko Uingereza atakutumia *message*.

Mhe. Mwenyekiti, haya ni masikitiko nasema humu ndani, tumo sawa hakuna mkubwa, hakuna mdogo kwa mujibu wa sheria hatuwezi kuzarauliana, aliyekuwa mbora ni yule anayetii amri za Mwenyezi Mungu, asimdharau mtu humu tuko sawa. *(Makofi)*

Mimi nimpongeze sana Katibu Mkuu kwa jitihada anazochukua. Mhe. Makame Mshimba alizungumza yuko kwenye kikao anamtumia mtu *message*, huu ndio uungwana na haya ndiyo malezi yetu ya Kiisilamu. Sasa matokeo yake nini, hasara yake?

Watendaji wamerithi tabia hizi hizi, unampigia simu mkurugenzi hakujibu ndio pale niliposema utachokipanda ndicho utachokivuna. Unampigia simu mkurugenzi hakujibu. Siku moja Naibu Waziri nilimkuta analia humu ndani anamtafuta mkurugenzi ili amsaidie hoja ya kujibu ndani hakukuwa na mashirikiano, Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais anakamatia hapa, ili kuokoa jahazi. Ndio yale niliyosema humu tumo ndani sote tuko sawa, hakuna mkubwa hakuna mdogo.

Mhe. Waziri hizo ni nasaha zangu wala asifikirie kama namuonea wala vipi, haya yako wazi na yanaonekana sio yangu mimi tu.

Mhe. Mwenyekiti, nije katika mchango wangu kuhusu maeneo ya Mji Mkongwe, ujenzi wa Mji Mkongwe. Mkurugenzi usije ukashituka huko, Mhe. Issa Makarani,

wala usije ukashituka kabisa mimi siko huko. Kuhusu ujenzi vibali vinatolewa kwa utaratibu unajua wakati ni mali, wakati ni ukuta, utaratibu wa ujenzi Mji Mkongwe mnapotoa kibali bora tukijue kimoja kimalize kile kile, sio kesho unapanda ngazi leo ukajenge tofali, kesho boriti, kesho *fence*, kibali kikitoka bora kitolewe kimoja, bora kiwe shilingi milioni sita au tano lakini gharama yake ijulikane; lakini kutoa vibali robo, nusu, robo tatu mpaka kikamalizika ni usumbufu kwa wananchi.

Vile vile kwa upande wenu mimi naona mna majukumu mengi Mji Mkongwe, barua ile uandike *stationaries* zinapotea, nguvu zinapotea, toeni kibali kimoja kifahamike kiwe cha *fence*, tofali, jiwe, boriti, mbao, bati, madirisha, huu ndio utaratibu uliokuweko Baraza la Mji. Jaribuni kufuata *formula* hiyo ni ushauri wangu, lakini mna hiari kuufuata au kutoufuata huu ni ushauri. Wananchi wana majukukumu mengi kwenda pale wakenda wakafuata kibali kile haiwezekani ni ushauri *take point* kama utaweza kuifuatilia.

Jengine, wazee wetu huko nyuma walikuwa wakipata shida na sisi tusiende na *formula* ile na huu ni ushauri mwengine wa pili. Nyumba kujenga kwa mawe wakati huo tofali lilikuwa halipo nchi hii, hata wazee wetu au bibi zetu walikuwa wakivaa tunguja kwenye masikio ndio urembo wakati huo, uliokuwepo hawakuyataka yale, ile ni shida.

Tunguja sijui kwa kwetu inajulikana mfano wa nyanya wanatia masikioni humu inaning'inia, hawakutaka urembo wa tunguja wakati ule ni dhiki. Leo tofali lipo mwananchi yule anaambiwa akajengee jiwe, wengine wajengee matofali; ni kitu cha kusikitisha, dunia sasa hivi imebadilika tunakwenda na wakati mnaona sasa hivi, tuna mitandao ya simu, tuna kompyuta, tunarahisisha mambo na hili si suala la *UNESCO* la mawe. Tofali sio suala la *UNESCO*, tumeona humu mambo mengi lakini mnyonge mnyongeni hii ndio hali ilivyo.

Utaratibu ule wa kujenga kwa mawe mimi nafikiri ishafika pahali uwe marufuku hivi sasa unasumbua watu. Mandhari inachafuka, mashimo yanachimbwa kila siku mawe zitajengwa nyumba ngapi. Huu ni ushauri wangu kama ujenzi mtaukubali huo ujengwe kwa matofali kama wengine wanavyoendelea, mna haki ya kuufuata au kuuwacha.

Baada ya hapo nije katika Mji Mkonge; katika kitabu hiki nafikiri imepewa majukumu ya kusimamia. Naomba ninukuu ukurasa wa 19 kifungu 49.

Kifungu cha 49 kinasema kwamba:

"Mhe. Mwenhyekiti, Mamlaka ya Uhifadhi na Uendelezaji wa Mji Mkongwe ina jukumu la Uhifadhi wa Urithi wa Kimataifa wa eneo zima la

Mji Mkongwe, ukijumuisha urithi wa kihistoria wa majengo, utamaduni wa asili, mandhari, ...".

Sasa nije hapo kwenye mandhari. Hivi kweli bandari ile pale makalbi yale ndio mandhari kweli yale? Hili ndilo tulilokuwa tunalipigia kelele siku zote. Nafikiri Mji Mkongwe hili mmeliona, njia ile mliifunga mlipokuja kuona ukweli dhahiri, njia ile mkaja mkaifungua mkaona faida yake. Maana yake vigezo mnavyokuja kuvitoa humu ndani wananchi wanafahamu na sisi wawakilishi hatukuwa tunasinzia humu ndani. Mwaka jana, mwaka juzi, nahoji naambiwa ili majumba yasije yakaporomoka kwa msongo wa magari.

Kuna njia kama ile ya Posta nyumba zimekutana karibu au jumba la kulelea watoto, gari zinapita chini jumba lile halijapata *crack* mpaka leo. Mambo mengine tuyapime tukiambiwa mkijenga hoja hii sisi Wawakilishi wengine tunazifuatilia, tuko makini hatuji kwa kubahatisha.

Kwa yale makalbi niwaombe Mji Mkongwe kama ndio mandhari kweli yamependeza pale sura ya nchi, kioo kiko pale pale katikati ya mji, wananchi, watalii wanapita pale. Ndugu zetu wa Tanzania Bara wanakuja pale kuja kutizama mandhari ile, makalbi yale mimi nafikiri Mji Mkongwe muyafuatilie.

Mhe. Mwenyekiti, kuna maneno mengine labda niweke akiba unajua binadamu usije ukayamaliza yote kuzungumza. Kuna mambo mengi ya Mji Mkongwe lakini mengine itabidi niyazuwie, nisije nikatoa maneno yote mengine ya akiba.

Kuna barua hii nimshukuru sana Kaimu Waziri hili suala limekuwa la muda mrefu lakini sijui kama hakuna kalamu ofisini, hakuna karatasi. Naomba ninukuu Mhe. Mwenyekiti.

"Maswali na Majibu Baraza la Wawakilishi, tafadhali husika na mada ya hapo juu. Kwa barua hii naomba kuleta *hansard* ya majibu uliyoyatoa katika kikao cha Baraza la Wawakilishi siku ya tarehe 25 mwezi wa Machi wakati nikijibu swali Nambari 49 la Wizara ya Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati. Naomba uipokee na kuifanyia kazi kwa mujibu wa taratibu na sheria zinazohusu ujenzi wa Mji Mkongwe".

Nashukuru, nimshukuru sana Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais na sijui yuko wapi, maana yake hata ningependekeza kwa utendaji wake kwenda kuchukua fomu ya Urais na mimi nikam-*support* kwa utendaji wake makini.

"Sheria za Uhifadhi wa Mji Mkongwe wa Zanzibar zimeweka kikomo cha idadi ya ghorofa kwa majengo yanayojengwa kwa kukarabati ghorofa tatu. Hivi karibuni tumeshuhudia majengo zaidi ya ghorofa tatu yakijengwa katika mji huo.

(a) Wizara kazi yake kusimamia sheria au kuvunja sheria kutokana na ujenzi kutofanyika na viongozi dhamana wanashuhudia.

(b) Kwa nini wafanyabiashara wakubwa na wawekezaji wanaruhusiwa kujenga zaidi ya ghorofa tatu na wananchi wanyonge wakikatazwa na sheria hiyo hiyo. Kitendo hicho si ubaguzi wa Katiba ya Zanzibar na inasema binadamu wote sawa mbele ya sheria.

(c) Kufanyika kwa vitendo hivyo bila ya viongozi dhamana kuchukua hatua tunajenga msingi wa utawala bora au tunabomoa".

Barua hii imeshakaa miezi na miezi na jawabu imeshaji-*commit* mwisho wake, wananchi wanataka kuingia Mahakamani serikali ipate hasara. Katibu Mkuu sijui barua imefika wapi, hii nakala ya Katibu Mkuu kama imekwenda Mji Mkongwe imepata kitanda, iko *ICU* haijulikani. Barua tu hiyo miezi sita, hakuna lililojibiwa na humu wameshaji-*commit*.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais alizungumza humu akimsaidia Mhe. Waziri na hili swali niliomba muda mrefu mimi halijapata jawabu. Nasubiri subiri hatimae likapata jawabu. Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais alijibu hivi:

"Pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati naomba niongeze majibu kwa Mhe. Jaku Hashim kama ifuatavyo:

Mhe. Naibu Waziri kama alivyosema kwamba serikali inaendeshwa kwa mujibu na taratibu za kisheria inayotokana na Katiba iliyopo na haina nia yoyote ya kubagua katika eneo lolote ikiwemo sekta ya ujenzi, hakuna mwenye fedha au asiyekuwa na fedha sheria ni msumeno na utaratibu lazima ufuatwe.

Mhe. Mwenyekiti, pale ambapo eneo tupu la ujenzi unaruhusiwa kwa ghorofa tatu, pale ambapo eneo tupu lipo tupu ujenzi wa ghorofa tatu".

Sio maneno yangu hayo *hansard* hii hapa Mhe. Waziri pale ambapo nyumba zinategemea idadi za ghorofa ziliopo ili ziwezwe kukisiwa ujenzi ule. Hii barua imepata kitanda Mhe. Waziri nitahitaji maelezo ya kina na ya ufafanuzi.

Nikitoka hapo nije katika Mamlaka ya Maji (*ZAWA)*. Kwanza nichukuwe fursa hii sana kumshukuru Mkurugenzi Mkuu na watendaji wake nitakuwa sijawafanya haki hata kidogo, panapo ukweli tuzungumze ukweli. Mkurugenzi Mkuu Sheikh Mustafa amefanya kazi kwa umakini wa hali ya juu, kabisa kwa kipindi hiki nilichomfahamu na mashirikiano makubwa sana uliyonipa kwa wananchi wangu wa jimbo la Muyuni. Nimshukuru tena vile vile Mkurugenzi Fedha, Ali Tamim amejitahidi sana kwa upande wangu kwa hali na mali. Hata fundi mkubwa bwana Eliasi amejitahidi sana na ndugu yangu Maulid amejitahidi sana.

Niwaombe sana katika Wawakilishi, nafikiri mimi sitofika namba tatu, nne sina nia ya kujisifu lakini katika kipindi changu katika jimbo langu nimewekeza karibu shilingi milioni mia moja zinaweza kukaribia kwenye suala la maji. Namshukuru sana Mkurugenzi wa Maji inapofika pahali ananambia bwana leo uwanja una maji hauchezeki katafute maarifa mengine, nakwenda kununua *pump* za maji kwa wananchi wangu wa Jimbo la Muyuni.

Sasa niombe tu kidogo Mkurugenzi na hili nafikiri atalifikiria kuna bili hizi nimeletewa za wananchi wa Jimbo la Muyuni ikiwemo Pete, Kitogani, Muongoni, Paje, Jambiani, Bwejuu, mngezifikiria kama mimi mwananchi na nimechangia kwa kiasi kikubwa kwenye sekta hii ya maji muwafikirie angalau ile mifereji ya nje isije ikafika pahali ikataka kulipiwa ile, ni mifereji ya wananchi wote na inapokuwa mibovu yote nahudumia mimi mwenyewe, kama hapo mwanzo ilivyokuwa. Hii mifereji ningeiomba sana serikali kwa upande wangu na nimejitahidi na anaebebwa hujikaza.

Kwa hiyo, mifereji ya wananchi wangu wa Muyuni nitapoondoka mimi mnaweza kutafuta utaratibu mwengine. Lakini kwa hivi sasa nimejitahidi sana sekta ya maji kuisaidia kwa nguvu zote na inapokuwa *pump* haipo, mimi sirudi nyuma najua Mamlaka ya Maji ina majukumu na Mwakilishi siko peke yangu wanahitaji msaada kwengine. Lakini ananambia kuwa hili litachukuwa miezi mitatu, miwili, ananambia ukweli namshukuru ni muungwana, huenda kutafuta *pump* na kuipeleka. Sasa wananchi wangu angalau wajisikie kwenye huduma hii.

Kwa hivyo, nimuombe Mhe. Waziri atakapokuja alitolee ufafanuzi na amuulize Mkurugenzi kweli huyu Mhe. Jaku anayoyasema au anajisifu tu. Maana nisijekuwa najisifu tu, amuulize Mkurugenzi wake kiasi gani tumeshirikiana kwenye suala hili la sekta ya maji na wanathubutu hata wananchi, mimi jimboni kwangu wananiita Mwakilishi Maji tu. Kwa hayo niliyoyafanya naitwa umaarufu wangu Mwakilishi maji.

Nimetoa maji kutoka Unguja Ukuu mpaka Pete, nimetandika mipira karibu mipya. Miaka sita wananchi wa Pete hawajapata maji hilo liko wazi na linaonekana. *Pump* nimenunua pale nimekujenga kisima tu ni cha serikali, lakini kibanda nimekijenga, nimekiezeka na wananchi wanafaidika na maji.

Kuna *pump* Kitogani karibu mbili nimeshanunua mimi. Jamani nimeshanunua mimi, Muyuni nimeshanunua. Kwa hivyo, atakapokuja kutoa uamuzi mimi niombe sana wananchi kutokana na hali ya maisha na dola ilivyopanda basi hata maji nayo tuyafikirie ile mifereji ya nje, ya ndani siwezi kuchukuwa jukumu.

Mhe. Mwenyekiti, nije katika uamuzi uliochukuwa hivi sasa kuhusu kufuta ardhi. Mhe. Waziri mimi nafikiri imefika wakati aangalie sheria kabla ya kufuta ardhi inasemaje. Sheria ya Ardhi ya mwaka 1992 kwenye kifungu namba 60 kinaeleza utaratibu. Kwanza kabla ya kufuta ardhi unatakiwa umwite mhusika umuulize kwa nini eneo lile hajaliendeleza na nafikiri hajamwita hata mtu mmoja, anaamua kufuta tu kupiga wino mwekundu twende mbele kwa mbele.
La pili, kama hakujiendeleza atupe sababu, sababu gani na unatakiwa umpe miezi kumi na nane, yaani mwaka mmoja na nusu, huwezi kufuta ardhi tu hivi hivi ya Mzanzibari. Haya yote naamini hujayafuata Mhe. Waziri.

Halafu chengine cha kusikitisha Mhe. Waziri, wewe ndie mwenye wizara, wewe umetembea sana, yaani katika waziri anaeongoza kusafiri nafikiri wewe ndio unaeongoza, hebu nenda hapo Botswana mwananchi anapewa kiwanja na pia anapewa laini ya maji, nguzo ya umeme mpaka laini ya simu unapewa Botswana tu hapo. Leo miundiombinu Tunguu hujaipeleka, hakuna barabara, hakuna maji unamfutia kiwanja mtu. *How come?* Haya ni masikitiko makubwa, miundombinu waziri hajapeleka kisha unamfututia mwananchi kiwanja, ndio ubinaadamu, ndio uungwa, ndio utaratibu waziri unaofanya huu.
Mwananchi hana kosa kule maji atajengea nini, hujampelekea miundombinu, leo unakifuta kiwanja hii si haki unayofanya na cha kusikitisha zaidi watendaji wako mawaziri umewafutia viwanja, tena unatafuta njia za kugombanisha unampa waziri huyu, unampata waziri huyu, *how come?* Hapo nyuma hayakutokea Mhe. Waziri, sasa unataka kugombanisha waziri kwa waziri, leo viwanja unavifuta, hakuna miundombinu, hakuna barabara na hakuna maji, atajengaje mwananchi yule, uhalali kweli huu?
Mheshimiwa, hapa tutabadilisha mawaziri siku zote wizara hii. Atatoka huyu, anakuja huyu, hapawezekani, hapo nyuma kulikuwa na utaratibu wa ugawaji wa viwanja, kulikuwa na kamati maalum inapendeza kugawa viwanja. Hii migogoro inatendelea na itaendelea, haishi.
Mhe. Mwenyekiti, nije kwenye Shirika la Umme. Niendelee kushukuru sana Shirika la Umeme kwa jitihada wanazozichukuwa. Lakini niwaeleze tu kuna matatizo mawili, matatu katika jimbo langu. Kuna umeme wa mkopo wananchi

wangu wa Paje, Jambiani, Bwejuu na Muyuni, sijui imefika wapi na watu wamekwenda na kurudi hakuna hatua inayoendelea. Kuna nguzo Mjimkongwe nazo zimeanguka nazo muda mrefu zimekaa hazijapitiwa hata kuondoshwa wala kufikiriwa. Mkopo ule wa masharti nafuu uko wapi, wananchi wanafaidika nao wipi.

Mhe. Mwenyekiti, kwa kumalizia nije kwenye suala la maji la wananchi wa Michamvi. Huu mwezi wa Ramadhani unakaribia na maji ni uhai wa kila mwanadamu au kila kiumbe hai kinahitaji maji. Niwaombe tu katika mwezi mtukufu wa Ramadhani kama ile ada itaendelea tena na wananchi wale waendelee kufaidika na hali ile na kama kutakuwa hali hairidhishi basi sisi tuko tayari kuchangia kwa wananchi wale, sio nia ya kutaka kujionesha.

Mhe. waziri, nikunasihi sana suala la kufuta ardhi uzingatie, vyengine vyote serikali mtakuja kuitia hasara Mwanasheria Mkuu tusaidie. Unafuta ardhi bila ya kumwita mtu, hajamuuliza kwa sababu gani unatakiwa umpe angalau mwaka mmoja na nusu, miezi kumi na nne, binaadamu na kule miundombinu hakuna, hakuna maji  wala barabara, unamfutia ardhi tu. Tutaendelea kugombana siku zote kwa suala hili wala hatupati ufumbuzi.

Mimi nafikiri kwa machache haya Mhe. Mwenyekiti, sina mengi ila niombe tu nipatiwe ufumbuzi wa kina kuhusu suala la ufutaji wa ardhi, maji katika jimbo la Muyuni, mimi nimechangia kwa kiasi kikubwa kwa wananchi wangu leo kujakulipishwa watu kama wale mifereji ya nje na muda wenyewe umekwisha walifikirie kwa jicho la huruma. Ile si kazi yangu kama Mwakilishi, mimi kazi yangu nije kuwasemea huko. Lakini huko nakutana na hali ya majukumu ya Mamlaka ya Maji kuwa ni mengi na Wawakilishi tuko wengi na majimbo mengi hawezi kunipa *priority* jambo hili, inabidi aangalie haki iko wapi kila mtu anastahiki, leo atanipa kesho *pump* yenyewe itaharibika.

Baada ya maelezo hayo Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru sana, sitounga hoja hii mkono mpaka nitakapopata maelezo ya kina, naweza kuiunga mkono hoja hii. Ahsante.

**Mhe. Viwe Khamis Abdalla:** Nakushukuru Mhe. Mwenyekiti, na mimi kwa kunipatia fursa hii asubuhi hii ya leo.

Mhe. Mwenyekiti, nichukuwe fursa hii nimshukuru Mwenyezi Mungu *Subhana wa Taala* kwa kunijalia leo hii nikasimama hapa nikiwa katika hali ya uzima.

Mhe. Mwenyekiti, nichukuwe nafasi hii nimpongeze Mhe. Waziri na watendaji wake wote kwa uwasilishaji wake mzuri na tumeuona.

Mhe. Mwenyekiti, nichukuwe fursa hii nimpongeze Mhe. Waziri kwa kutekeleza vyema ahadi ambazo anaziweka Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya hayo nianze na mchango wangu kwenye Shirika la Umeme.

Mhe. Mwenyekiti, niwapongeze wafanyakazi wa Shirika hili la Umeme kwa juhudi zao na jitihada zao walinazozichukuwa kwa kuwapatia huduma hii

wananchi wa Zanzibar. Mhe. Mwenyekiti, pamoja na pongezi hizo bado nina masikitiko yangu kidogo.
Mhe. Mwenyekiti, Shirika hili la Umeme siku hizi kumetokea na tabia ya kuzimwa umeme mara kwa mara hasa katika maeneo ya Jangombe. Mhe. Mwenyekiti, wanazima umeme kuanzia asubuhi mpaka saa tatu za usiku. Namuomba Mhe. Waziri, atakapokuja kwenye maelezo yake aje anipatie maelezo, ni tatizo gani linalosababisha katika maeneo haya ya Jang'ombe ya kuzimwa umeme kuanzia asubuhi tena siku za kazi mpaka saa tatu za usiku, tukiangalia kuna wafanyabiashara ambao huwa wanahitaji huduma hizi za umeme.
Mhe. Mwenyekiti, nikitoka hapo niende kwenye Mamlaka ya Maji *ZAWA*. Mhe. Mwenyekiti, niwapongeze wafanyakazi hawa wa Mamlaka ya Maji *ZAWA* kwa usimamizi wao mzuri wanaochukuwa kwa jitiahada zao nzuri wanazozifanya katika kuhakikisha kuwa wananchi wa Zanzibar wanapata maji.
Lakini niseme kama mimi mwenyewe nina masikitiko makubwa katika kijiji changu cha Kiuyu Minungwini Kigongoni, hii ni bajeti ya pili nasimama hapa nachangia, lakini bado mpaka leo tatizo lile halijaondoka ndani ya kijiji changu. Mhe. Mwenyekiti, wanawaka wa kijiji kile wanamenituma nije niwasemee kuhusu suala hili la maji ambalo kuwa linawasumbua katika kijiji chao. Mhe. Mwenyekiti, ndani ya kijiji cha Kiuyu Minungwini kuna kisima kimoja, kisima hicho kimoja cha maji kilipatikana kutokana na mradi wa *TASAF*.
Mhe. Mwenyekiti, kijiji cha Kiuyu Minungwini ni kikubwa sana kuna Mjini Kiuyu, Mjini Ole, Mjini Koongo, Mjini Fimbo, Mjini Kigongoni. Mhe. Mwenyekiti, kijiji hichi wananchi tulioko Sheha ya Kiuyu Kigongoni hatupati maji kwa wakati, hiyo siku yanayotoka maji yanatoka usiku wa saa sita hadi nane wakati wa usiku Mhe. Mwenyekiti, ni wakati wa kupumzika, si wakati wa kusumbuka na ukatafuta maji.
Mhe. Mwenyekiti, ukiangalia wanawake wa kijiji kile wengi ni wakulima, mchana wa kutwa wako kondeni wanatafuta maisha yawasaidie na watoto wao. Mhe. Mwenyekiti, hili ni tatizo kubwa sana, namuomba Mhe. Waziri, atakapokuja aje anambie tatizo hili litaondokaje katika hichi Kijiji cha Kiuyu Kigongoni.
Mhe. Mwenyekiti, kijiji hichi tuna maeneo makubwa, tuna maeneo mazuri ya kupatikana sehemu ya kichimbwa kisima. Lakini hili ni tatizo toka niingie kwenye Baraza hili tukufu jambo hili nalisemea na sasa hivi tayari nimeshatimiza miaka mitano, namuomba Mwenyezi Mungu anirejeshe ndani ya Baraza hili ili niweze kuwatetea wana kijiji hawa wa Kiuyu Kigongoni.
Mhe. Mwenyekiti, pamoja na tatizo lote hilo linalowatokea wananchi wale wanaopata maji usiku saa nane ikifika mwisho wa mwezi wanakwenda wanadaiwa malipo, hujatoa malipo unafungiwa huduma mpaka mifereji ya nje inakatwa na hivi karibuni nilisikia kuwa mifereji hii ya nje wamesamehewa wale wanaotumia na jamii wote, basi sijui kama hili ni kweli au maana sina uhakika nalo.

Mhe. Waziri, nadhani wewe ni waziri msikivu sana na unaetekeleza majukumu yako vizuri, nakuomba uwaonee huruma wanawake wale wa kijiji hichi cha Kiuyu Kigongoni waweze kupatiwa huduma hii ya maji.
Mhe. Mwenyekiti, nikitoka hapo niende kwenye Mamlaka ya Nyumba. Mhe. Mwenyekiti, wenzetu wa Baraza wameweza kutekeleza mkopo nafuu wa nyumba. Mhe. Mwenyekiti, kuna wafanyakazi wa Shirika la Umeme wanasumbuka kukodi vijumba vya watu, kwa nini serikali yetu haikai ikatafakari tukaanza na sisi kujengewa nyumba hizi ambazo kuwa zinakuwa na mkopo nafuu kama wenzetu wa Watanzania Bara ili wafanyakazi wa nchi hii na wao wakaweza kufaidika.
Mhe. Mwenyekiti, tunayo maeneo mengi sana ambayo kuwa zinaweza zikajengwa nyumba hizi ili wafanyakazi wetu na wao wakaweza kufaidika. Mhe. Mwenyekiti, pamoja na mchango wangu huo mchache, nitaunga mkono pale Mhe. Waziri, atakapokuja akanipa majibu ya kina kutona na masuala haya na mchango wangu huu ambao nimeuchangia.
Kwa niaba ya vijana wangu wa Mkoa wa Kaskazini Pemba naunga mkono asilimia sabini na asilimia thalathini litaziacha mpaka nikatapokuja majibu. Ahsante.
**Mhe. Mussa Ali Hassan:** Ahsante Mhe. Mwenyekiti, kwa kuweza kunipa nafasi ya kuweza kuchangia wizara hii ya Ardhi pamoja na mambo ya umeme.
Kwanza sina budi kumshukuru Mwenyezi Mungu kutufikisha hapa tukiwa wazima wa afya tukaweza kuendelea na shughuli zetu za leo kwa salama.
Mhe. Mwenyekiti, kwanza nimpongeze Mhe. Waziri, kwa shughuli zake nzuri alizozipanga katika wizara yake pamoja na watendaji ambao wanashughulika nae kwa shughuli za kazi za kila siku.
Mhe. Mwenyemkiti, kwa leo nianze kuchangia ukurasa wa 15 kuhusu masuala ya Idara ya Ujenzi. Mhe. Mwenyekiti, kwanza nampongeza Mhe. Waziri kwa shughuli za ujenzi ambazo zinafanyika nchini kwa wakati. Hapo hapo nimpongeze Mhe. Waziri, kuhusu shughuli na mambo mengi ambayo anashughulikia pamoja na hivi karibuni kwenda katika ziara yake ili kuhakikisha kwamba analeta maendeleo nchini kwetu.
Mhe. Mwenyekiti, nimsisitize Mhe. Waziri, kuhusu masuala ambayo aliahidi kuyatekeleza lakini hadi leo tunaona bado hayajatekelezeka hasa katika ujenzi wa jumla lile kubwa la treni ambalo liliahidiwa kufanyiwa ukarabati kwa muda mrefu sana kwa faida ya wananchi wanaokaa mle kwenye nyumba pamoja na wapita njia.
Mhe. Mwenyekiti, jumba lile ni la muda mrefu labla sisi wengi hatujazaliwa tumelikuta linaishi na linahatarisha usalama wa wananchi wanaoishi katika nyumba ile pamoja na wapita njia ambao wanapita, pamoja na wageni wa nchi mbali mbali. Namuomba Mhe. Waziri, suala jumba lile kuna usemi "Tusipoziba ufa tutajenga ukuta" kwa hatari ya nchi yetu.
Kwa muda mrefu jumba lile limesisitizwa, lakini tunasikia sababu ndogo ndogo ambazo kuna wananchi wamesema hawaondoki kwa sababu wanataka kuishi muda wote mpaka waporomokewe, tuna mifano mizuri ya majumba makongwe kule

mjini, hatari kama hizo zilitokea na wananchi wengi walipoteza maisha yao halafu inakuja kulaumiwa serikali pamoja na sisi wapangaji sheria katika chombo hichi.

Namuomba Mhe. Waziri, atakapokuja anihakikishie ni lini atachukuwa hatua ya majukumu ambayo amepewa na serikali kuhakikisha usalama wa wananchi anautekeleza kwa faida yetu sote. (*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti. vile vile, naomba kuchangia ukurasa namba 22 Mamlaka ya Maji. Kwa kweli serikali yetu inajitahidi sana katika utendaji au utekelezaji wa ahadi zake. Lakini hazifikii mwisho ili wananchi wakala keki ile kwa wakati mzuri. Mhe. Mwenyekiti, nakumbuka kwamba katika wilaya yangu pamoja na jimbo langu la Koani tumetekeleza ilani nzuri ya Chama Cha Mapinduzi kuhusu tatizo la maji, tumejenga mtaro mkubwa wa maji kupitia Mkorogo, Mwera Pongwe hadi kufukia kujenga tangi kubwa la kisasa Machui ambalo wamejenga ndugu zetu Wachina katika shughuli hizo.

Mhe. Mwenyekiti, ukweli kwamba shughuli hizo zimechukuwa muda wa zaidi ya miaka miwili zimeshamalizika. Kwa kweli Wachina wameshaondoka na tangi lile limeshakabidhiwa serikali. Lakini hadi leo wananchi hawajafaidika kula keki ile ya maji wakaondokana na matatizo ya makubwa ya maji ambayo yanapata Jimbo la Koani Wilaya ya Kati.

Wananchi wa sehemu ya Mkorogo, Mwera Pongwe, Machui walikuwa wanategemea sana kuhakikishiwa kwamba tangu 2014 iwe tayari maji yameshatoka, limefunguliwa tangi lile lakini mpaka sasa hata ile tone ya maji hamna kwenye matangi yale, sielewi kuna matatizo gani ambapo hadi leo wananchi wanasononeka sana na sisi tunawasemea hapa mbele ya chombo hichi cha kupanga sheria ukweli wananchi wanasumbuka sana. Wengi wanaokwenda kuliangalia lile tangi wanaliangalia kwa macho na kwa huzuni sana, kwa sababu kama lingelianza kazi zake wananchi wengi wangalifaidika na mtaro ule pamoja na matangi yale ambayo yamejengwa kwa faida ya wananchi.

Hivyo, namshauri Mhe. Waziri, akija atueleze ni sababu gani hadi leo tangi ile bado haijaweza kutoa maji kwa wakati uliotakiwa. Vile vile, wananchi wengi ambao walitoa sehemu zao kwa ajili ya kuhakikisha kupita mitaro ya maji ile hadi kufikia Machui hadi leo bado hawajapata malipo yao na kwa kweli wana matatizo makubwa kwamba tangu siku hiyo iliyopita mitaro hadi leo si chini ya miaka miwili hawajapa hata senti za kuweza kulipiwa kwa ajili ya faida ya kukimu maisha yao. Ukweli wananchi hao ni wa Mwera Pongwe pamoja na Mkorogo hadi kufikia kwenye tangi kubwa la Machui. Tunaomba Mhe. Waziri, ahakikishe kwamba anafanya kila awezavyo ili kuhakikisha kuwapunguzia matatizo wananchi kupata haki zao za malipo kwa wakati.

Vile vile, kuhakikisha kwamba wananchi wa Machui hivi sasa wanatapa tatizo kubwa sana la maji safi pamoja na vitongoji kwa kupitia sehemu ya Mwera Pongwe hadi Mkorogo ambapo lilihakikishwa kwamba tangi ile kama ingelikuwa inafanyakazi hivi sasa, ingelikuwa tatizo lile limeisha na imebaki simulizi tu

kwamba zamani kulikuwa na matatizo ya maji Machui au kulikuwa matatizo ya maji sehemu ya Pongwe na Mkorogo yake.
Namuomba Mhe. Waziri, achukuwe sehemu kubwa ya wakati wake kutembelea kila baada ya muda kama sisi tunavyokwenda katika sehemu ile lakini kwa vile hatuja ujuzi wa kuweza kuyatoa yale maji tunayaangalia tu na mara nyingi huwa tunalipiga picha. Hivi sasa ninayo picha moja ambayo niilichukua kuhakikisha kwamba lile *tank* ni kubwa, lakini halina maji ambayo yanayowasaidia wananchi.
Mhe. Mwenyekiti, kutokana na muda wako kwamba wengi wanataka kuchangia. Sasa niweze kuchangia ukurasa wa 35 kuhusu masuala ya umeme. Mhe. Mwenyekiti, nampongeza sana Mhe. Waziri kwa juhudi anazozichukua za kuweza kusambaza umeme vijijini pamoja na nguzo za umeme ambazo hivi sasa zimesambaa sana katika vijiji vyetu. Hilo ninampongeza, hivi karibuni kwa kuweza kunipa huduma kwenye Jimbo langu la Koani katika sehemu ya Mtakuja, Ungujaukuu-Kaepwani na Ungujaukuu Tindini. Hivyo, Mhe. Mwenyekiti, ninampongeza sana Mhe. Waziri, kwa juhudi zake na ukweli aliotimiza katika suala lake na hivi karibuni aliniahidi kabla ya uchaguzi mkuu wa 2015 atahakikisha kwamba sehemu ya Mtakuja pamoja na Ubago-uwandani kuwa ameshanipelekea zile nguzo ambazo tulizokubaliana. (*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti, kwa kweli suala hili ninampongeza sana pamoja na kutoa mashirikiano kwa umeme wa mkopo, kwa kweli amesaidia sana vijiji vyetu kupata maendeleo pamoja na umeme wa kileo. Hivyo, ninamshukuru sana na ninampongeza pamoja na watendaji wake, hivi sasa wana bidii sana, wameamka vizuri sana na ukenda ahadi zao zinakuwa sio za uwongo, wanakuhakikishia kwamba muda mdogo tu utapata huduna na ni kweli wanatoa huduma nzuri. Hivyo, Mhe. Mwenyekiti, ingawa Mhe. Waziri, alikuwa safarini nimpongeze vijana wake wanafanya kazi vizuri hivi sasa. (*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti, vile vile. suala kubwa ambalo tulikuwa na kilio kikubwa cha umeme *LUKU* hivi sasa, hili suala naona ameshalimaliza wakati muda mrefu ilikuwa mimi ninazungumzia naye kienyeji hadi kwenye Baraza ahakikishe kwamba anatumia teknolojia ya kisasa na hivi sasa kwa kweli umeme unapatikana kwa teknolojia ya kileo hata kwa kutumia simu zetu za kileo. (*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti, kwa kweli mimi mchango wangu utakuwa sio mkubwa sana kwa leo kutokana na muda wako ambao wenzangu wanataka kuchangia sehemu nyingi ambazo zinataka kutekelezwa na Wajumbe hao. Kwa kweli ninakubaliana na Wizara hii pamoja na wananchi wangu wa Jimbo la Koani kwa asilimia mia kwa shughuli zake zinavyotekelezwa.

Mhe. Mwenyekiti, ahsante sana. (*Makofi*)

**Mhe. Mwenyekiti:** Ahsante sana Mhe. Mussa, mchangiaji anayefuata ni Mhe. Hassan Hamad Omar baada ya hapo ni Mhe. Kazija Khamis Kona.

Waheshimiwa Wajumbe nafasi ipo baada ya Mhe. Kazija sina mtu, kwa hivyo, anayetaka kuchangia naomba alete karatasi hapa.

**Mhe. Hassan Hamad Omar:** Mhe. Mwenyekiti, na mimi nikushukuru sana kwa kunipa fursa hii kuweza kutoa mchango wangu katika Wizara hii ya Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati.

Mhe. Mwenyekiti, lakini kabla ya yote nimshukuru Mwenyezi Mungu *Subuhana Wataala* aliyenijaalia kuwa katika uhai, uzima na afya. Mhe. Mwenyekiti, nimpongeze sana Mhe. Waziri, Mhe. Ramadhani Abdalla Shaaban, vile vile, nimpongeze sana Mhe. Naibu Waziri, Mhe. Haji Mwadini Makame, pia nimpongeze Mhe. Katibu Mkuu wa Wizara hii na Naibu Katibu Mkuu Ndg. Mustapa Aboud Jumbe pamoja na Mkurugenzi Ndg. Januari Fusi kwa kazi nzuri wanayoifanya kwa mashirikiano mema, bila ya mashirikiano mema wangekuwa hawafikii malengo waliyofikia. Lakini hawa mimi ninawapa pongezi hizi za dhati kwamba mashirikiano yao ni mazuri, bila ya mashirikiano yao kungekuwa hakuna maendeleo, hakuna chochote kinachofanyika kwa sababu wameshikamana kila kitu kinaweza kufanyika kwa utaratibu wanaojiwekea. Mwenyezi Mungu awaalie waendelee na kazi za kuwahudumia wananchi. (*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti, nikiendelea na mchango wangu moja kwa moja ninajikita katika Mamlaka ya Hifadhi ya Mji Mkongwe. Mhe. Mwenyekiti, Mamlaka hii sina jengine ila ni kuwapongeza katika kazi kubwa iliyofanyika na sasa hivi tuna matumaini kama inaendelea, ni ujenzi wa ukuta ambao tayari tumeona bati yameshazungushwa kwa ajili ya kuanza ujenzi. Jambo lile ni zuri sana na *Inshaallah* utakwenda kama ulivyokusudiwa, basi pale patakuwa kama Ulaya kwa sababu mchoro tuliouona wakati nikiwa Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Mawasiliano na Ujenzi, tulikuwa tunalipigania hili na nimeshaona matumaini kama limefanikiwa. Mwenyezi Mungu awezeshe ukuta ule ujengwe na utakuwa na bustani nzuri, wananchi watafarijika sana. (*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti, lakini niende katika mchango wangu kwenye ukurasa wa 22 katika Mamlaka ya Maji na ninaomba ninukuu:

"Mhe. Mwenyekiti, Wizara yangu kwa kuzingatia malengo ya Milenia, Dira ya Maendelea ya 2020, Mkakati wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umaskini Zanzibar (MKUZA II), Sera ya Maji ya Mwaka 2004, Sheria ya Maji ya Mwaka 2006 na Maelekezo ya Ilani ya Uchaguzi wa

CCM ya Mwaka 2010 katika kipindi cha mwaka wa fedha wa 2014/2015, imetekeleza programu na miradi ya maji ifuatayo."

Kama inavyooneshwa hapo mimi nitaendelea na mchango wangu.

Mhe. Mwenyekiti, hili ni kweli katika miradi ya upelekaji maji vijijini, kwanza mimi ninashukuru Kojani ni kisiwa, lakini kisiwa kilichokuwa na dhiki ya maji kama Kojani ilikuwa inaongoza Zanzibar hii. Ilifika kipindi cha Ramadhani kama tunachoelekea mtu anakwenda maji kuanzia saa nane mpaka siku ya pili au ya tatu hajapata maji, ilikuwa ni usumbufu wa kutosha. Lakini tunashukuru Mwenyezi Mungu katuletea neema maji masaa ishirini na nne yanapatikana Kisiwani Kojani. Mhe. Mwenyekiti, na *pipes* zinazokwenda Kojani hazikuruhusiwa kutoboa sehemu yoyote, hili tunawapongeza sana, tunapata maji wingi, tunawashukuruni sana. (*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti, lakini niseme tu hakuna zuri linalokosa kasoro japo kidogo, wala hii si kasoro bali hawajafikia tu na *Inshaallah* Mwenyezi Mungu awawezeshe wafikie. Mhe. Mwenyekiti, katika Jimbo la Kojani kwenye Kijiji cha Gombeume pale wananchi wanapata dhiki ya kutosha mambo haya maji. Mhe. Mwenyekiti, wanakesha maji hayapatikani. Ila kuna mradi huu uliopita wa China unaoelekea Bahanasa huu, tunaomba na wale wananchi waunganishiwe maji kutoka huu mradi wa China nao watapata maji na alau watakidhi haja.

Lakini katika watu wanaokesha Kijiji cha Gombeume ni hatari kubwa sana. Mhe. Waziri, nipo tayari kushirikiana na wewe, lakini pale tupate maji na wananchi wale wafaidike na maji, wasiwe na dhiki usiku kutwa watu wanataka kuzaa, lakini bado wanakwenda katika maji hayapatikani, ni tatizo. Ninakuomba mashirikiano mimi na wewe, unipe muongozo wako tufanye hili jambo wapate wananchi wa Kijiji cha Gombeume.

Mhe. Mwenyekiti, kama haitoshi, katika mradi huu wa maji unaoelekea Bahanasa kupitia Mchangamdogo, Cairo, Vumba, Kijikani mpaka kufikia Bahanasa kuna watu walioharibiwa vipando vyao kwa kupitisha ule mradi na mpaka leo hawajapata haki yao, wengine tayari wameshalipwa, wengine hawajapata haki yao. Ninayo majina wala sitaki kuyataja kwa siku ya leo, lakini watu wanafikia zaidi 30 hawajapata haki yao.

Kwa sababu wengine wamelipwa na hawa waliobakia Mhe. Waziri, tunaomba nao wapatiwe haki yao, si vizuri sana kwamba wengine walipwe na wengine wasilipwe, hii itajenga chuki, tunaomba pasiwe na chuki. Tunaomba Mhe. Waziri, ufuatilie kwa ukaribu sana katika vijiji nilivyovitaja kuna watu wameathirika na mradi huu, ardhi ni mali ya Serikali lakini vipando ni mali ya mtu binafsi

anayejituma kutoa jasho lake. Kwa hivyo, hawa wapatiwe haki yao ya kimsingi na *Inshaallah* Mwenyezi Mungu atakuwezesha katika mafungu haya yaliyotengwa nao walipwe.

Mhe. Mwenyekiti, nikitoka hapo niende katika Shirika la Umeme. Shirika hili linathubutu kusema kwamba nao ninawapongeza sana, ninampongeza Meneja ndugu Hassan, ninampongeza Meneja aliyeopo tawi la Pemba kule ndugu Salim vile vile wanafanya kazi vizuri pamoja na watendaji wao wote wanafanya kazi vizuri tu. Ushahidi kamili kama mvua hizi za Masika zilizopita Mhe. Mwenyekiti, nyumbani kwangu mimi unapojua wewe, pana nguzo kubwa inayopeleka umeme pale nyumbani kwangu, nguzo ile waya ulianguka chini na nikajaribu kuwapigia simu, na wakaniambia Mheshimiwa tunakuahidi dakika kumi na tano tutafika.

Ninawashukuru sana baada ya dakika kumi na tano hazikumaliza wameshafika kwenda kulishughulikia tatizo ambalo ilikuwa ni hatari kweli kweli. Ninawapongezi kweli kweli na ninawaombeni mwende na mwendo huo huo, kwa sababu umeme ni kitu cha hatari, unapopata taarifa kwa mtu yeyote mulifuatilie suala hili kwa ukaribu kabisa, umeme ni kitu hatari kweli kweli. Mimi siku ile sikupata kwenda kazini bila ya kulishughulikia lile tatizo. Kwa hivyo, ninawashukuru sana. (*Makofi*)

Lakini vile vile katika tatizo hili hili lililonikuta mimi bado linaendelea katika nguzo hiyo hiyo, ile nguzo haina *stair* na niliwashauri watie *stair* kwa sababu hivi sasa imeinama na zile waya zinakuja chini. Kwa hivyo, naomba walishughulikie mara moja hili. Nikitoka hapa katika mambo haya *Inshaallah* itapita kwa nguvu zote hii, lakini zile nguzo ziwekwe kwa *stair*.

Mhe. Mwenyekiti, nimejikita katika Shirika la Umeme kupeleka umeme vijijini, tunawashukuru sana vijiji vingi vimeshapata umeme. Lakini Mhe. Mwenyekiti, ndani ya Jimbo la Kojani, kijiji chenye tatizo la umeme ni Kijiji cha Chambaje sehemu za Pembeni kwenye Jimbo la Kojani. Hawa wananchi wana hamu nao wapate alau mwezi huu wa Ramadhani nao wanywe maji baridi, wahifadhi vitu vyao vyengine *Alhamdulillah* kama wenziwao. Naomba nao muwaangalie kwa jicho la huruma wananchi wa Kijiji cha Chambaje, wana matatizo makubwa sana, lakini nina imani kwamba Shirika hili la Umeme wanavyokwenda watafanya hili na watalishughulikia na *Inshaallah* Mwenyezi Mungu awawezeshe tushirikiane, umeme ukija pale ufike katika Kijiji cha Chambaje.

Lakini Mhe. Mwenyekiti, niseme tu na niungane na mwenzangu Mhe. Jaku Hashim Ayoub, alivyochangia. Kama ili mambo yawe mazuri zaidi wananchi wetu ni maskini na tena ni maskini wa kutosha. Tumeomba ile miundombinu wanapoleta katika miji mipya basi miundombinu ipelekwe haraka sana, ikiwemo

huo umeme na maji. Mtu hana uwezo wa kuweza kuzitoa nguzo kama saba, nane akapeleka kama si mtu wa kampuni au tajiri wa kutosha, maskini ya Mwenyezi Mungu hawezi kupeleka. Miundombinu ipelekwe sehemu ile na iachwe sehemu ndogo tu kama pahala pa nguzo moja au posi, lakini umeme upelekwe ndiyo mambo ya maendeleo hayo. Mahali popote panapokuwa na umeme na maji, basi maendeleo hayakosi kuwepo. Lakini leo mtu atajenga sehemu inakuwa na matatizo.

Mhe. Mwenyekiti, ukiangalia katika kijiji cha makazi mapya Kojani umeshafika mbali *Alhamdulillah* tunashukuru, ni makazi ambayo yanaridhisha sasa hivi. Hebu jaribuni kuwapelekea wananchi sehemu ile umeme ili wafaidike na hili jambo. Kule mwahali kwa kwenda kisimani ni tatizo kwa kweli.

Mhe. Mwenyekiti, ninashukuru na kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Kojani ninaunga mkono kwa asilimia mia kwa mia Wizara hii katika hoja yake ya hotuba hii.

Mhe. Mwenyekiti, ahsanteni sana ninakushukuruni. (*Makofi*)

**Mhe. Mwenyekiti:** Ahsante sana Mhe. Hassan Hamad Omar, anayefuata ni Mhe. Kazija Khamis Kona na baadae Mhe. Hussein Ibrahim Makungu na baadae ajitayarishe Mhe. Salim Abdalla Hamad.

**Mhe. Kazija Khamis Kona:** Mhe. Mwenyekiti, ahsante sana na mimi kwa kunipa nafasi ya kuchangia hotuba ya Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati.

Mhe. Mwenyekiti, na mimi niungane na wenzangu kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia hali ya uzima na afya njema tukaweza kutekeleza majukumu yetu. Lakini Mhe. Mwenyekiti, naomba nimpongeze Mhe. Waziri, pamoja na watendaji wake wote kwa jitihada ambazo wanazozichukua kwa kuwatekelezea wananchi na kuwapatia huduma mbali mbali. (*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti, kwa kuanzia na mchango wangu ninaanzia na Idara ya Mipango Miji. Mhe. Mwenyekiti, Idara ya Mipango Miji ina jukumu kubwa sana la kutuwekea mji wetu vizuri ili uendane kutokana na ardhi yetu ilivyo, basi uendane na matakwa yetu yalivyo. (*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti, Wizara hii kama itafanya kazi zake vizuri na kutupangia miji yetu vizuri, basi nchi yetu itakuwa ipo katika hali nzuri. Mhe. Mwenyekiti, hivi sasa watu wanajenga tu kiholela jinsi wanavyojua wao na Idara hii ipo na tunaambiwa inafanya kazi zake ipasavyo. Sasa Mhe. Waziri, aje aniambie ni

sababu gani zinazopelekea kuwaachia wananchi kujenga kiholela wanavyoona wao inafaa bila ya kuwapa maelekezo yanayostahiki.

Mhe. Mwenyekiti, Idara hii kama itajipanga kutupangia miji yetu na katika miji hiyo wakatuwekea huduma za kijamii, mfano kama masoko kwenye miji yetu, njia ambazo zinazoweza kupishana gari, lakini pia wakatuwekea njia za kupitisha maji, waya za umeme ili tuwe na miji mizuri, lakini hili bado halijafanyika. Katika Mji wa Mombasa hapa zimepangwa nyumba vizuri lakini njia zake ni nyembamba sana. Sasa njia hii inapopita gari haziwezi kupishana. Sasa bado Idara hii haijafanya kazi ipasavyo.(*Makofi*)

Sasa naiomba Wizara hii Mhe. Mwenyekiti, ifanye kazi zake kwa kina ili tupange mji wetu vizuri, miundombinu ya maji na ya umeme ionekane vizuri na njia pia ziwe pana, zisiwe nyembamba kama zilivyokuwepo pale Mji wa Mombasa.

Mhe. Mwenyekiti, wakati umefika sasa katika nchi yetu kubadilika, kwenye ujengaji wa nyumba. Sasa hivi tubadilike kutokana na ardhi yetu ni ndogo sana, tuwe na mfumo mpya wa kujenga nyumba za ghorofa. Mhe. Mwenyekiti, tukifanya hivi tutapata maeneo ambayo ya kilimo na maeneo mengine, lakini tusipofanya hivi tutaendelea kulalamika kila siku. (*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti, sasa Mhe. Waziri, aje aniambie amejipange vipi kuhusiana na suala hili ili kuhakikisha sasa hivi mji wetu unabadilika kwa kujengewa nyumba za ghorofa. Pia, Mhe. Waziri, aje aniambie tuseme hii nchi yetu bado hawajatokea wawekezaji wenye kutaka kuwekeza katika kutujengea nyumba za ghorofa ili tubadilike, na kama bado ninamshauri Mhe. Waziri, kwamba ajitahidi kuwashauri wawekezaji kujenga nyumba za kisasa za ghorofa kama pana uwezekano hizi nyumba za chini chini zote zilizojengwa na wananchi kutokana na hali walizokuwa nazo kwa utaratibu wao wanaouona unafaa zikabomolewa zikajengwa nyumba za ghorofa, ikisha mwananchi akalipia kwa bei nafuu. Sasa Mhe. Waziri, namuomba Mhe. Wizara yake hili alichukue alifanyie kazi, ili tubadilike na mji wetu ubadilike.

Mhe. Mwenyekiti, nikiondoka hapo ninaendelea katika Mamlaka ya Maji. Mhe. Mwenyekiti, Wizara yake inajitahidi lakini bado kuna vijiji havijapata maji. Sasa Mhe. Mwenyekiti, katika jadweli namba tatu ameainisha hapa vijiji ambavyo vimesambazwa, kazi ambazo zimefanyika katika kipindi hichi, anasema uchimbaji wa visima kazi zimekamilika, usambazaji wa mabomba kazi hii ni endelevu.

Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Waziri, aangalie sehemu ambazo wananchi wanashida ya maji, shida ambazo ni ngumu, na katika sehemu nyingi wananchi wanatumia visima vya maji ya kuchota kwa kamba. Sasa hili ni tatizo, wananchi wetu bado

hawajafaidika na huduma hii. Kwa mfano, katika kijini cha Kijini, hapa anasema; Kijini, Nungwi kazi endelevu ya usambazaji huo wa mabomba. Sasa nimuulize Mhe. Waziri, usambazaji huu ingawa ni endelevu kwa maeneo hayo ya Kijini utaisha lini, ili wananchi wafaidike na huduma hii ya maji.

Mhe. Mwenyekiti, nilipata malalamiko kutoka kwa wananchi wa Matemwe, kwamba ilipopitishwa miundombinu ya maji, waliathirika kwa kiasi fulani. Kuna baadhi yao wamelipwa na wengine hawajalipwa fidia. Mimi nataka nimuulize Mhe. Waziri, aje anijibu, ni utaratibu gani uliotumika wa kuwalipa fidia wananchi hawa, ambapo wengine wamelipwa na wengine hawajalipwa na wengine nyumba zao zimepasuka. Sasa sijui hapa atawasaidia vipi wananchi hawa.

Pia, Mhe. Mwenyekiti, mradi huu uliokuwepo Kiashange, ambapo nikiuliza swali hapa naambiwa karibu utamalizika, karibu utamalizika. Je, ni lini hasa mradi huu utamalizika na wananchi watafaidika kupata maji, kwa sababu siku zimekuwa nyingi na tukiuliza tunaambiwa tusubiri sijui mradi huu karibu utamalizika. Sasa ni lini mradi huu utaanza kazi na wananchi wafaidike na maji.

Mhe. Mwenyekiti, kuna kijiji. Namuomba Mhe. Waziri hapa anisikilize kwa makini kinaitwa Kigomani. Hawa wananchi wa Kigomani wanafuatilia sana suala hili la kuhusu maji. Mhe. Waziri, hebu niambie kwa nini wananchi wa Kigomani hawapati maji ipasavyo. Kwa sababu kuna siku tulikwenda na Mhe. Naibu Waziri, wananchi hawa walilalamika, baada ya hapo tukalifuatilia suala hili. Tulichokigundua Mhe. Waziri, ni kwamba sehemu, kama ukiingia katika kijiji cha Kigomani kuna hoteli inaitwa Azaz. Huyo mwekezaji wa hoteli hiyo yeye anayavuta maji kwa pampu na kuingiza katika hoteli yake.

Pia, Mhe. Mwenyekiti, tulichokigundua chengine ni bomba la kuendea kwa wananchi wa Kigomani limezibwa. Sasa je, Mhe. Mwenyekiti, ndio kweli serikali hii inawajali wananchi wake au inawajali wawekezaji. Baada ya kulifuatilia suala hili kwa muda wa wiki mbili wananchi wale walipata maji, lakini hadi leo hii maji hawapati tena. Sasa je, mwananchi hana haki au sijui vipi, Mhe. Waziri, naomba uje unijibu na kama ana haki, kwa nini anapewa fursa mwekezaji kuziba bomba, wananchi wasipate maji na ayapate yeye. Mhe. Waziri, naomba uje unijibu ili nikikutana na wananchi wa Kigomani niwaeleze na wao kama wanasikiliza wajuwe vipi watasaidiwa. Maana kila siku wanakuja katika Mamlaka ya Maji.

Mhe. Mwenyekiti, kuna mwananchi mmoja alifika mpaka kuchukua maji ya Kigomani na kuyaleta katika Ofisi ya Mamlaka ya Maji, akaambiwa Mkurugenzi anywe ayaonje kutokana na shida wanazozipata wananchi. Kwa hivyo, Mhe. Waziri, kama wananchi hawajachukua hatua zisizostahiki basi naomba suala hili lifuatiliwe ili tuhakikishe wananchi wanapata maji safi na salama.

Mhe. Mwenyekiti, vile vile, usambazaji wa umeme vijijini na wananchi wa Jimbo la Matemwe, katika kijiji cha Kijini na Kandwi na wao hawajafaidika na huduma hiyo. Kwa hivyo, namuomba Mhe. Waziri, aje aniambie ni lini wananchi hao watafaidika na matunda ya Mapinduzi ya Miaka 51 kwa kupatiwa huduma ya umeme.

Mhe. Mwenyekiti, nikiondoka hapo kuna jadweli hapa katika ukurasa wa 22, kuhusu ukaguzi wa nyumba ndani ya eneo la Mji Mkongwe. Mhe. Mwenyekiti, nyumba hizi tumeambiwa kuna mmiliki, serikali, Kamisheni ya Wakfu na watu binafsi, jumla ni nyumba 40. Lakini nyumba 21 zilizokuwa katika hali mbaya ni za serikali na zilizokuwa katika hali mbaya sana kabisa ni 4 za serikali, na katika Kamisheni ya Wakfu ni 12 na 6 ni mbaya sana. Watu binafsi ni 56 na zilizokuwa mbaya sana ni 30.

Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Waziri, hapa ametuambia nyumba zilizokuwa mbaya sana ni 4 za serikali. Katika ukurasa wa 18, chini mwisho huku naomba nikinukuu, anasema;

"Pia, katika ukaguzi uliofanywa katika nyumba za serikali Mji Mkongwe Zanzibar zimebainika kwamba nyumba 26 ziko katika hali mbaya na zinahitaji matengenezo makubwa ya haraka. Hatua ambayo imechukuliwa katika nyumba hizo, tayari wamejulishwa wapangaji juu ya ubovu wa majengo hayo, na hatari ya kuendelea kuyatumia majengo hayo."

Mhe. Mwenyekiti, mimi Mhe. Waziri, aje anipe ufafanuzi, kwa sababu huku nyumba 26 za serikali ni mbaya sana, lakini huku ametuwekea 21 ambazo ni mbaya kiasi na 4 ni mbaya sana. Lakini pia Mhe. Mwenyekiti, huu ushauri alioutoa hautoshelezi, kwa sababu nyumba zikiwa ni mbaya sana, basi muda wowote inaweza kutokea athari na watu wakapata majeraha mbali mbali. Kwa hivyo, namuomba Mhe. Waziri, kwa ushauri huu, bado hautoshelezi, isipokuwa atafute namna nyengine, ili watu hawa awahamishe na nyumba hizi zipate kufanyiwa ukarabati, zikawa nzima na baadae wawarejeshe.

Mhe. Mwenyekiti, sasa niende katika Idara ya Ardhi. Mhe. Mwenyekiti, migogoro ya ardhi bado ipo. Kwa hivyo, namuomba Mhe. Waziri, aje atuambie, kwa sababu bajeti ya mwaka 2011/2012, iliposomwa bajeti ya Mhe. Makamu wa Pili wa Rais, ilieleza kwamba migogoro ya ardhi inasababishwa na baadhi ya viongozi. Sasa aje atufafanulie.

Pia, alisema kwamba migogoro hiyo wamewaachia waitatuwe wenyewe. Kwa hivyo, mimi nauliza migogoro hiyo ambayo imesababishwa na viongozi wa

serikali, je, imeshatatuliwa na kama imetatuliwa, ni migogoro mingapi na kama bado ni sababu gani zilizopelekea isitatuliwe migogoro hiyo. Kwa nini viongozi wanahusika na migogoro hiyo, kuna nini hapa Mhe. Mwenyekiti? Kiongozi yeye anapaswa kuwaelekeza wananchi na kuwafahamisha, halafu yeye ndio anajihusisha na migogoro hiyo, kulikoni.

Mhe. Mwenyekiti, juzi nilipata malalamiko kwa wananchi wangu wa Matemwe. Malalamiko hayo waliyonipa Mhe. Waziri, naomba uyasikilize halafu uyafanyie kazi. Wananchi wao wana maeneo yao hawapungui watu 12, maeneo hayo yako Muyuni Matemwe huko karibu na *beach* huko, lakini kumetokezea Mwekezaji ambaye anataka kuwekeza sehemu hiyo. Wananchi hao waliitwa wilayani wakaambiwa kwamba ardhi ni mali ya serikali, wao watapaswa kupewa tu chochote. Wananchi hao wako 12 na eneo lao halipungui heka saba. Wao wanaambiwa eneo hilo watapatiwa shilingi milioni 22.

Mhe. Waziri, hebu nieleze, kwa nini wananchi hao wana miti yao, wengine wana michungwa, wengine midimu, wengine wana minazi na wengine miti tu ya kawaida. Kwa nini wanaambiwa wapewe shilingi milioni 22, kumefanyika tathmini gani na utaratibu gani kwamba hili eneo anapewa mwekezaji halafu wananchi hao wanapewa kiasi hicho kidogo cha fedha. Kwa kweli wananchi watakuwa hawana imani na serikali yao, ingawa ardhi ni mali ya serikali. Lakini je, hii milioni 22 ndio inaendana na tathmini ya miti yao iliopo pale. Mhe. Waziri, naomba ulifuatilie hili kwa kina na halafu uje unipa ufafanuzi na mimi kwa kina vile vile.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya kusema hayo siungi mkono mpaka Mhe. Waziri, aje anifafanulie kwa kina. Ahsante Mhe. Mwenyekiti. *(Makofi)*

**Mhe. Hussein Ibrahim Makungu:** Nakushukuru Mhe. Mwenyekiti. Kwanza awali ya yote namshukuru Mwenyezi Mungu, kwa asubuhi hii kuwa sote tuko katika hali ya uzima na afya njema humu ndani katika Baraza lako tukufu. Pia, nikushukuru wewe Mhe. Mwenyekiti, kwa kunipa nafasi hii kuchangia, Hotuba ya Makadiria ya Mapato na Matumizi ya Fedha kwa mwaka wa 2015/2016 kwa Wizara ya Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati.

Kwanza nimpongeze Mhe. Waziri, kwa juhudi zake kubwa Mhe. Ramadhan Abdalla Shaaban, alizozitekeleza katika wizara hii. Pia, nimpongeze Mhe. Naibu Waziri, Makatibu wote wawili, Ali Khalil Mirza na Mustafa Aboud Jumbe, kwa umakini wao mkubwa katika wizara hii kwa wanavyojitahidi pamoja na watendaji wao wote.

Vile vile, Mhe. Mwenyekiti, nimpongeze Mhe. Mwenyekiti wa Kamati Mhe. Mahmoud, kwa juhudi zake kubwa alizoonyesha na mimi pia ni mjumbe wa kamati hiyo, lakini nimpongeze sana Mwenyekiti wangu kwa jitihada zake kubwa na umakini wake mkubwa anaoufanya katika kazi hii ya kamati katika wizara hii.

Mhe. Mwenyekiti, pia, niwapongeze Waheshimiwa Wajumbe, wote tumefanyakazi pamoja na mimi nikiwa mmoja na wengine nawapongeza wote kwa juhudi zao mbali mbali walizoonesha.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nianzie katika ukurasa 35, ambapo ni suala muhimu sana katika nchi yetu kwenye kuleta maendeleo. Nije kwenye suala la Shirika la Umeme. Shirika hili mimi nawapongeza sana kwa juhudi zao wanazo wanazofanyakazi. Kwa kweli mnyonge mnyongeni lakini haki yake tumpe jamani. Hawa ndugu zetu wanajitahidi sana, kama tunavyojua umeme ni hatari na unaweza ukapoteza maisha yako, kwa kweli hawa ndugu zetu wanafanyakazi usiku na mchana na mimi mjumbe wa kamati mmoja ninapokwenda basi nayaona yale maendeleo ambayo wanayofanya na kujitahidi ili umeme usikatike hata dakika tano.

Lakini kwa vile mambo mengine yanakuwa nje ya uwezo wao, na wana matatizo mengi ya usafiri, siku nyengine wanachelewa kufika. Lakini wao wako *on the sport* Mhe. Mwenyekiti. Wakisikia kuna tatizo wameshafika na mafundi wapo wakati wote wanajitahidi ili kuhakikisha umeme usikatike katika visiwa vyetu vya Zanzibar Unguja na Pemba.

Mhe. Mwenyekiti, nilisema nianze 35 katika mwaka wa fedha 2014, shirika lilikadirio kukusanya bilioni 87, hili ni jambo la kupigiwa mfano kweli kweli Mhe. Mwenyekiti, kwa sababu hawa ndugu zetu bila kutoka nakufuatilia maeneo husika, hizi fedha wasingezipata. Na ukitizama tarehe Machi, 2015, shirika limekusanya bilioni 58 sawa na asilimia 67, hili ni jambo kubwa sana na mimi nawapongeza sana hawa ndugu zetu wa Shirika la Umeme kwa juhudi zao hizi za kukusanya mapato hayo.

Mhe. Mwenyekiti, kwa upande wa matumizi yao ni makubwa na wanajitahidi kutengeneza, ili likitokea tatizo na kununua vifaa, vifaa hivi vinatumika havina muda mrefu, vinatumika miaka miwili, mitatu vibadilishwe na ukiangalia, kwa mfano suala la nguzo, transfoma na waya haviwezi vyote kutumia muda mrefu sana. Lakini hao wenzetu wanajitahidi kubadilisha na matumizi yao yanakuwa mengi hadi kufikia mpaka bilioni 86. Hili ni jambo la kutia moyo sana na wanajitahidi kukusanya fedha na kuweza kulipa.

Mhe. Mwenyekiti, mimi niseme kwamba ukienda Shirika la Umeme mara nyingi sana wanalalamika. Kuna taasisi nyingi sana za serikali hazilipi umeme na wao kama watumizi wanatakiwa matumizi watumie kama hivi bilioni 86 kwa gharama zao tu za uendeshaji au matumizi mbali mbali. Lakini taasisi nyingi za serikali zinashindwa kuwalipa hawa ndugu zetu. Ukiangalia wadaiwa sugu kama *ZAWA*, JWT wanadaiwa fedha nyingi na taasisi za serikali nyingi zinadaiwa fedha nyingi sana Mhe. Mwenyekiti. Kwa hivyo, mimi naiomba sana serikali izihimize hizo taasisi za serikali zinazodaiwa ili waweze kuwalipa hawa *ZECO*, ili waweze kufanyakazi zao kwa ufanisi.

Mhe. Mwenyekiti, kuna kipindi nilikuwa Dar es Salaam tulikuwa na kamati tukitembelea *TANESCO*, tulikwenda Makao Makuu ya umeme *TANESCO* pale Ubongo. Kwa kweli nilisikitika sana Mhe. Mwenyekiti. Kufika pale Mkurugenzi anasema tunawadai Zanzibar karibu bilioni 70 za umeme, ni fedha nyingi. Mwisho yule Mkurugenzi akatuambia pale basi mtambo mmoja tu huu chukuweni nyinyi tieni mafuta tu kama mtaweza. Wanasema pesa zao zinachelewa kulipwa na mara nyengine mpaka hutoa barua za vitisho na *notice* kali kuwa watakata umeme Unguja na Pemba, kwa kweli inasikitisha.

Mhe. Mwenyekiti, kwa vile Muungano huu na tunaheshimiana, Muungano wetu wa kidugu basi hawatukatii umeme ndugu zetu. Lakini ingekuwa ule mtambo wa mtu binafsi, mmoja basi leo sisi tungekuwa tunakaa kiza Mhe. Mwenyekiti. Mimi nawashukuru sana ndugu zetu wa Tanzania Bara, hasa *TANESCO* kwa umoja wao huu na kutuvumilia sana haya madeni.

Mhe. Mwenyekiti, kuna kipindi katika safari zetu za kwenda Shirika la Umeme na kamati yetu, tukapata taarifa kwamba sasa deni limepungua tunadaiwa mpaka bilioni 45, lakini mpaka kesho bado tunadeni Mhe. Mwenyekiti. Kwa hivyo, naomba sana serikali iwaangalie hawa ndugu zetu tuweze kuwalipa na taasisi za serikali zilipe, ili na wao waweze kulipa. Nasema hivi kwa sababu wananchi wanyonge wanajitahidi Mhe. Mwenyekiti, kulipa umeme. Kila siku ukienda kwenye vituo vya kuuza umeme utawakuta wananchi wanyonge wanalipa shilingi 10,000, 20,000, 40,000 wanalipa umeme na ukiyatizama makusanyo yale madogo madogo yanafikia mpaka milioni 40,000 kwa siku au milioni 35,000 mpaka 40,000 zinakusanywa, lakini hazitoshi.

Mhe. Mwenyekiti, kama nilivyoeleza matumizi yao Shirika la Umeme ni bilioni 86 kununua vifaa na vitu mbali mbali. Kwa hivyo, naomba Mhe. Mwenyekiti, kama nilivyoeleza taasisi za serikali zipewe kipaumbele kulipa hizi fedha, ni fedha nyingi sana zinadaiwa hizi taasisi za serikali. Hatuwezi kuwalaumu Shirika la Umeme Mhe. Mwenyekiti, hawa ndugu zetu wanajitahidi kwa nguvu zao zote kuwalipisha wawekezaji mahotelini, wanakwenda mpaka mashamba usiku na

mchana kutafuta fedha hizo, wakikuambia lipa milioni 20,000,000 hujalipa wanakukatia. Lakini bila ya hivyo wasingepata pesa. Mimi nawapongeza sana ndugu zetu hawa wajitahidi sana ili kuweza kuyaondosha madeni ili twende salama.

Mhe. Mwenyekiti, nikiendelea katika hili shirika, kama nilivyosema nimewapongeza sana na nitasema mafanikio gani ambayo hawa ndugu zetu wamepata. Shirika limebadilisha waya chakavu karibu kilomita 34, hizi waya ni *expensive* na wakati mwengine zinakuwa *underground cable*, lakini waya ni *special* kabisa. Kwa hivyo, mimi nawapongeza kwa kubadilisha waya kilomita 34. Mimi ni mjumbe wa kamati hiyo hali ninaijua na tumeshakwenda kuangalia mara nyingi katuonesha ile *physical* yenyewe. Kama nilivyosema Mwenyekiti, yuko makini anataka kuona kila kitu kinachofanyika kwa macho, Mwenyekiti wetu wa Kamati. Kwa hivyo, nampongeza sana na yeye kwa juhudi zake hizo.

Mhe. Mwenyekiti, Shirika tunabadilisha nguzo za umeme 1,247, hizi pia ni za fedha nyingi. Ukitizama nguzo moja unaweza kufikia hata shilingi milioni moja na zaidi, au kama milioni 1.8, hii nguzo sio ya kawaida ni nguzo ya gharama kubwa sana. Kwa hivyo, nawapongeza ndugu zangu hawa kwa kuzibadilisha bila ya kuleta athari kwa wananchi wetu. Wameona bora waziondoshe mwanzo, bora kuziba ufa kuliko kujenga ukuta, wameziondosha nguzo hizi na wameweka nguzo mpya kabisa.

Lakini pia kwa juhudi zao kubwa kwa kuondosha usumbufu wa kukatika umeme mara kwa mara hata hizi *transformer* wamezirekebisha, *transformers* 385 Mhe. Mwenyekiti, nimekwenda kuzikagua *transformers* hizi karibu *transformers* 20, nyengine tumesema basi tumesharidhika kwa *transformers* 20 hizi nyengine tuziache, lakini wamefanya kazi nzuri kuzifungua, kuzisafisha na kuzitia *oil*, girisi na kila kila kitu.

Kwa hivyo, hawa ndugu zetu wanafanya kazi nzuri na utaalamu wao waliokuwa nao wa uhakika kabisa, lakini mimi niseme kitu kimoja nawaombea sana ndugu zetu wanafanya kazi ya kuriski hasa wafanyakazi wa Shirika la Umeme, huu umeme wao unakuwa *high voltage,* ukigusa umekwisha au umegeuka unakuwa kama makaa vile na mara nyingi wanakuwa hata umeme wamezima lakini unakuta wanarushwa kwa mbali, anaweza kuanguka kwenye nguzo, madhara kwa kweli makubwa yanaweza kuwapata wakati wowote wafanyakazi wetu wa umeme.

Lakini mimi naomba sana Mhe. Waziri, uangalie suala la kuwapatia bima hawa wafanyakazi wa Shirika la Umeme, kama sasa hivi unajua Mheshimiwa katika hospitali yetu iliyofunguliwa hapa mpya ya *Vigo Majestic* wanachukua mpaka *Insurance* ya Jubilee, kwa hivyo, ukiwa na *insurance* pengine kwa mwezi laki

moja, lakini unatibiwa pale bure kabisa. Kwa hivyo, mimi naomba sana hawa ndugu zetu wa shirika la umeme wapatiwe bima hii haraka ili wanapofanya kazi zao wanapoumia Serikali itaondosha kuweka mzigo wa kuwatibu au mambo mengine, kwa hivyo, atashughulikiwa na hii bima inaweza ikaondosha usumbufu.

Mhe. Mwenyekiti, mimi niseme tu kidogo katika maeneo mengine bado umeme mdogo mimi nasema katika jimbo langu pia kuna eneo linaitwa Kiboko yoa Mwanyanya jeshini juu kule, umeme ni mdogo hasa ikifika saa moja ya usiku, Mhe. Waziri, hili naomba uliangalie kwa umakini kabisa, najua una moyo mkubwa na wafanyakazi wenye jitihada kubwa, lakini kuna maeneo bado na hili bora nilisemee hapa kabisa ili muweze kulishughulikia eneo hili wananchi wetu waweze kupata wa uhakika. Vitu vyao vingi vinaungua kila ukienda unapata malalamiko kama *TV* imeungua, Friji limeungua, pampu ya mashine haina nguvu kupandisha maji, kwa hivyo, wanapata usumbufu. Kwa hivyo, naomba uliangalie eneo la Kiboko yao juu kule karibu na Mwanyanya na Mtoni zinalingana pale karibu umeme wao mdogo sana wananchi hao wanapata usumbufu.

Mhe. Mwenyekiti, niingie kwenye ukurasa wa 19 kifungu namba 50 katika kitabu cha bajeti cha Mhe. Waziri, Mamlaka ya Mji Mkongwe katika mwaka 2014/15. Mheshimiwa, katika Mamlaka ya Mji Mkongwe wamefanikiwa kutekeleza mafanikio mengi na wamejitahidi sana Mamlaka ya Mji Mkongwe kuimarisha mji wetu uwe mji wa kitalii wa kimataifa kama unavyojua kwa Hifadhi ya *UNESCO*.

Lakini mimi nisikitike sana Mhe. Mwenyekiti, tumeshakwenda na Kamati zaidi ya mara mbili, tatu kuangalia hili Beit-al Ajab bado lipo kwenye hatari sana, kila tukienda kwenye kamati Mhe. Mwenyekiti, unaambiwa miaka miwili sasa wafadhili ni Oman wanaotengeneza kwa ufadhili, lakini mpaka leo wametengeneza kidogo wameacha.
Sasa sijui tatizo lipo wapi Mhe. Mwenyekiti, naomba sana jengo hili lipo hatarini na pale wananchi wanapita mara kwa mara, kwa hivyo, ningeomba sana kama huyu mfadhili atakuwa hawezi kutufadhili kwa kutusaidia basi naomba Serikali itie mkono wake ili tuweze kujenga pale kumaliza lile tatizo la Beit- al Ajab kuondoshwa kule nyuma kulikobomoka kuweze kukaa vizuri na kuondosha matatizo ya wananchi wetu na katika kuishi na kupita kwao wasije wakapata madhara.

Mhe. Mwenyekiti, jengine niende kwenye suala hili la nyumba pale Forodhani jumba lile la Abdulhamid. Mhe. Mwenyekiti, lile jumba tumeshakwenda zaidi ya mara tatu kwenye kamati na kashapewa taarifa huyu mmiliki wa jumba hili ili lile jumba alitengeneze, kwa kusikitisha mpaka wafadhili washakwenda kununua jumba lile hataki kuliuza. Sasa mwisho wa siku tutakuja kuulisha wananchi wetu na pale wananchi wanapita wengi na jumba limeshakuwa bovu bovu, sasa likija

kuanguka na watu wakija wakifa pale hii hasara itakuwa kubwa na wadau wakubwa watakuwa ni serikali wameachia mpaka watu wale wakafa.

Mimi naomba sana huyo mmiliki kama hataki kulitoa jumba hili na yeye hana uwezo wa kulitengeneza hii Serikali itaifishe Mhe. Waziri, afutiwe umiliki wa hiyo nyumba huyu mtu na apewe mtu mwengine anayeweza kutengeneza kwa sababu tunachoogopa ni maisha ya watu, hatuangalii kumuonea mtu ila tunaangalia maisha ya watu kama yeye hawezi kutengeneza itakaa mpaka lini nyumba ile pale.

Mhe. Mwenyekiti, watu wanapita wakienda Forodhani na watalii wanapita pale, limeanguka jumba lile je, mimi naomba sana Mhe. Waziri, kama uwezo unao wa kumfutia mfutie miliki yake nyumba hii ili tuweze kumpa mtu mwengine akajenga, hii ni amri ya maamuzi magumu ya Serikali tuweze kufanikisha suala hili tusisubiri tu mpaka waje kufariki watu.

Mhe. Mwenyekiti, niingie ukurasa wa 22, ukurasa wa 57, Mamlaka ya Maji Serikali inaendelea kuwapatia maji safi na salama kwa nia njema kabisa Serikali iliyokuwa nayo kujitahidi kila siku usiku na mchana, hasa kupitia Rais wetu wa Zanzibar kila akiamka akenda anataka wananchi wake wapate maji safi na salama kuwaondoshe usumbufu, lakini mimi kidogo Mhe. Mwenyekiti, mimi kidogo katika kitabu cha Mhe. Waziri, nimekisoma hapa kimenisikitisha kidogo kwa sababu nia ya Rais wetu tofauti kidogo na hapa, naomba anipe maelekezo akija ili kuja kunifahamisha kakusudia nini, naomba ninukuu katika kifungu cha 57, ukurasa wa 22;

> "Mhe. Mwenyekiti, Serikali imeendelea kuwapatia maji safi na salama wananchi waishio vijijini katika umbali usiozidi mita 250 kutoka kwenye makaazi ya kupitia programu ya usambazaji wa maji vijijini, kwa ukamilishaji wa miradi ukarabati wa miundombinu, uzalishaji mabomba, ufungaji wa mita, upekekaji umeme katika visima vya maji."

Mhe. Mwenyekiti, mimi nina wasi wasi hapa, hapa tumeambiwa Rais kafuta visima vyote kwenye vianzio vya maji viondoshwe mita zote, yale maji yawe *free* tu yanapanda *time* zote, hamna kuchajiwa kwa mambo ya umeme, wala nini. Halafu leo Rais kupitia Wizara ya Fedha atatoa milioni mia tano kuwapa *ZECO*, sasa naona hapa ufungaji wa mita unaendelea, sasa sijui hili suala, naomba ufafanuzi mzuri kwa sababu wananchi wetu wana matumaini makubwa kwa Serikali yao kwa kutuletea maji safi na salama.

Na hili tatizo kubwa linatokea *ZECO* wanawadai *ZAWA* na hii imepelekea mpaka kuletwa kwenye kamati unakuta visima viko vizuri, mota zipo lakini umeme hamna umekatwa kwa ajili ya usumbufu wa umeme madeni yamekuwa mengi.

Sasa Rais akasema mita ziondoshwe kwenye visima vya maji, sasa hili naomba Mhe. Waziri, ukija uniambie nia ya Rais aliyosema na wazo lake ni zuri, sasa hapa itakuwaje visima vya maji kuwa na mita tena. Mimi naomba ufafanuzi mzuri kuhusu hizi mita kwenye vianzio vya maji.

Mhe. Mwenyekiti, niendelee hapa katika ukurasa wa 17, kifungu namba 44, Idara ya Nyumba na Makaazi, mimi nianzie kwenye nyumba hii ya Kengeja/Mtambile Mhe. Mwenyekiti, kamati imetembelea nyumba ile na nyumba ile mpaka leo wananchi wale wanaishi kule Kengeja wanaishi ndani ya ile nyumba, ukitizama nyumba yenyewe ni mbovu kweli kweli, *time* yoyote inaweza ikaanguka na imeathirika sana kwa sababu juu inavuja nyumba ile, lakini bado wananchi wetu wanyonge na masikini, lakini wanaishi kwenye nyumba ile mpaka leo na wengine mpaka wameshajukuu pale pale.

Kwa hivyo, mimi naomba sana Serikali ilisema kupitia Wizara yake itatoa milioni mia mbili ili kuezeka nyumba hiyo, lakini mpaka leo kwa masikitiko makubwa Wizara haijapata fedha hizi kuweza kuezeka nyumba ile. Kwa hivyo, naomba sana Mhe. Mwenyekiti, suala hili la milioni mia mbili la kuezeka nyumba ya Mtambile ile wapatiwe fedha hizi haraka kwa sababu bado wananchi wanaendelea kuishi na wala hawana pa kwenda, washakaa pale wameshajukuu, wamekaa muda mrefu tokea Mapinduzi yetu mpaka leo wanaishi pale. Kwa hivyo, naomba sana milioni mia mbili hizi Wizara ipatiwe iweze kumaliza jengo lile kuezeka juu angalau wale wananchi wapate kuishi vizuri.

Mhe. Mwenyekiti, mwisho kabisa niende Idara ya Nishati kama Mjumbe wa kamati, sasa hivi hapa ninavyoona mafuta wakati mwengine yanakuwa shida hasa *diesel* na *petrol* inakuwa shida kweli kweli, maana yake mpaka unakuwa mtu unashinda sheli pale kwa ajili ya kupata mafuta, lakini hapa nina masikitiko makubwa niliyokuwa nayo wawekezaji wanakuja wanataka wajenge *Deport* mpya kwa *facilities* tafauti tafauti ili waweze kuhifadhi mafuta ili mafuta hapa yasiadimike.

Sasa mimi nashangaa kwa nini wawekezaji wanacheleweshewa kupewa kwa haya maendeleo wanayotaka kuyafanya ili haya mafuta ya *diesel* na *petrol* yawe masaa 24 unakwenda sheli unapata, kwa sababu unapokwenda sheli saa nyengine unakuta unakaa karibu saa nzima kwenye mafuta na huku una shughuli zako za kimaisha, kwa hivyo, huwezi kufanya maendeleo ya nchi yetu bila ya kupata mafuta yale ya *petrol*.

Nataka Mhe. Waziri, unijibu, kwa nini wawekezaji wanakuja wanacheleweshewa kupata hii *Deport facility?* Kwa hivyo, mimi naomba sana Mhe. Waziri, unijibu vizuri suala hili nipate kujua na wananchi wasikie lengo la Serikali yao ni nini

kuwasaidia wananchi, kuondosha usumbufu wa mafuta, sasa hivi nchi iliyoendelea Mwenyekiti, huwezi kwenda kupanga foleni ya mafuta, tazama Dar es Salaam tu hapo ukenda sheli unapapatikiwa mafuta yako mengi wateja hamna.

Lakini sisi unakuja hapa unakwenda pale unaambiwa aa, mafuta yanataka kupanda bei, mafuta leo hamna, yule muuzaji anaringa kwa sababu anajua yuko peke yake, lakini ikiwa mafuta mengi nafikiri Mhe. Mwenyekiti, wale wenye masheli watakuwa wanaomba wateja wende kutia mafuta, tufuate mfano mzuri Tanzania Bara tu hapa ukenda sheli mpaka kioo unasafishiwa, gari yako unapangusiwa mavumbi ili utie mafuta.

Kwa hivyo, naomba tufikie hatua hiyo, tusiwe kama tunaomba mafuta kwa ajili ya hawa ndugu zetu unakwenda pale kama wakusaidie wakati unatoa pesa zako nyingi sana na Serikali inapata pesa nyingi kwenye mafuta kwenye malipo mbali mbali hasa ya kodi. Kwa hivyo, naomba sana wawekezaji hawa wapewe kipaumbele sana, washakuja kwa nia yao njema na Serikali iwapokee na iwafungulie milango waweze kufanya kazi vizuri kabisa ili kuleta maendeleo mazuri katika nchi yetu.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nakushukuru sana naunga mkono asilimia mia kwa mia bajeti hii, mimi na wananchi wangu wa Jimbo la Bububu hatuna mashaka nayo, nakushukuru sana. Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti. *(Makofi)*

**Mhe. Mwenyekiti:** Waheshimiwa Wajumbe, dakika zilizobakia ni chache mno kwa ajili ya kuchangia, hivyo, ningeomba tukubaliane kwamba wale wengine ambao wameleta majina yao watachangia jioni tutakapokuja.

Lakini kabla ya kuahirisha Waheshimiwa Wajumbe, nina tangazo dogo linalohusiana na Kamati ya Uongozi kwamba kile kikao cha saa 9.30 kimeahirika hadi hapo *notice* itakapotolewa. Baada ya kusema hayo Waheshimiwa Wajumbe, nawashukuru kwa mchana huu na *Inshaalla* tutakutana tena saa 11.00 Jioni.

*(Saa 5.54 Mchana Baraza liliahirishwa mpaka Saa 11.00 Jioni)*

*(Saa 11:00 jioni Baraza lilirudia)*

*Majadiliano yanaendelea*

**Mhe. Mwenyekiti:** Majadiliano yanaendelea, kabla sijamkaribisha Mhe. Salim Abdalla, naomba kwanza nimkaribishe Mhe. Nassor Salim Ali, kwa sababu ana dharura, Khalafu baadae Mhe. Salim Abdalla Hamad, ataendelea atafuatiwa na Mhe. Abdalla Muhammed.

**Mhe. Nassor Salim Ali:** Ahsante Mhe. Mwenyekiti na mimi kunipa fursa hii ya kuchangia kidogo hotuba ya Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya kukushukuru wewe kwanza nichukue fursa hii pia kumpongeza sana Mhe. Waziri, kwa kazi nzuri ambayo anaifanya, pamoja na watendaji wake akiwemo Katibu Mkuu na Naibu Katibu Mkuu na Wakurugenzi wote, katika kuleta maendeleo katika Wizara yetu hii ambayo ina jukumu kubwa la kusimamia mambo nyeti ya kimaendeleo katika nchi yetu.

Mhe. Mwenyekiti, pia, nichukue fursa hii kumshukuru sana na kumpongeza sana Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Mhe. Ali Muhammed Shein, kwa kazi nzuri anayoifanya kwa kutekeleza vyema ilani ya Chama cha Mapinduzi kwa mwaka 2010/2015 ambapo amefanya kazi kubwa na anastahiki kupewa pongezi kubwa kwa kazi anayoifanya.

Mhe. Mwenyekiti, nianzie katika Mamlaka ya Uhifadhi na Uendeshaji wa Mji Mkongwe. Kwa kweli na mimi nichukue fursa hii kumpongeza sana Mkurugenzi wa Mji Mkongwe kwa kazi ambayo anayoifanya katika kusimamia vyema maendeleo na kuboresha vyema hifadhi ya Mji Mkongwe. Watalii wote wanaokuja nchini ni kivutio kikubwa tulichonacho cha hifadhi ya Mji Mkongwe. Kuendeleza Mji Mkongwe ndio faida ambayo tunaipata katika kukuza uchumi wa nchi yetu.

Mhe. Mwenyekiti, katika kitabu hichi ambacho Mhe. Waziri, alikisoma ukurasa wa 20 ameeleza kwamba mamlaka ilifanya ukaguzi wa jengo la *People's Palace* na kuona kuwa ukuta wa kusini wa jengo hilo uko katika hali mbaya. Mamlaka ikachukua hatua ya kuweka miega kona ya kusini na magharibi na kuzisaidia katika kuta hizo pamoja na kuweka mihimili.

Mhe. Mwenyekiti, mimi niiyombe sana Mamlaka husika pamoja na wizara husika ili kuweza kuzifanyia kazi za ziada katika nyumba za kumbukumbu ambazo zina historia kubwa na ambazo inakuwa ni kivutio kikubwa kwa wageni wanaokuja Zanzibar, kuona haiba ya majengo yetu, kuona haiba ya mji wetu ambao ndio kivutio kwa watalii hao. Sasa kuweka miega, nadhani miega sote tunajua maana ya miega ni kiswahili ambacho tunakifahamu. Mimi niombe sana wizara basi angalau kufanya ukarabati kuliko kuweka miega. Mhe. Aballah, anajua maana ya miega kwa sababu hata migomba ya mtwike inaitwa miega. Mhe. Waziri, atakapokuja atwambie ni mikakati gani ambayo inayowekwa ili kuweza kufanyiwa ukarabati jengo kama hilo ambalo lina historia kubwa.

Mhe. Mwenyekiti, nikitoka hapo nije katika Mamlaka ya Maji, katika programu ya usambazaji wa maji vijijini. Mheshimiwa, niishukuru sana na niipongeze sana

Wizara na Idara ya Maji kwa kazi nzuri ambayo wanayoifanya vijijini katika kuwapatia wananchi na kuwaondolea matatizo ya maji katika vijiji mbali mbali kwa Unguja na Pemba. Nichukue fursa hii Mheshimiwa, kuipongeza sana Wizara ya Mamlaka ya Maji Pemba kwa msaada mkubwa ambao wameutoa kwa kutatua matatizo ya maji katika Shehia ya Jombwe.

Mhe. Mwenyekiti, kule Pemba katika maeneo ambayo yalikuwa yana matatizo makubwa ya maji ambayo shehia hii ya Jombwe iko katika Jimbo la Kiwani. Wananchi wa Jombwe walikuwa wana matatizo makubwa sana. Lakini kutokana na wananchi wenyewe kujikusanya na kupata wafadhili mbali mbali wameweza kuchimba kisima cha kuweza kusambaza maji katika Shehia nzima ya Jombwe katika mitaa ya Chanjaani, Kwasanani na Jombwe yenyewe. Mamlaka ya Maji imetoa ushirikiano mkubwa sana. Sasa haya ndiyo maendeleo na ndiyo dira na ilani vile vile ya Chama cha Mapinduzi. Kazi ambazo wameifanya Mamlaka ya Maji Pemba ni kazi kubwa na inastahiki kupewa pongezi.

Mhe. Mwenyekiti, mradi huu wa maji ambao umechukua takriban kwa gharama ya milioni 50. Niiyombe Wizara kuipa kipaumbele zaidi mradi huu wa maji ili wananchi waweze kupata maji katika vijiji vyengine vya jirani viliopo katika maeneo ya Jombwe na maeneo mengine katika maeneo ya Mwambe. Taarifa nilizonazo Mhe. Mwenyekiti, kwa sababu nimeshawahi kufanya ziara katika mradi huu wa maji na hii kuthibitisha kwamba kuwa Wawakilishi hususan wa CCM wanajali maendeleo ya kila kona katika nchi yetu ya Zanzibar.

Mhe. Mwenyekiti, nilifanya ziara katika maeneo haya na nikaona mradi huu wa maji ambao kwa kweli ulinivutia sana na niipongeze sana serikali katika kusaidia kutatua matatizo haya ya maji. Lakini mradi huu unahitaji msukumo zaidi katika kuimarisha zaidi miundombinu ya mradi huu wa maji. Taarifa ziliopo kwamba hivi karibuni Mhe. Mwenyekiti.

**Mhe. Mwenyekiti:** Samahani Mheshimiwa Mjumbe, kuna tangazo kwamba kuna mtu ameweka gari njiani yenye Na. Z928FM akaiondoe msafara wa Makamo wa Rais unataka kupitia. Tuendelee Mheshimiwa.

**Mhe. Nassor Salim Ali:** Mhe. Mwenyekiti, mradi huu wa maji ambao Mhe. Makamo wa Pili wa Rais kwa taarifa zilizokuwepo kwamba ataenda kuzindua mradi huu wa maji. Kwa hivyo, nimuombe Mhe. Waziri, kumuunga mkono Mhe. Makamo wa Pili wa Rais ili kwenda kujionea mwenyewe mradi huu wa maji ambao umetatua matatizo makubwa ya wananchi katika shehia hii ya Jombwe na kuweza kusaidia kufanya miundombinu zaidi.  Mbali na mradi wa usambazaji maji vijijini lakini kuna mradi, programu ya Uhuishaji na upanuzi wa shughuli za maji mijini.

Mhe. Mwenyekiti, kwa kweli Zanzibar hasa katika maeneo ya Mjini katika kipindi cha nyuma kulikuwa kuna matatizo makubwa ya maji na wewe ni shuhuda hata katika Jimbo lako la Kikwajuni, Rahaleo, Mji Mkongwe kwa Hani na maeneo mengine ya Mjini. Lakini nichukue fursa hii kuipongeza sana Wizara kwa kazi kubwa ambayo wameifanya kuona kwamba leo matatizo ya maji yamepungua katika kiwango kikubwa. Nina imani kwamba katika asilimia 80 mpaka 90 matatizo ya maji yamepungua katika mji wetu.

Mhe. Mwenyekiti, tunaelekea katika mfungo Mtukufu wa Ramadhani, katika kipindi hichi cha mfungo Mtukufu wa Ramadhani huwa kunakuwa na upungufu sana wa tatizo hili la maji. Nimuombe Mhe. Waziri, ili kusimamia vyema utakapofika Mwezi Mtukufu wa Ramadhani liondokane kabisa tatizo hili la maji katika mji wetu. Nina imani hiyo kwamba uwezo anao na Mamlaka ya Maji inayo uwezo huo. Kuondoa matatizo ya maji katika mji wetu, katika majimbo yetu, katika kila kona kwa sababu kipindi kile Mhe. Mwenyekiti, ni kipindi ambacho matumizi ya maji huwa ni makubwa. Sote tunajua hivyo na nina imani kubwa tatizo hilo basi litaondolewa.

Mhe. Mwenyekiti, nije katika mradi wa kuimarisha miundombinu ya maji pia. Miundombinu ndiyo muhimu inayotakiwa katika mji wetu, mbali na kwamba maji yanakuwepo lakini tatizo ni miundombinu. Sasa nimuombe Mhe. Waziri, kupitia Mamlaka ya Maji, kufanya kazi ya ziada katika maeneo yetu ya Mjini kwa sababu maeneo mengi tatizo linakuja la miundombinu ambayo imechakaa ni ya zamani hasa ukija katika maeneo ya jimbo langu la Rahaleo.

Mhe. Mwenyekiti, katika Jimbo la Rahaleo, maeneo ambayo yanakuwa na matatizo makubwa ni katika jumba No. 4. Mbali na mipango na maarifa tuliyoifanya Mbunge na Mwakilishi katika jimbo la Rahaleo, kutatua tatizo la maji lakini bado miundombinu inahitajika ili kuweza kupata wananchi wetu kutatua tatizo hili la maji katika Jumba No. 4 pamoja na Jumba No. 3. Kwa hivyo, nimuombe sana Mhe. Waziri, Mamlaka yake kufanya kazi ya ziada ili kuweka kutatua matatizo haya. Nina imani kubwa sana ukifika mwezi wa Ramadhani katika maeneo hayo maji watapata ili wananchi wetu waondokane na dhiki inayowakabili katika maeneo yetu.

Mhe. Spika, nigusie kidogo katika Shirika la Nyumba ambalo tayari Mhe. Rais kwa taarifa tulizonazo kwamba Rais ameshaitia saini Shirika la Nyumba la Zanzibar. Ukizungumza Shirika la Nyumba ni mategemeo makubwa ya wananchi kwamba kutakuwa na mabadiliko makubwa katika kutatua matatizo ya nyumba za wananchi. Hapa juzi kuna Mjumbe mmoja aliuliza kuhusiana na suala zima la Shirika la Nyumba, akatoa mfano wenzetu Tanzania Bara wamekuwa na mpangilio

mzuri katika kuzitambua nyumba za Shirika. Sasa niiyomba sana Wizara kuhakikisha inafanya mipango mizuri ya kuhakikisha kwamba inatambua nyumba zao kwa kuweka namba ili zijulikane kwamba nyumba hii ya shirika.

Lakini vile vile Mhe. Mwenyekiti, hapo nyuma kulikuwa na mipango ambayo ilizungumzwa kwamba litakapokuja Shirika kutakuwa na mipango ya kujenga nyumba za bei nafuu kwa ajili ya wananchi wetu. Sasa Mhe. Waziri, atakapokuja atueleze ile mipango ya kujenga nyumba kwa bei nafuu ili kuweza kuwasaidia wananchi wetu ili kuendana na Mapinduzi matukufu ya mwaka 1964. Nina imani kubwa kwamba suala hili katika kipindi kijacho serikali itatekeleza ahadi yake na kuweza kuwasaidia wananchi wanyonge kupata makaazi yaliyobora na yenye bei nafuu.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya kuyasema hayo nichukue fursa hii kukushukuru sana na niiyunge mkono kwa asilimia mia moja na niwaombe Wajumbe wenzangu kuiyunga mkono hotuba hii kupitisha bajeti kwa asilimia 100. Nakushukuru sana Mhe. Mwenyekiti.

**Mhe. Salim Abdalla Hamad:** Mhe. Mwenyekiti, na mimi nashukuru kwa kupata nafasi hii ambayo leo nitazungumza machache tu kuhusu hotuba hii ya Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati kuhusu makadirio ya mapato na matumizi, kwa mwaka wa fedha 2015/2016 katika ukumbi huu wa Baraza lako Tukufu, Baraza la Wawakilishi.

Mhe. Mwenyekiti, kwanza nianze kwa kuwapongeza Mhe. Waziri na watendaji wake na hususan Naibu Katibu Mkuu kwa mashirikiano makubwa waliyotupa tulipokuwa tukifanya kazi kwenye Wizara hii katika Kamati yetu ya Kuchunguza na Kudhibiti Hesabu za Serikali na kujua mambo mengi bila ya Kificho yaliyokuwemo katika hii Wizara, nawapongeza sana.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nianze kwa ukurasa wa 3 ambao nitaanza kuzungumzia Idara ya Mipango, Sera na Utafiti. Idara hii imewajibika katika kusimamia na kuratibu kazi zote za Wizara zikiwemo za kawaida na za maendeleo. Ninalotaka kuzungumza hapa ni ile miradi inayosimamiwa na sehemu hii, lakini siyote niko kwenye kifungu Nam. 9(8) kinachoeleza kuhusu utafiti wa nishati mbadala.

Mhe. Mwenyekiti, sote tunafahamu kuwa umeme ni moja ya nishati na kuwa sisi tunatumia umeme kwa Unguja na Pemba kutoka upande wa pili wa Muungano. Sote tunafahamu kuwa umeme huu Shirika la Umeme la Zanzibar *ZECO* linaununua umeme kwa bei ghali, lakini kwa kujali umuhimu wa wananchi kupata huduma hii ya umuhimu na ya ulazima wanayowafidia wananchi katika kuwauzia umeme huo kiasi ambacho hivi sasa kama sikosei Shirika letu la Umeme la

Zanzibar *ZECO* halipungui kudaiwa fedha taslimu za shilingi za Tanzania bilioni 45 na hii ni fedha nyingi sana. Naamini moja lililosababisha deni hili ni fidia wanayotoa na jengine ni kwa sababu ya baadhi ya watumiaji wetu wa nishati hii kutolipa malipo yao ipasavyo.

Ndiyo maana hata *ZAWA* ikiwa ni taasisi iliyokuwemo katika Wizara hii hii inadaiwa mabilioni ya fedha ni Shirika hili la Umeme, kwa hivyo, ni moja kwa moja ni kutaka kusema kuwa pamoja na nia safi ya shirika hili la kusambaza umeme kwa wananchi wote lakini linashindwa kutokana na umeme wanavyonunua na umeme unavyolipwa na wengine wanaokosa kulipa ipasavyo, ikawa Shirika kila siku linajiendesha kwa hasara na ninaamini kila siku zikenda mbele hasara hiyo itaongezeka.

Sasa basi pengine ndio sababu ikaonekana ipo haja ya Zanzibar kufanya utafiti wa umeme au wa nishati mbadala. Tunajua kuwa kuna aina nyingi tu za nishati mbadala kuna umeme wa jua, kuna umeme wa upepo, kuna umeme wa mawimbi ya bahari, hata kuna umeme tunaita *biogas* wa kinyesi na mengi mengineyo yanayohusiana na hayo.

Mhe. Mwenyekiti, utafiti wowote ule na hasa utafiti mkubwa kama huu unahitaji gharama kubwa sana na kama fedha haikupatikana ipasavyo, kwa hivyo, nahakikisha utafiti huu hautaweza kufanikiwa ipasavyo na lile suala la Serikali kuzidi kuingia hasara kwa sababu ya umeme huu litakuwa likiendelea siku hadi siku.

Mhe. Mwenyekiti, katika mwaka 2014/2015 kulikuwa na michangio ya aina mbili kwa utafiti huu wa nishati mbadala. Kulikuwa na mchangio wa Serikali na kulikuwa na mchangio wa hisani wa maendeleo. Tukifungua viambatanisho nambari 81 na nambari (b1) na nambari (b2) ukurasa wa 51 na 50 hii taarifa tutaiona kwa ukamilifu. Tukiangalia muhtasari wa matumizi ya fedha kwa kazi za maendeleo Julai, 2014 mpaka Machi, 2015, yaani ya mchango wa SMZ tukija katika sehemu hii ya utafiti wa nishati mbadala hapa jumla ya shilingi 219,000,000 zilikisiwa zitumike kwa shughuli hiyo, lakini mpaka kufika mwezi huo wa Machi, ni jumla ya 70,000,000 zilizopatikana ikiwa ni asilimia 32. Tukiangalia mchango wa wahisani kwa shughuli hiyo hiyo utaona kuwa utafiti huu ulikuwa wahisani wachangie jumla ya 1,621,600,000, lakini zilizopatikana ni 262,269,988 tu, sawa sawa na asilimia 16.

Kwa vile kutokana na umuhimu wa utafiti huu ili kuweza kuingiza Zanzibar kuwa na nishati mbadala na *response* iliyofanywa na Serikali na hata mashirika naona haitoshelezi. Kwa sababu ilikuwa hii kwa umuhimu wake ninamuomba Mhe. Waziri, anieleze kwa asilimia hii 32 ikiwa ni mchango wa Serikali na asilimia hii

16 ikiwa ni mchango wa wahisani, je, utafiti huo umefikia katika lengo gani na halafu kuna ushauri gani zaidi ya hapo. Hiyo ni moja.

Mhe. Mwenyekiti, nikiendelea sasa nitaendelea na kifungu cha 46 kilioko katika ukurasa wa 18 na kifungu hiki moja kwa moja kinahusiana na kuzifanyia matengenezo nyumba za Serikali. Ipo kazi kubwa imefanywa hapa kwa majumba yaliyoko Michenzani na sehemu nyengine na usafishaji wa makaro na kadhalika napongeza, lakini chini huku imeeleza kuwa;

> "Katika ukaguzi uliofanywa katika nyumba za Serikali Mji Mkongwe imebainika kuwa nyumba 26 ziko katika hali mbaya sana na zinahitaji matengenezo makubwa na ya haraka na hatua tayari zimeshachukuliwa kuwajulisha wapangaji juu ya ubovu wa majengo hayo na hatari ya kuendelea kuyatumia majengo hayo."

Majengo 26 kwenye Mji Mkongwe ni majengo mengi sana na Mji Mkongwe ni mji wetu wa urithi wenye historia unaoingiza fedha nyingi kwa watalii wanaokuja kuangalia hapa Zanzibar. Kila majumba yakizidi kuporomoka kiasi hiki maana yake ndio yale mapato tuliyoyapata yatazidi kupungua na mwisho wake himaya ya mji huu itaondoka moja kwamoja. Mimi kwanza nataka kuelewa hapa inakuwaje wakati tunaujua umuhimu wa Mji Mkongwe yakaachiwa majumba yakaharibika mpaka kufikia hali hii hayatengenezwi mapema wakati mule mnaishi wananchi.

Halafu pamoja na kuwa wizara imewaeleza wapangaji juu ya ubovu wa nyumba hizo, lakini pengine wapangaji hawa hawana pengine pa kwenda, sijui Wizara imechukua hatua gani ya kuwatafutia mahala hawa watu wakaishi japo kwa muda wakati yapo majumba mengi tu ya Serikali na haya majumba yakafanyiwa matengenezo kwa maslahi yetu na maslahi ya hawa wanaokaa.

Halafu (b) kama utaangalia Jaduweli nambari mbili ambayo hii inahusiana na ukaguzi wa nyumba ndani ya eneo la Mji Mkongwe hapa kuna majumba yamekaguliwa, kuna majumba 25 ya Serikali, kuna majumba 18 ya Kamisheni ya Wakfu, kuna majumba 86 ya watu binafsi na jumla ya majumba yote hayo yaliyokaguliwa ni mengi kama ilivyoonesha katika jaduweli. Lakini hapa ninachotaka kuzungumza ni kuwa haya majumba ya Serikali huku katika ukurasa huu wa 18 yalielekezwa kuwa ni jumla ya majumba 26, lakini hapa yamo majumbe 21 tu yenye hali mbaya na manne ndio yenye hali mbaya sana hayakutimia 26. Kwa hivyo, hapa nataka nipate maelekezo. Halafu majumba haya ya watu binafsi Serikali hasa ina mpango gani ya uzungumzaji na hawa watu binafsi ili wakakubali kuondoka na utengenezaji wa majumba haya ambayo yanahatarisha maisha yao na maisha ya wapita njia yatamalizikia vipi.

Jengine Mhe. Mwenyekiti, niende katika nyumba tatu maarufu ambazo zinafanyiwa matengenezo, hapa kuna ukarabati wa jengo la *People's Palace*, hili jengo ni muhimu sana, hili jengo ni la historia, hili jengo linavutia, hili jengo linahitaji kuenziwa, sijui na *people* 's' inakaa baada ya 'e' au inakaa baada 's'. Kwa sababu hii *comma* hukaa baada ya 'e' kama hili jengo ni la mmiliki wa mtu mmoja lakini ikija 's' ndio comma ambayo inaitwa *apostrophe* itakuwa ni la watu, naomba kwanza nipate maelekezo hayo.

Mhe. Mwenyekiti, sasa kwa mujibu wa taarifa zilizokuwa hapa Mhe. Mwenyekiti, ni kuwa Mamlaka imeliezua na kuliezeka upya paa lililokuwa likivuja katika Ofisi ya Naibu Katibu Mkuu wa Baraza la Mapinduzi liliopo Forodhani, pia, Mamlaka imefanya matengenezo na marekebisho ya eneo linalotarajiwa kuwa ukumbi wa huduma ya chakula katika jengo hilo la *People's Palace* na mazingira yake.

Mhe. Mwenyekiti, mimi ninashukuru kwa juhudi hiyo ya wizara ya matengenezo, lakini ukija chini imeandika kuwa;

"Aidha, mamlaka ilifanya ukaguzi wa jengo la *People's Palace* na kuona kuwa ukuta wa kusini wa jengo hilo uko katika hali mbaya."

Mhe. Mwenyekiti, zaidi ya matengenezo hayo kuna ukuta wa kusini uko katika hali mbaya sana na Mamlaka imechukua hatua ya kuweka miega katika kona ya kusini, yaani magharibi ili kusaidia kuta hizo pamoja na kuweka mihimili, yaani *vertical support* ndani ya chumba cha chini cha ghorofa ya kwanza kuzuia dari ya nyumba hiyo.

Sasa Mhe. Mwenyekiti, kumekuwa na matengenezo lakini mimi bahati mbaya hii nyumba sijaiona, lakini kuweka mega hii na hizi *vertical support,* kinachofuatia baada yake ni kitu gani nataka nijue. Na kama imefanya hivyo kwa sababu wizara haina fedha ya kutengeneza hizo sehemu zilizobakia mpaka ikabidi ifanye hivyo, tupe maelekezo imechukua hatua gani kutokana na umuhimu wa kuwepo jengo hili la *People's Palace*.

Jengine Mhe. Mwenyekiti, ni hili Jengo la Ajabu, yaani Beit-al Ajab, hili jengo ni la historia, vile vile ni la kivutio na hasa kwa pale lilipo kwenye bahari, yaani ukiwepo kwenye bahari huku unaliona vizuri sana ni kivutio kizuri sana. Sasa jengo hili pamoja na kuwa kuna mtaalam huyu wa masuala ya uhifadhi kutoka Oman ambaye alikuja mwezi wa Februari na kufanya majadilianona uongozi wa Mamlaka ya Mji Mkongwe pamoja na wataalam wa Makumbusho Zanzibar. Majadiliano ambayo Mhe. Mwenyekiti, yamepelekea mapendekezo ya ukarabati huo yawe kwa awamu, yaani yawe *phase* baada ya *phase*.

Vile vile, mapendekezo haya yamepelekea marekebisho madogo madogo ya ramani pamoja na gharama ambayo Mamlaka imeshakamilisha na kuwasilisha nchini Oman. Niipongeze wizara kwa kuchukua hatua kubwa hii mpaka kupata mtaalam huyu na kuja kuona hapa na kufanya makisio. Lakini zaidi ya maelezo hayo haikuelezwa hatua yoyote ambayo inaendelea ambayo imo katika uwezo wetu ya kulifanya marekebisho jengo hili ambalo ni muhimu sana na linaendelea kuporomoka.

Kwa hivyo, kwa jengo hili pamoja na hatua iliyochukuliwa na Wizara, namuomba Mhe. Waziri, anieleze hasa zaidi ya kuwa imeshawasilisha hayo makisio na gharama na kadhalika, kuna mpango gani hasa wa kuona kuwa jengo hili halitosubiri kwa sababu unapopeleka makisio hatujui ni lini utekelezaji utaanza, haitosubiri ikaja ikatokezea hatari ya jengo hili kuanguka na kutokuwa la kuweza kutengenezeka tena wakati ni jengo muhimu sana la kihistoria na lina mambo ya kuvutia tuone, ni namna gani wizara imechukua *seriousness* ya kuona jengo hili halitapotea ovyo. Kwa sababu hii iliyopo hapa ni mipango na wenzetu wanasema; "mipango si matumizi".

Mhe. Mwenyekiti, la mwisho kwa sababu ya majengo, naomba nizungumze jumba la reli kwa hali lilivyo na hatua ambayo imechukuliwa bado haijaonekana kuwa kuna nia ya kulifanyia marekebisho lakini liko katika hatari kubwa sana na lipo katika mahala pabaya sana. Kwa hivyo, naomba na naungana na wenzangu waliotangulia kuzungumza, kama kuna mpango wowote wa kuweza kubadilisha umiliki ufanywe, apewe mtu mwenye uwezo alishughulikie kwa manufaa yetu kwa uchumi wa nchi na manufaa watakayokuwa wanaishi mule ndani. Hilo nimalize kuhusu mambo ya majengo.

Mhe. Mwenyekiti, sasa nikitoka hapo niende kwenye Programu ya Usambazaji Maji Vijijini ambayo hii utaikutia katika ukurasa wa 22 na 23 kwenye 56 na 57 na kwenye jaduweli nambari 3 kama ifuatavyo:-

Mhe. Mwenyekiti, hapa kwenye Programu ya Usambazaji wa Maji Vijijini, imeelezwa kuwa;

"Serikali inaendelea kuwapatia maji safi na salama wananchi waishio vijijini katika umbali usiozidi mita 250..." na mambo mengine yameendelea.

Mhe. Mwenyekiti, kwanza ninashukuru kuwa wizara huo ndio msimamo wake kuona kuwa haizidi mita 250 wananchi wanapatiwa maji safi na salama. Lakini pamoja na nia safi iliyoko bado kuna sehemu tatizo la maji ni gumu sana na hata wananchi hawaamini kuwa pamoja na kuwa Serikali yetu ya Mapinduzi imeshatimiza umri wa miaka 51 na kifungu cha 56 kinasema mambo yote haya ya

utekelezaji ni pamoja na maelekezo ya Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2010 na ninaamini hii CCM haina ubaguzi inataka watu wote waweze kufaidika katika jambo lolote kwa njia ya usawa kwa wote, sisemi haki sawa.

Mhe. Mwenyekiti, sasa katika jimbo langu mimi ninasikitika sana kuwa mpaka leo nina maeneo tena maeneo mengi hayapati huduma hii ya maji. Mfano nianze tu Mtambwe Kusini. Mtambwe Kusini kuna kiiji cha Makoongeni pale pana skuli ambayo ni kuanzia darasa la kwanza mpaka darala la kumi na mbili, pale pana hospitali, pale pamejengwa nyumba ya daktari kutokana na umuhimu wake, pale ni mahala *isolated* na kijiji chenye watu wengi, kila siku ninapiga makelele, kila siku ninazungumza jambo hili na pale hata mita 2000 zinafika mpaka huko kwa watu wanaopata maji. Kwa sababu maji yanapatikana Kivumoni na maji yanapatikana Mkanjuni ndio vijiji vilivyo karibu na kijiji cha Makongeni.

Sasa ninamuoma Mheshimiwa, anieleze ikiwa lengo ni kuwa watu wapate maji safi kwa umbali uliokuwa haupungui 250, hawa wenzetu wa kijiji cha Makongeni ambao tayari ninashukuru Wizara imeshawapatia umeme, je, suala la maji litapelekwa lini pale? Hiyo ni (a).

Halafu kutoka pale Makongeni kwa kufata barabara mpaka ukafika Kinazini ni kilomita hazipungui mbili na nusu mpaka tatu na huko kuna vijiji chungunzima; kuna Utaani, kuna Mitambuni kuna Kinazini na kadhalika, kote huko hakujafika maji na ikiwa msimamo ndio huu kwa kweli Mhe. Waziri, atanieleza vipi ni lini hasa na vipi na kakusudia nini kuwaondolea watu shida hii ya maji katika vijiji hivi vilioko katika Shehia ya Mtambwe Kusini kama vilivyoondolewa katika shehia nyengine za jimbo langu.

Halafu jengine Shehia ya Mtambwe Kusini Mhe. Mwenyekiti, kiko kisima cha maji kililetewa pampu kubwa ya maji na ingeweza kusambaza maji kwa Mtambwe nzima ya Kusini, lakini kwa bahati mbaya utawala ulikuja ukaitoa pampu ile na kuweka pampu ndogo kiasi ambacho sasa haikidhi haja hata kwa hivyo vijiji vitatu vililivyopelekewa haya maji.

Kwa hivyo, ninaiomba wizara na ninaiomba kwa nia safi kabisa ione kuwa Mtambwe Kusini kuna binaadamu wanahitaji maji na marekebisho ya mwanzo ama katika mawili moja yafanywe; kwanza ama ni kuweka pampu pale Daya ili maji yafike mote kama ilivyo Mtambwe Kaskazini au ni kuchimbwa kisima chengine katika maeneo ambayo wataalam wataona inafaa ili maji yaweze kuenea. Lakini kwa kuweka watu katika hali ile kama kuwa hawana Mwakilishi wa kuwatetea inaonesha huruma sana, kama kuwa wao si sehemu ya Serikali hii tuliyonayo inaonesha vizuri sana. Naomba Mhe. Waziri, tena ninamuomba kwa

nguvu zangu zote aone kuwa atanisaidia kuona kuwa Mtambwe Kusini na maji nako yanapatikana katika huu mpango aliouweka kwa maslahi yetu sote.

Kwa kumalizia suala la maji, tuna kisima cha maji pale Mtambwe Kaskazini na bahati mbaya kwa nia safi Mamlaka ya *ZAWA* walikwenda kukisafisha kikaharibika, lakini ninaipongeza sana wizara haikutimia hata wiki moja kikachimbwa chengine kikubwa na chenye maji zaidi kuliko kile, lakini kwa bahati mbaya sana ile *pump* yake ya zamani ambayo ilitumika kwa kile kisima kikongwe, kwa umeme unaopatikana pale haifanyi kazi ipasavyo, mpaka ikabidi *ZAWA* watuwekee *pump* ya muda ndogo, ili watu wapate umeme angalau kwa mgao na mpaka sasa hivi ndio tunavyoendelea.

Kwa vile tuna *pump* yetu ya zamani, na bado ni nzima, tatizo ni umeme tu ni kwenye mamlaka yao. Kwa hiyo, naomba kwa heshima yote na unyenyekevu, wizara ione kuwa imepeleka mafundi kule Mtambwe Kaskazini, kwanza kwenye kisima na kukiona kisima chenyewe na *transformer* ilipo na ilivyo na kuiona *transformer* yenyewe, kama ni *transformer* yenye matatizo basi ifanyiwe marekebisho. Lakini kama kunahitaji *transformer* ni kwamba uwezo wake ni mdogo kwa kuweza kuifanya *pump* kubwa ikafanya kazi maji yakapatikana.

Kwa hivyo, naomba sana, naomba sana wizara inisaidie kupatikana *transformer* nyengine ndogo ili tuone kuwa kile kisima kinatoa maji ipasavyo kwa maslahi ya wananchi.

Mhe. Mwenyekiti, na ule mpango wa kujenga tangi narudia tena pale ndio iwe ni zizi ambalo litakusanya maji kutoka Daya na maji kutoka Uwondwe yaingie kwenye *tank*, halafu tena yaweze kusambazwa mote, nahimiza kwa sababu itafanya hata hizi *pump* zenyewe ziweze kupumua na kuwa na maisha endelevu.

Mhe. Mwenyekiti, la mwisho katika maji Shehia ya Kisiwani Mheshimiwa na Shehia ya Piki kwanza nishukuru tumejengewa *tank* kubwa pale kwa ule mradi wa Wachina…

**Mhe. Mwenyekiti:** Una dakika tano za ziada.

**Mhe. Salim Abdalla Hamad:** Na *tank* ile tunasikia tu kwamba wizara haina fedha za kutosha ikafanyiwa majaribio na ikaanza kufanya kazi na wananchi wakafaidika na maji.

Kwa hivyo, mradi umemalizika umeshafunguliwa lakini tatizo ni hilo, naomba Mhe. Waziri si kwa tangi lile tu liliopo pale au si kwa mradi ule tu uliopo pale

Bahanasa, na miradi mengine kama hiyo amefanya ushauri gani ili kuona kuwa inafanya kazi na halafu wananchi wanapata maji wanayoyahitaji.

Mhe. Mwenyekiti, kwa vile muda umemaliza naomba kidogo nizungumze katika suala la umeme. Vile vile niishukuru wizara inajitahidi kusambaza umeme japo kwa kadri inavyosambaza inaingia hasara, lakini bado katika jimbo langu kuna sehemu hazijafika umeme.

Mheshimiwa kwa mfano kule kule Mtambwe Kusini; Kivumoni hakuna umeme halafu Mitambuni na Kinazini Mtaani mote hamna umeme, barabara nashukuru tayari iko magari yanafika na kadhalika.

Kwa hiyo, ningelimuomba Mhe. Waziri kama nilivyokuomba kwa maji kwa Mtambwe Kusini na kwa umeme sijui atanisaidia vipi kuona kuwa wananchi walioko kule na wao wanafaidika na suala hili la umeme.

Na kwa umeme kuna Kijiji cha Tondooni Mhe. Mwenyekiti namaliza kiliopo katika Shehia ya Kisiwani kule ndio kabisa umeme hakuna, lakini kwa bahati nzuri kuna sehemu ambayo umeme umepelekwa na wale Wachina walipokuwa wakichimba kisima, hivyo ni rahisi kuuchukua pale ukaupeleka kule kwani wenyewe ni wataalamu.

Kwa hivyo, ningeliomba Mheshimiwa anieleze ni lini na kijiji hiki ambacho wameshafika katika taasisi yake kuomba hili suala watasaidiwa ili waweze kupatiwa umeme.

Mhe. Mwenyekiti, kwa sababu ya wakati naomba nimalizie hapo, na *inshaallah* matarajio yangu ni kupata majibu ya mafanikio kutoka kwa Mhe. Waziri, na kwa sababu nina tamaa hiyo nitamke rasmi naunga mkono hotuba hii mia juu ya mia.

**Mhe. Mwenyekiti:** Waheshimiwa Wajumbe, kabla sijamwita mchangiaji anayefuatia Mhe. Abdalla Mohammed kuna tangazo hapa tumebahatika kupata wageni ambao ni wageni wa Mhe. Spika.

Wageni hawa wametoka *European Centre for Electoral Support* tuna Bibi Anne Sofie Gerhard ambaye ni *Zanzibar Project Manager, may you stand up*, tuna Bibi Victoria Florinder ambaye ametokea katika Taasisi ya *Election Conflict Management Adviser*, *you are most welcome! Thank you.*

**Mhe. Abdalla Mohammed Ali:** Mhe. Mwenyikiti, ahsante na mimi kupata fursa karibu ya Magharibi haya kusema machache.

Mhe. Mwenyekiti, kwa ujumla tumeshasema mengi na wengine tunajiandaa kwamba tena tusiwemo humu tukawa tunaendelea kusema, lakini sasa kuna waliosikia na wakatekeleza na kuna ambao bado hawajasikia na hawajatekeleza.

Sasa kwa mwaka huu Mhe. Mwenyekiti, naona tuendelee kusema kidogo tu *inshaallah,* kwa sababu yale ya mwisho tumeambiwa huenda yakawa yana kheri zaidi kuliko yale ya mwanzo.

Mhe. Mwenyekiti, mimi kuna mambo machache tu katika mpango huu wa Wizara ya Maji na Nishati ambayo nataka nikumbushie tu, lakini kwa ujumla katika wizara ambayo nahisi imejitahidi sana katika kutuonesha utendaji wake ni wizara hii. Kusema kweli kuna mambo ambayo ukitembea vijijini na mijini unayaona, isipokuwa tu wanahitajika watembee nchi nzima ambayo nahisi uwezo huo kwao ni mdogo. Lakini kwa ujumla naweza kusema kwamba wametuonesha kwamba wao ni watendaji na wala si wababaishaji.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nianze kidogo kuhusu hii Idara ya Ardhi na Usajili. Mheshimiwa hivi sasa kuna dhana kwamba ardhi ni mali ya serikali, na wananchi wengi kwa ujumla dhana hii wanaisikia tu lakini ufahamu wake bado ni mdogo.

Kwa hiyo, mimi nahisi ushafika wakati hivi sasa dhana hii ikaelezwa kwa wananchi hasa tunaposema kwamba ardhi ni mali ya serikali kusudio ni nini? Ukiangalia migogoro mingi na madai mengi yanayotokea yanatokana na dhana hii, watu wanafika Mahakamani, watu wanafika maofisini, mawizarani kudai haki wakitambua kwamba haki hii ni yangu lakini kinyume chake haki ile pengine sio yake, na hiyo inatokana na kutoelewa nini maana hasa ya ardhi mali ya serikali.

Kwa hiyo, nahisi tumeshafikia karne sasa ya kwamba wananchi wa Zanzibar dhana hii waweze kuielewa ili kuondosha ile misururu ya kupelekana Mahakamani na kufikishana wizarani kudai haki ambazo pengine ni zao au sio zao.

Mhe. Mwenyekiti, jengine ninalotaka kusema linahusiana na hiyo hiyo hasa Mahakama ya Ardhi. Hivi sasa kuna kesi nyingi sana Mhe. Mwenyekiti zilizopo katika Mahakama ya Ardhi, na ukiangalia Mahakama zetu hizi nafasi ni ndogo sana.

Ukienda pale kwenye Mahakama utakutia watu wengine wako barabarani, wengine wako nje, wengine hujui hata wanakaa wapi, huyo Hakimu wenyewe hana raha ya kuendesha kesi. Kwa hiyo, nahisi sasa ipo haja na watu hawa wakaonekana ili wale wanaokwenda pale wakajihisi kwamba wamekwenda Mahakamani, na yule Hakimu naye akaona kwamba ah kweli mimi ni Hakimu na nastahiki kukaa katika sehemu hii kuendesha kesi.

Mhe. Mwenyekiti, lakini katika hilo pia kuna wale ambao wanaitwa wazee. Mhe. Mwenyekiti, hadi hivi sasa wale wanakwenda katika mfumo wa kufikirika tu, hakuna *vote* maalum ambayo imetengwa kwa ajili ya watu wale.

Nafikiri karne sasa imeshabadilika tunahitaji sasa watu wale na wao tuwawekee *vote* maalum; ule utaratibu wa kwamba wewe kubahatisha bahatisha sasa tuondokane nao, nahisi na wao watajisikia kwamba ni watu waliothaminiwa na wataendesha kazi zao kwa utaratibu bila pengine kupokea mambo ya rushwa na mengineyo. Kwa sababu wakiwa wanajua kwamba mimi malipo yangu yatakuwa yana uhakika, basi na wao taratibu zao zitakuwa zinakwenda vizuri sana.

Mhe. Mwenyekiti, katika Idara hii hii kuna ofisi ambayo inaitwa Ofisi ya Mrajis wa Ardhi. Mheshimiwa ofisi hii ina zoezi ambalo inaliendeleza na zoezi hili ni la kusajili. Sasa hili zoezi ni zuri sana, na imani yangu kwamba kama zoezi hili litaendelezwa basi migogoro mingi ya ardhi itapungua, sisemi kwamba itakuwa haipo lakini itapungua.

Kwa hiyo, namuomba Waziri kama kuna *vote* na najua iko katika mgao, basi iwaone watu hawa waingiziwe pesa ili hili zoezi liwe linakwenda vizuri sana. Kwa sababu nina imani hivi sasa limesimama, kwa hiyo kusimama kwake huenda kukasababisha matatizo na watu wataendelea kudaiana huko. Sasa ili kuondosha hizi longolongo za wananchi, ni vyema sasa zoezi hili likawa endelevu lisimame ili kila mmoja ajue haki yake na atakapokwenda Mahakamani mwengine atakuwa ana uthibitisho. Kwa hiyo, ni rahisi itakuwa sasa kwa kesi zetu ambazo zinapelekwa Mahakamani kufanya taratibu za maamuzi, si hivyo itakuwa bado tunampa kazi au tunazipa kazi Mahakama zetu za Ardhi.

Mhe. Mwenyekiti, mimi ni matarajio yangu kwamba labda awamu mbili zinazokuja hii migogoro kama utaratibu huu utakwenda kama kawaida, basi Mahakama za Ardhi huenda tukazifunga kwa sababu kazi itakuwa haipo kila mmoja atakuwa anajua chake bila ya watu kupelekana Mahakamani.

Mhe. Mwenyekiti, jengine ninalotaka kusema ni kuhusu Mamlaka ya Maji. Kwa ujumla serikali ilifanya juhudi kubwa sana ya kuwatafuta ma-*comrade* wenzetu wa China kuja kutusaidia katika upatikanaji wa maji safi na salama katika miji yetu na vijiji vyetu.

Kwa ujumla miji imepata miradi na vijiji pia vimepata miradi, isipokuwa tu Mhe. Mwenyekiti, nilikuwa nataka kugusia kuhusu mradi mmoja ambao ulikuwa uko katika Kijiji cha Wambaa. Mradi ule Mhe. Mwenyekiti, ninavyofahamu mimi ulikuwa ukamilike kwa kuziboresha karibu kilomita 17, lakini kwa bahati mbaya

hadi hivi sasa miundombinu ya maji katika kijiji kile imefikia kilomita 10 tu, kilomita 7 bado hazijakamilika. Sasa sijui hapo katikati Mhe. Waziri palitokea nini, ingawaje tumewahi kuonana mara nyingi na kulizungumzia suala hili lakini ufumbuzi wake haujapatikana.

Mhe. Mwenyekiti, unajua binadamu tumeumbwa tukiwa na choyo, na wananchi wengi walikuwa hawajaipata huduma hii kwa muda wa miaka karibu 50, sasa ukiona jirani yako huduma ile ameshaanza kuipata wewe bado unajenga roho nyengine.

Kwa hiyo, Mhe. Waziri mimi ningemuomba tu ninavyofahamu kwamba mradi ule ulikuwa ukamilishe kilomita 17, lakini na wananchi walikwishaona kwamba sasa maji yanataka kutufikia, kwa sababu hata mitaro ilikwishachimbwa kwa ajili ya kuzika mabomba, lakini bahati mbaya hadi hivi leo mradi ule tayari umeshazinduliwa baadhi ya wengine wanafaidika lakini wengine bado.

Sasa hebu tupe utaratibu sijui katika awamu hii tutaendeleza ule upatikane wa miundombinu ili na wananchi wale ambao labda huduma ile walikuwa tayari wameshaitilia tamaa wameikosa, na labda wataipata wakati gani.

Mhe. Mwenyekiti, tunakumbuka na kila mmoja anafahamu kwamba mwezi wa Ramadhani huwa tunakuwa taabani, na pia huwa tunatumia maji kwa wingi, sasa utaratibu nafikiri ungefanyika mapema japo tunaanza siku tano zinazokuja mbele, lakini nafahamu kwamba wizara hii ina mabingwa na wataalamu wanaweza wakaandaa taratibu zao za kufikisha huduma hii kwa wananchi mara moja.

Mhe. Mwenyekiti, lakini mara nyingi tunakuwa na miundombinu, na visima vyetu huwa vinatumia mashine wengine tunaziita *pump*, sasa mimi sikitiko langu ni kwamba mara nyingi kwamba *pump* imeharibika katika kisima huwa tunachukua muda mrefu kufanya *replacement*, tunachukua siku nyengine mpaka siku 10.

Utaratibu hivi Mhe. Mwenyekiti, ni kwamba wananchi hawalipi maji lakini wanachangia, sasa inafika hadi wanajiuliza ah mimi mbona naambiwa nichangie na nachangia. Sasa inafikaje kwamba siku 10 tena au 15 ikawa pengine bomba tu imepasuka pahali ikawa haijafanyiwa *replacement* au mashine hizo za *pump*.

Kwa hiyo, naomba hivi tuwe na utaratibu mwengine kwamba tufanye tuwe tuna kitu ambacho kipo, pale itapotokea kwamba kumetokea tatizo basi pale pale wananchi waone kwamba ah ile huduma tunayoitoa, ule mchango wetu tunaoutoa ah kumbe upo hauendi katika mifuko, hauendi *wrong pocket*.

Kwa hiyo, kwa vile hili ni suala la kuwajengea imani wananchi, basi tufanye hivyo tujaribu mapema kwamba tunajua kuwa *pump* aina fulani ndio inayohitajika kisima fulani tuweke kitu ambacho kipo wakati wowote kikiharibika kile tunafanya *replacement* ndani ya masaa 24 watu wanapata huduma, tubadilikeni tena wakati sio tena wa kumuweka mtu mjini siku 15 hajapata maji.

Mhe. Mwenyekiti, halafu katika hili pia siku ya Jumamosi na Jumapili kunapotokea *breakdown* siku ya Ijumaa ina maana wewe tena hata ukapeleka ripoti usubiri mpaka siku ya Jumatatu.

Haya mambo haya tena tunakwenda katika *century* nyengine, sasa haya tuyaangalie kwamba ni changamoto na hivi sasa kwa vile na sisi tunachangia chochote katika uendelezaji wa miundombinu hii, basi tuhisi kwamba zile pesa zetu zinatumika vizuri na ile huduma inapatikana kwa wakati.

Mhe. Mwenyekiti, jengine ninalotaka kusema ni hili la uendelezaji na utekelezaji wa Mradi wa Nishati Mbadala. Kama nilivyosema mwanzo Mhe. Mwenyekiti, ni kwamba awamu inamalizika na kusema kweli mimi nasikitika kidogo kwamba tunakuwa hatuko *systematic* kwamba tunajua kuwa sisi tunakwenda wapi.

Mheshimiwa mwaka 2011 hapa tulilетewa *concept* kwamba sasa serikali ishaandaa utaratibu wa kutaka kutafuta nishati mbadala ya umeme. Lakini ilipofika 2012/2013 *concept* ile ikabadilika tukaletewa *concept* nyengine, kwa hivi sasa tushapata wataalamu ambao wamekwenda kuangalia Matemwe, Nungwi, Makunduchi, sijui Micheweni kwa ajili ya kuleta umeme wa upepo.

Mwaka huu tena tushaletewa *concept* nyengine, hebu tunasimama wapi hizi *feasibility study* hazijamalizika tu, tukajua sasa tunashika ipi? Kwa sababu *from 2011* mpaka leo 2015 bado tuna *feasibility study* tu, sisi tunahitaji tupate umeme mbadala hivi sasa! Sasa hizi *concept* hebu tuzifanye iwe *concept* moja *from the beginning* tujue tunakwenda katika *concept* hii tuimalize. Lakini mwaka 2011 mnatwambia tunataka umeme wa jua, 2012 tunataka hiki, *feasibility study* umeme wa upepo tunakwenda wapi?

Mhe. Mwenyekiti, mimi nafikiri tuwe tuna *system* maalum kwamba tunataka kwenda katika umeme wa aina fulani, hizo *feasibility studies* zifanywe zimalizike tujue huduma imetufikia, lakini kwa mtindo huu tunaokwenda Mheshimiwa hatutofika, kwamba kila mwaka tubadilishe *concept* ziende kwa Makatibu Wakuu waje wataalamu wengine wafanye *feasibility study* waondoke, wakishaondoka waje wengine wafanye *feasibility study*, hakuna kitu *tangible* tunachokigusa.

Kwa hiyo sasa tuamue awamu hii ishamalizika Mheshimiwa sawa, lakini awamu zinazofuata kama mara hii tumeshaweka kwamba tunakwenda katika kitu fulani *concept* hii basi i-*materialize*, tukisha- *materialize* ndio tutajua tunafanya jambo jengine, kwa kubadilika kila mwaka itakuwa ni kama kuja hapa sasa ukatwambia tu kwamba mwaka huu tutafanya hivi, tunawaimbia nyimbo watoto. Leo unanambia baba yangu wee kazaliwa wapi, bibi yako sijamuonapo, hakuna!

Jengine ni kuhusu Shirika la Umeme. Kule kisiwani Pemba mimi nawasifia sana mwaka huu wao wameanza kubadilika. Wenzangu wanasema wame- *brain storm,* yaani wao wameipiga hasa ile kwamba wanajua sasa nini wanachokifanya.

Ukienda Shirika la Umeme hivi sasa unajua kwamba wao sasa wako kama ni shirika ambalo labda wamejipanga *in five years* waweze kuwa wao wenyewe sasa wanajitegemea. Sasa utaratibu huu wasije wakaurudisha nyuma.

Hivi sasa wameandaa taratibu za kuwakopesha watu wafanye haraka haraka, isiwe tena mtu anataka kuungiwa umeme akae miezi aa, kama wewe unataka kuungiwa umeme mafundi wapo kuna vijana waliosoma hapo wanaweza wakawachukua *part time*, mtu anataka kuungiwa umeme tena ajaze fomu mpaka fomu zibadilike rangi, haya yaondoke tena tufanye *computerization* kila kitu, ukienda pale nani, fulani unaangaliwa kwenye kompyuta kweli upo sawa, haya Mheshimiwa.

Mhe. Mwenyekiti, jengine ni kwamba mafundi wetu hawa ambao wanakuwa wako *standby* bado wangali kidogo mimi nafikiri. Kwa sababu zinatokea kesi unakwenda pale katika Shirika unaripoti unaambiwa kuna kesi zisizopungua 40 *within one hour*, lakini mafundi wetu ni wanne au watano gari zetu mbili. Sasa tuandae utaratibu mwengine tuweke watu wa kutosha wa kuweza kutatua hayo matatizo madogo madogo yanayotokea katika mitaa yetu.

Mhe. Mwenyekiti, kama nilivyosema mimi mara hii nataka nipongeze tu, kwa sababu miaka mitano tena ishamalizika nishaona mengi. Kwa hiyo, kwa hayo machache mimi naunga mkono.

**Mhe. Abdi Mosi Kombo:** *Bismillahi Rahmani Rahiim*. Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi kwa jioni ya leo na mimi kuchangia hotuba hii ya Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati.

Kabla ya hapo namshukuru Mwenyezi Mungu vile vile kwa uwezo wake wa kutuwezesha kufika hapa jioni ya leo tukiwa tunachangia, si ujanja wetu ila ni uwezo wa Mwenyezi Mungu, na mimi namuomba Mwenyezi Mungu anijaalie hapa nichangie kama nitavyoweza.

Mhe. Mwenyekiti, mimi sina mchango mkubwa kwa sababu mengi yameshazungumzwa hapa juu ya maji na umeme. Mimi mchango wangu nitaanza ukurasa wa 12, ibara ya 31, Idara ya Mipango Miji na Vijiji.

Mhe. Mwenyekiti, wakati wa mwaka 1964 baada ya Mapinduzi ya Zanzibar Rais wa Kwanza marehemu Mzee Abeid Amani Karume alituwekea mipango miji kama tunavyoiona Michenzani, Kiinua Miguu na Kikwajuni kwa Mjini. Kwa shamba kule Chaani, Bambi, Makunduchi na kwengineko na Pemba ni Wete, Chake Chake, Mkoani na Mtambile.

Kwa hivyo, nyumba zile zilipojengwa na Mhe Rais wa Awamu ya Kwanza ndani yake mna umeme, maji na barabara zimepita kwa *line*. Lakini baada ya kuondoka duniani mipago miji ile imekufa, sasa ikawa wananchi wanajenga tu wanavyotaka wenyewe, sasa ikawa ujenzi wenyewe balozi anatoa kiwanja hata mimi nikiwa nimezidi zidi mtaani nina uwezo natoa kiwanja ikawa tena mkorogovyogo, hapana ujenzi wa uhakika.

Hapa kitabu kinasema kwamba, "Idara ya Mipango Miji na Vijiji". Sasa namuomba Mhe. Waziri aje atueleze mipango miji hii iliyomo katika kitabu hiki itakuwa namna gani, kama ile ya Mhe. Rais wa Kwanza au itakuwa vipi. Kwa sababu ujenzi wa leo tuliokuwanao Zanzibar umeshamaliza ardhi, sasa hivi serikali ikitaka kupanua barabara inabidi ibomoe nyumba zilizoko barabarani zote, na itakuwa gharama kubwa sana, hata zile barabara zetu zilizokuwa finyu kwa sababu ya kutokuwa na mipango miji.

Tatizo linalotupata kila siku kwamba wananchi wanadai maji na umeme kwa sababu ile mipango miji imekosekana. Mipango miji ya mara ya kwanza ya Marehemu Mzee Karume ilikuwa haina tatizo, unaikuta nyumba imejengwa tayari maji, umeme vipo; lakini sasa ujenzi wetu wa kileo ni wa kiholela. Kwa hivyo, Mhe. Waziri namuomba aje atueleze mipango miji hii ya mwaka huu itakuwa namna gani.

Mhe. Mwenyekiti, nikiendelea niende katika Mamlaka ya Maji (*ZAWA*). Kwanza naipongeza Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar inayoongozwa na Rais wetu Dkt. Ali Mohamed Shein kupitia Wizara ya Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati. Kule kwetu Matemwe imetujengea *tank* kubwa sana la maji lakini bado maji yale hayajatumika kwa wananchi.

Kwa hivyo, namuomba Mhe. Waziri awahakikishie wananchi wa Matemwe maji yale yatatumika lini? Kwa sababu kama Wajumbe wenzangu walivyosema hapa Mwezi wa Ramadhani ukija huwa na tatizo kubwa linalotupata la maji, aghalabu

inakuwa kipindi cha Kaskazi. Wilaya ya Mjini husikia kwamba huitwa masheha wakasambaziwa maji kwa magari lakini kwa shamba hakuna.

Kwa hivyo, namuomba Mhe. Waziri atufanyie mpango na sisi hasa kule Matemwe wakati wa Mwezi wa Ramadhani tupate mpango huo wa kusambaziwa maji pindi ikiwa maji bado hayajafika kule kwetu. Mhe. Waziri hili jambo naliomba sana, kwa sababu na sisi Mwezi wa Ramadhani tunapata tabu ya maji katika vijiji vyetu. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, kifungu cha 57 Programu ya Usambazaji wa Maji. Pale Mamlaka ya Maji kifungu cha 56 hii hapa kifungu cha 57 ukurasa wa 22 Usambazaji wa Maji Vijijini.

Mhe. Mwenyekiti, katika jimbo langu la Matemwe kuna vijiji nitavitaja hapa na Mhe. Waziri atavielewa hivi bado havijapata maji. Kijiji cha kwanza kinaitwa Kigomani Juu umaarufu wake kunaitwa kwa Faki Kibuku bado hayajafika maji.

Halafu katika vijiji vyengine kusini ya Matemwe anavijua Mhe. Waziri Mikuuni, Jomba, Kigomaji, hivi vijiji bado havijafika maji. Mhe. Waziri namkumbusha tena kwamba *ZAWA* ilichimba kisima katika kijiji cha Mikuuni Mhe. Waziri anakijua na Mkurugenzi anakijua, bado kisima kile toka kuchimbwa hakijapata huduma yoyote ya kusambazia wananchi maji. Kwa hivyo, namuomba kisima hiki akitambue na bajeti ya mara hii kifanye kazi ili wananchi waondokane na matatizo.

Mhe. Mwenyekiti, nikizungumza tena katika huduma za maji katika Jimbo la Matemwe katika Shehia ya Kijini, Mutende bado haijafikiwa na maji mpaka sasa hivi.

Kwa hivyo, namuomba Mhe. Waziri akija anihakikishie kwamba lini na siku gani vijiji hivi nilivyovitaja vitapata huduma ya maji. Kwa sababu Mwezi wa Ramadhani ukifika hakuna huduma yoyote, ni tatizo! Sasa namuomba Mhe. Waziri aje anihakikishie wananchi wa Matemwe kule wanamsikia na mimi ananisikia nawaombea usalama wa maji upatikane.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nikimalizia katika mchango wangu kwa sababu wizara yetu hii imeshajitahidi sana, lakini bado kidogo isuuzesuuze.

Mhe. Mwenyekiti, huduma za umeme katika jimbo la Matemwe Shehia ya Kandwi, Matemwe Kusini, Kijini, Mbuyutende, bado havijafika umeme. Namuomba Mhe. Waziri atambue kwamba bado umeme haujafika sehemu hizo nilizozitaja zinahitaji huduma za umeme.

Mhe. Mwenyekiti, kwa kumalizia mchango wangu namalizia kwa kumuomba Mhe. Waziri atuhakikishie kwamba wakati wa Mwezi wa Ramadhani tatizo la maji kwa upande wa kwetu Matemwe na sisi atufanyie mpango; ikiwa maji yale ya bomba hayajafika, basi na sisi tupate maji ya mgao.

Mhe. Mwenyekiti, namalizia kwa kusema mimi naunga mkono hotuba hii ya Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati, nakushukuru.

**Mhe. Mohammedraza Hassanali Mohammedali:** Mhe. Mwenyekiti, awali ya yote napenda kuchukua nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu aliyeweza kutupa pumzi hizi tulizokuwanazo ambazo ndio tunazoringia sisi Wajumbe ambapo ndio amana yake. Vile vile nichukue nafasi hii kuwashukuru wenzangu na kadiri ambavyo jua linavyotua.

Mhe. Mwenyekiti, napenda kuchukua nafasi hii kumshukuru Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati kwa hotuba yake nzuri pamoja na kamati, hotuba ambayo inalingana na hekima, busara na usikivu. Napenda kumpongeza mzee wangu Maalim Ramadhan Abdalla Shaaban pamoja na watendaji wake.

Mhe. Mwenyekiti, Serikali yetu ya Mapinduzi ya Zanzibar imeshafanya mambo mengi sana katika sehemu zote za maji, umeme, ardhi, afya na miundombinu. Mambo yote kwa jumla lakini na changamoto zipo.

Changamoto hizi Mheshimiwa mengi yanatokana na hali ya uchumi inayotukabili. Mimi wizara hii pamoja na taasisi zake za maji, umeme, Mamlaka ya Mji Mkongwe na sehemu zote zinazohusika napenda kuwapongeza watendaji wake wote wakiongozwa na Mhe. Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na wasaidizi wake wote. Kwa kweli wana usikivu mkubwa, wana hekima na busara katika kila jambo linapotokea.

Mhe. Mwenyekiti, sote sio wakamilifu, lakini wenzetu hawa katika umeme, ardhi na mambo mengine kwa kweli niwapongeze kwa uvumilivu wao. Kwa sababu sisi viongozi wakati mwengine tunapokuwa tunatoka tunakuwa tunajisahau, lakini kwa kweli watendaji hawa wanakuwa wasikivu sana katika kila sehemu. Kwa hivyo, Mhe. Mwenyekiti, mimi nilikuwa niombe wizara hii maana ni wizara yetu sote tunatakiwa sote kushirikiana kwa pamoja.

Mhe. Mwenyekiti, wizara hii inagusa uhai wa binadamu na uhai wa viumbe ikiwemo wanyama, maana ukisema maji ni jambo ambalo sote linatugusa, huwezi kutoa hata mifugo yetu kama hakuna maji; wanyama wanaweza kukonda na wakapungua thamani yake. Sasa mimi niiombe serikali iweke kifungu maalum kwa wizara hii, nina sababu zangu Mhe. Mwenyekiti.

Bajeti imesomwa lakini changamoto ninayoikuta sana katika wizara kwa mfano kwa umeme, ardhi kwanza ni nyenzo za kufanyia kazi; halafu sehemu za usafiri magari pamoja na hizi *pump*.

Mhe. Mwenyekiti, *pump* haimo ndani ya bajeti, kwa mfano *pump* imeungua sehemu iliyoungua kwa sababu haina bajeti inaweza ikafika *pump* za siku hizi shilingi milioni kumi au kumi na tano, matokeo yake wakaazi waliokuwa katika maeneo yale maji yapo ya kutosha lakini uwezo wa wizara haupo kwa sababu haipo kwenye bajeti, inakuwa ni vigumu sana.

Sasa Mhe. Mwenyekiti, ningeliomba wizara hii lazima tutafute ufumbuzi wa mambo haya yanapotokea. Kwa kweli Mhe. Mwenyekiti, sote sisi tuna huruma sana hasa katika mambo haya yote tunayoyajadili humu ndani. Lakini tusipokuwa katika mazingira mazuri leo Mhe. Mwenyekiti, kuna sehemu Mwenyezi Mungu ndiye mwenye nguvu zake analeta dharuba unaambiwa kuwa *transformer* tatu kwa upepo tu, ni kazi ya Mungu huwezi kuizuia, *transformer* zimekwenda. Shirika halikupanga bajeti ile lakini sisi kama wananchi tunakuwa wakali mno. Kwamba bwana hii serikali gani, sijui wizara gani imefeli. Lakini mtu anasahau kwamba yule tunaye Mwenyezi Mungu ambaye ndiye anayetuneemeshea neema kubwa kubwa na ndogo ndogo inakuja mvua ambayo inaathiri sehemu nyingi sana.

Sasa Mhe. Mwenyekiti, mimi ningeliomba serikali ikajipanga kuona kuna vifungu maalum katika mambo ya *water pump,* mambo ya *transformer* ambayo yanajitokeza na Mwenyezi Mungu ndiye mwenye kuyapanga. Kwa sababu unaweza kununua *water pump* leo ikaja ikaungua matokea yake inachukua wiki tatu, wiki nne, miezi miwili kutokana na hali ilivyo.
Sasa Mhe. Mwenyekiti, mimi ningeliomba wizara hii lazima tutafute *solution* ya mambo haya. Shirika la Umeme linafanya kazi kubwa sana Mhe. Mwenyekiti, na Shirika la Maji *ZAWA* linafanya kazi kubwa sana, ndugu zetu wa Ardhi hawa katika upimaji na migogoro mingi sana wakati mwengine ni nyenzo ambazo zinakosekana.

Sasa Mhe. Mwenyekiti, katika haya kama hatukujadili vitu ambavyo tunaona vipi tunaweza kuisaidia wizara hii, na serikali ikaipangia namna gani ya kuweza kuondosha matatizo kama haya. Bado tatizo tutakuwa nalo na matokeo yake mafundi, shirika litabeba lawama ambayo wala halina makosa.

Kwa hivyo, mimi nilikuwa nataka kutoa mawazo kwa serikali, kwamba sisi wafanyabiashara Mhe. Mwenyekiti, *alhamdulillah* sasa ningeliomba tu Shirika hili na wizara hii tubadilike katika kusaidiana katika vitu kama hivi vya *pump*, nguzo, wakati unapotokea upepo, *transformer*, ili kuweza kusaidiana na wizara hii.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nashukuru wizara hii katika kipindi changu cha miaka mitatu nilivyowatumikia wananchi wa Jimbo la Uzini nimepata mashirikiano makubwa sana, na kwa sababu na mimi nilikuwa tayari kuisaidia serikali na wizara. Kwa mfano pale Bambi katika uwanja wa mpira kulikuwa na nyumba karibu mia moja na sehemu ya michezo.

Nilipokwenda kwenye Shirika la Umeme basi Meneja akanambia Raza hii kuna gharama kubwa lakini kama Mwakilishi basi changia *transformer*. Sasa uzuri wa jambo ni mashirikiano, na mimi haikufika wiki nikapeleka *transformer*. Lakini baada ya wiki na mimi nikaletewa umeme kuna *give and take, scratch my back and I'll scratch yours!*

Sasa Mhe. Mwenyekiti, hivyo ndio vitu vya kusaidiana, sasa mimi ningeliomba tubadilike ili tuweze kuona namna gani tunaisaidia serikali katika mambo mengi sana.

Mhe. Mwenyekiti, katika vitu vyote hivyo bado nina kilio changu *"mkaa na maiti haachi kulialia"*. Bambi Kijopwe Mhe. Mwenyekiti, nilikuwa naomba tu na niko tayari kushirikiana wakati wowote kwamba bado umeme ni tatizo, maji ni tatizo. Sasa ningeliomba tu kwa uwezo wa Mwenyezi Mungu leo mwezi 25 ya Shaabani wafanye utafiti, halafu tuone tunachangiana vipi katika kuwasaidia wananchi wa Bambi Kijibwe mtu na sehemu nyengine ili kuona namna gani tunaweza kusaidiana.

Mhe. Mwenyekiti, katika vitu vinataka mashirikiano, lakini ukisema tu maji hamna tatizo lazima tupate mashirikiano na tuone namna gani ya kuweza kusaidiana katika vitu kama hivi.

Mhe. Mwenyekiti, kwa bahati nzuri wenzetu hawa katika sehemu mbali mbali ya upimaji ardhi ya umeme ya maji *wallahi* Mhe. Mwenyekiti, wana utalaamu mkubwa sana Mwenyezi Mungu kawapa kipaji, tuna hazina kubwa sana sisi Wazanzibari kwamba watu wana uwezo wanaweza kufanikisha, lakini panakosekana siku nyengine bajeti, panakosekana na vitendea kazi. Kwa sababu ukimwambia leo *ZAWA* maji hakuna, atakwambia sina usafiri au mafuta au bajeti.

Kwa hivyo, mimi naomba Mhe. Waziri tusaidiane, na mimi niko tayari kusaidia katika sehemu yoyote ya Unguja na Pemba, ndio utamaduni wetu sisi tuliokuja humu ndani. Tumekuwa ndani *Zanzibar as cosmopolitan* bila ya kujali rangi, kabila na dini na ndio tulivyo humu ndani katika Baraza hili la Wawakilishi.

Kwa hivyo, niko tayari kushirikiana, na mimi kutoa na kuwashirikisha Wazanzibari walioko nje ya nchi kuona jinsi gani tunaweza kuisadia Zanzibar hasa katika masuala ambayo yanawakumba wananchi wetu vijijini.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nina miaka 25 sikufichi Mhe. Mwenyekiti, mimi sina maji Kibweni nyumbani kwangu lakini sijifikirii mimi nafikiria mwenzangu ambaye yuko kijijini, mie *alhamdulillah*, yule maji hata ya kisima hana. Sasa lazima tuwe na muongozo, tuwe na jambo ambalo liende kwa wenzetu na huko ndio tulikotoka.

Kwa hivyo, Mhe. Mwenyekiti, ninachotaka kusema kwamba katika mazingira yote haya tuweze kufika pahala namna ya kusaidiana kuna suala la wanakijiji hawa upimaji wao wa ardhi au sehemu yao ya shamba, hati zao siku nyengine zinachelewa. Tuone namna gani kuweza kuwasaidia hizi sehemu zetu za vijijini kote katika mazingira katika sehemu zote hizi, tuone namna gani ya kuweza kuwabeba.
Mhe. Mwenyekiti, naona nifikie hapa kwa kusema kwamba kwa kweli haya yote yanayozungumzwa ni fedha, bila ya fedha hayatekelezeki na pesa ambayo serikali inayopata ndio itakayotumia.

Sasa Mhe. Mwenyekiti, nimalizie. Mimi nashukuru sana Baraza hili, na Baraza hili hata Mwenyezi Mungu akitujaalia tukimaliza kila mmoja ataweka historia, na historia itatuhukumu sisi kwa vizazi vijavyo, wajukuu na watoto kwamba kila Mwakilishi aliyekuwa amechangia ameisemea nchi yake basi itabakia na itabakia kwa miaka mia mbili, mia tatu na zaidi.

Sasa Mhe. Mwenyekiti, sote tuna uchungu na nchi, nataka nitoe taarifa kwa wenzangu kwa Wazanzibari, na kwa Waheshimiwa Wawakilishi wote kisiwa cha Fungu Mbaraka.

Mhe. Mwenyekiti, tulikuwa tumezungumza kwa hekima, kwa busara na ikatolewa tamko rasmi hapa ndani ya Baraza na serikali kwa jumla, kwamba kisiwa hichi cha Fungu Mbaraka ni kisiwa cha Zanzibar, hiyo si kauli yangu Mhe. Mwenyekiti, ni kauli ya Baraza la Wawakilishi na serikali kwa jumla na kitaendelea kuweko kwenye ardhi ya Zanzibar , na sote Mhe. Mwenyekiti, tukakipigia kelele kisiwa hichi cha Fungu Mbaraka.

Mhe. Mwenyekiti, napenda niseme kwamba baada ya Mwanasheria Mkuu lilipotoka tamko akakaa na Mwanasheria Mkuu mwenzake ikakubalika na ikaja hapa rasmi kwamba kisiwa cha Fungu Mbaraka ni cha Zanzibar, na Mhe. Mwenyekiti, kisiwa hichi hata Tanganyika haikuzaliwa kisiwa hichi kilikuwa Zanzibar ndio historia, na Mwanasheria Mkuu hapa ndiye aliyetueleza kwa miaka nenda rudi, sote hatujazaliwa.

Mhe. Mwenyekiti, nataka niseme hivi na leo ndio nathibitisha pumzi ninazo mimi za Mwenyezi Mungu basi, ndio ninazoringia, ninayemuogopa yule ninayemuendea sijda.

Mhe. Mwenyekiti, wenzetu juzi pale wameingia na meli zao wameingia *Petrogas* wamekuja na meli zao mbili, ndugu zetu Bara wameshakata huo ndio ukweli, wamekuja pale, wamevamia kisiwa, meli zao zimekuja. Na mimi naishukuru meli yetu ya KMKM, naipongeza sana Komadoo ikafanya kazi lakini kwa kweli kile kisiwa wameshakichota.

Sasa Mhe. Mwenyekiti, wakati tulipokuwa wastahamilivu tulisema serikali na serikali wafanye majadiliano. Sasa kama wanafanya majadiliano Mhe. Mwenyekiti, tumekaa humu watu wazima halafu zitoke meli zije tu pale, taarifa hii aah kwa sababu mimi namuomba Mhe. Waziri namstahi sana kama baba yangu, kwa kweli tunaringa na pumzi za Mungu aje atuhakikishie kwa jina la Mwenyezi Mungu, atwambie, na kwa kweli labda itakuwa jana imeondoka, na ushahidi upo hizo meli mbili za kufanya utafiti *Petrogas,* labda itakuwa jana imeondoka na walikuwa wakilindwa pale.

Sasa Mhe. Mwenyekiti, kuna vitu hivi hakuna mtu asiyeupenda umoja, na hivi vimekuja tu kwa sababu ya mafuta. Mhe. Mwenyekiti, nilipokuwa Dodoma kwenye Bunge la Katiba ambayo niliiunga mkono. Wenzangu pale wengine walikuwa Wajumbe wa Kamati Kuu, Mawaziri pale kwa bahati nzuri mimi nilikuwa kama nimekaa pembeni walisema aah! hawa Wazanzibari unajua sasa hivi kwa sababu tunaelekea kwenye uchaguzi tuwaitikie tu vitu hivi, *wallahi*, *billahi*, *tallahi*, tuwaitikie na ikimalizika uchaguzi tutavichukua tu. Lakini sasa tuwaachilie tu hao *wallahi*, *billahi*, kwa jina la Mungu yale ndio nathibitisha sasa.

Mhe. Mwenyekiti, hili halina vyama, si la CUF wala si CCM, hili linagusa umma na nchi, kwa sababu sisi ndio dhima. Komandoo Dkt. Salmin alikwenda akaweka bendera pale, na akazuia visiwa vyengine vya Pemba pale na kwa sababu tu ni chetu.

Sasa Mhe. Mwenyekiti, na tulikubaliana hapa kuna Wajumbe wengi hawakufika kule wa Baraza la Wawakilishi, na tulikubaliana twendeni. Sasa Mhe. Mwenyekiti, napenda nitoe tahadhari, naipenda nchi yangu naupenda Muungano wangu, lakini tu uwe Muungano wa kujadiliana, kuheshimiana na kuvumiliana.

Sasa katika vitu hivi Mhe. Mwenyekiti, na sijui labda meli itakuwa imeondoka jana au leo taarifa zipo, *satellite* zipo. Sasa tujue hapa kwamba mazungumzo yameshafanyika, Mwanasheria Mkuu keshatoa kauli yake, serikali ishatoa kauli yake, waziri muhusika mwenyewe keshatoa kauli yake.

Sasa kama vitu hivi inatoka hiyo mijina hata siijui kama natapika, *TPP* sijui wa Bara kule vijana tu watoto hawafahamu mambo ya nchi.

Haiwezekani Mhe. Mwenyekiti, kwa hivyo, naomba katika hili tukae tuone jinsi gani tunaweza kufaidika na kuendelea na udugu wetu na kuendelea na Utamaduni wetu wa kupendana na kuendelea na huu umoja wetu Mhe. Mwenyekiti.

Kwa hivyo, mimi namuomba sana Mhe. Waziri aje atuhakikishie, na kama hizi meli labda itakuwa ni suala la kunusa tumbaku basi atwambie tu hapakuwa na meli, hii tumbaku tu Raza amenusa, aje atwambie, lakini ninamuheshimu sana!

Mhe. Mwenyekiti, katika kumalizia mimi naitakia kheri sana wizara hii ambayo inakabili sana masuala ya maji, na kuna mwezi mtukufu wa Ramadhani basi wizara na sisi itwambie wafanyabiashara kama watahitajia kuna sehemu hamna maji wanahitaji mafuta, watwambie tunahitajia hapa mafuta lita mia mbili, tupo Mheshimiwa hizo ndio zakka zetu sisi Mhe. Mwenyekiti.

Mwezi wa Ramadhani wafanyabiashara wengi tunakuwa na zakka. Kwa hiyo, ni moja katika kuisaidia Taasisi ya Serikali, watwambie tu lita ngapi sehemu gani sisi tutawapelekea mafuta, sio pesa!

Sasa Mhe. Mwenyekiti, kwa jambo lolote sisi tuko tayari kushirikiana kama wafanyabiashara. Mimi nina ushawishi mkubwa kwa wafanyabiashara kwa kuweza kunisikiliza.

Mhe. Mwenyekiti, kwa niaba ya wananchi wa Uzini, na kwa niaba yangu mimi naitakia kila kheri wizara hii na nawatakia Mwenyezi Mungu awasaidie vijana wetu hawa kwa ustahamilivu wao, kwa udugu wao pamoja na wizara nzima na Serikali nzima ya Mapinduzi ya Zanzibar chini ya Serikali ya Umoja wa Kitaifa.

Naunga mkono kwa niaba ya wananchi wa Uzini kwa zaidi ya asilimia mia, lakini naomba tu Mhe. Mwenyekiti, kwa kumaliza waziri kama mwanawe mimi aje atwambie suala la kisiwa cha Fungu Mbaraka. Ahsanteni sana. (*Makofi*)

**Mhe. Mohammed Mbwana Hamad:** Mhe. Mwenyekiti, na mimi nakushukuru kunipa nafasi hii ya kuchangia.
Kwanza namshukuru Mwenyezi Mungu kutujaalia kuwepo jioni hii kwa madhumuni yale yale ya kusimamia serikali na kuwatetea wananchi wetu katika maslahi yao ya maisha yetu ya kila siku.

Pa nichukue nafasi hii kukushukuru na wewe kwa kunipa nafasi hii katika nyakati hizi za magharibi angalau na mimi kuchangia mawili matatu katika Hotuba ya Wizara ya Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati.

Aidha nimshukuru waziri na kumpongeza pamoja na watendakazi wake wote wa wizara kwa kazi kubwa muhimu na adhimu sana katika visiwa vyetu hivi vya Unguja na Pemba, kwa kufanya kazi ya kuwaboresha wananchi wa visiwa hivi katika shughuli za kimaendeleo ya maji pamoja na nishati.

Mhe. Mwenyekiti, kwa kweli wizara hii ni miongoni mwa wizara ambazo zimebeba majukumu makubwa na muhimu sana katika nchi. Kwa sababu bila ya ardhi kuiwekea mipango mizuri ya matumizi basi migogoro itakuwa haiishi na makaazi yatakuwa hayapo vizuri na vile vile kila siku tutakuwa tunatafautiana, lakini wizara kwa sababu ya majukumu yake ya kuiweka vizuri ardhi yetu kwa ajili ya makaazi ya watu wetu na wanyama wetu wanapaswa kufanya hivyo.

Pia maji ni miongoni mwa mambo muhimu na ni uhai. Kwa hivyo, imebeba wizara hii lakini vile vile na nishati kama ni miongoni mwa masuala muhimu katika maisha ya wanadamu.

Mhe. Mwenyekiti, mchango wangu niende katika ukurasa wa 12 haraka haraka katika Idara ya Mipango Miji na Vijiji.

Mhe. Mwenyekiti, kwa kweli niungane na Mhe. Abdi Mosi ambaye alizungumza kabla ya mchangiaji aliyechangia hivi punde.
Mhe. Abdi Mosi alizungumzia mipango miji iliyoanzishwa na Rais wa Kwanza wa Zanzibar Marehemu Abeid Amani Karume.

Mhe. Mwenyekiti, kwa kweli Rais huyu alionekana kwamba alikuwa na nia thabiti na ya dhati kuweka mipango miji katika Visiwa hivi vya Unguja na Pemba. Maeneo yote ambayo alianzisha ujenzi basi mpaka leo inaonekana kwamba maeneo yale yana utaratibu mzuri wa uwepo wa barabara, bustani na vyenginevyo. Lakini baadae mipango ile tumeiweka kando na hivi sasa tunajenga ndivyo sivyo, tunajenga kiholela, tunavamia maeneo na Serikali ipo.

Mhe. Mwenyekiti, tuna Idara ya Mipango Miji lakini mipango miji haiendelezwi bali mipango miji imo tu ndani ya karatasi. Mhe. Mwenyekiti, inasikitisha sana kuona kwamba maeneo mengi hivi sasa hata hakuna barabara za kuingia katika miji ambayo tunajenga, hiyo yote ni ukosefu wa kuiweka mipango miji vizuri na vijiji.

Mhe. Mwenyekiti, tuna miji mingi ambayo ipo katika *zone* hii ya Mjini Unguja, lakini kutokana na kuijenga kiholela inasikitisha sana kwamba mji wetu umekosa kuwa na sura ya kupendeza kutokana na kukosekana kwa kuujenga mji wetu vizuri.

Kwa hivyo nimuombe Mhe. Waziri tulipopita tumepita, twende tulipo na twendako. Tunapokusudia kuweka mipango miji katika miji yetu ambayo tunakusudia basi tuijenge katika utaratibu unaopendeza, wanapotokea wenzetu wakataka kutembea kwenye maeneo yale basi waone tu kwamba kwa kweli maeneo yale yanapendeza, ni mazuri, kunafikika kwa gari wakati wowote.

Mhe. Mwenyekiti, minghairi ya hivyo basi Mji wetu tutakuwa tunaujenga ovyo ovyo. Kifungu cha 34, naomba nikinukuu;

"Mhe. Spika, kwa muda mrefu sasa suala la ujenzi holela katika Mji wa Zanzibar limekuwa likipigiwa kelele, zipo sababu nyingi zinazopelekea ujenzi holela katika miji na vijiji, miongoni mwao ni ukosefu wa mipango ya matumizi bora ya ardhi na usimamizi mdogo wa shughuli zote za ujenzi ndani ya miji yetu".

Sasa Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Waziri akitwambia hivi, sisi tumuulize kwani anayetoa vibali vya ujenzi ni nani? Nani anayetoa ruhusa ya kujenga, tumetoa mamlaka kuanzia kwa Sheha, Naibu Sheha na wengine wanaofuatia, wao tumewapa fursa au Serikali imewapa fursa ya kukata ardhi kwa ajili ya kujenga. Lakini kumbe Serikali yenyewe haipendezewi na yale, lakini nani asimamie?

Kwa hivyo Mhe. Mwenyekiti, mimi ninamuomba Mhe. Waziri suala hili aliangalie kwa upana wake, na masuala haya ya ujenzi holela kwa kweli yamepitwa na wakati.

Sasa hivi ni lazima Mji wetu uwe ni wenye kupendeza na minghairi ya kuujenga vizuri basi tunakokwenda tutakuja kulaumiwa na watoto wetu, kwa sababu Mji utakuwa umejengeka kiholela, na tunazaa asubuhi na jioni, umma unaongezeka katika visiwa vyetu vya Unguja na Pemba, tunapaswa bila ya kuoneana haya Mji wetu kuujenga katika majengo ambayo yana mpango maalum.

Mhe. Mwenyekiti, nikiendelea na mchango wangu niende katika Idara ya Nyumba na Maendeleo ya Makaazi kwenye ukurasa wa 17.

Mhe. Mwenyekiti, Idara hii bila shaka ina nyumba nyingi za Serikali, nyumba ambazo ilikuwa Idara hii inapaswa kuziangalia kwa kina pamoja na kuzifanyia matengenezo kila inapostahiki kuzifanyia matengenezo siku hadi siku. La

kusikitisha ni kwamba kuna baadhi ya maeneo, kuna nyumba za Serikali kwa kweli hazifai kabisa, hizi nyumba hazina huduma ya aina yoyote, ingawa huku mbele tumeelezewa kwamba kuna maeneo yamefanyiwa matengenezo kama Michenzani.

Kuzibuliwa mabomba mbali mbali ambayo yalikuwa yameziba lakini nyumba zenyewe, pale Mkoani kuna eneo la Makadara kuna nyumba kwa kweli mabomba yameziba, nyumba zinavuja, watu wanapangishwa.

Mhe. Mwenyekiti, hili ni tatizo, nyumba zinapangishwa na Serikali, kwa nini nyumba hizi zisiweze kujitegemea wenyewe kwa kujitengeneza na zinapangishwa.

Kwa hivyo tunaiomba Idara ya Nyumba kwa kweli iwe makini katika kuzitengeneza nyumba, wakodishwe watu kwa bei stahiki, kwa bei za sasa lakini pia na hizo nyumba ziendane na wakati wa sasa.

Mhe. Mwenyekiti, kama nyumba hizi imeshindikana kutengenezwa na Serikali, basi vyenginevyo wale wakaazi waliokaa muda mrefu wauziwe ili waweze kuzitengeneza wao wenyewe.

Mhe. Mwenyekiti, kwa kweli inasikitisha sana kuona kwamba nyumba za Serikali hazikaliki zinavuja, huko vyooni mtihani. Hivyo niiombe Serikali, Idara ya Nyumba na Maendeleo ya Makaazi basi haya maendeleo ya makaazi yawe kwa ufanisi wa hali ya juu, tusiwe na Idara ya Nyumba lakini ndani ya karatasi tu, lakini mwelekeo pamoja na ufanisi wa nyumba hizi hautoshelezi.

Mhe. Mwenyekiti, kwa kweli inasikitisha sana kuona kwamba nyumba hizi miongoni mwao likiwa jumba lile pale Kengeja kila siku linapigiwa kelele, kila siku linapangwa kwamba tutatoa milioni mia moja na ngapi, milioni ngapi lakini jumba lile limeachwa mpake leo, jambo ambalo ni hatari kwa maisha ya watu wetu.

Mhe. Mwenyekiti, nikiendelea na mchango wangu niende katika Mamlaka ya Maji. Mhe. Mwenyekiti, Mamlaka ya Maji ni miongoni mwa Mamlaka ambayo ina jukumu kubwa la kusambaza maji katika miji na vijiji.

Niseme kwamba hii Mamlaka inafanya kazi zake vizuri, na *alhamdulillahi* maeneo mengi yanapata maji, changamoto zipo kuna maeneo bado hayajafika maji lakini naiomba Mamlaka iendelee kufanya kazi zake vizuri na *inshaallah* palipo na nia njema basi kila kitu kinakuwa kizuri. Nina imani kwamba changamoto zilizopo utafika wakati zinaweza zikatatuka.

Mhe. Mwenyekiti, lakini kuna tatizo ambalo limetokea katika Jimbo langu la Chambani kwenye Shehia yangu ya Chambani, pamechimbwa kisima pale, kuna sehemu inaitwa Kwapopo.
Kisima hichi ninafikiri kilichimbwa na wafadhili hawa Ras al Khaimah kama sikosei, lakini kisima hichi kilikuwa ni tegemeo kubwa sana la watu wa Chambani.

Kisima hichi kilikaa kwa muda mrefu kabla hakijatumika kwa wananchi, kilikuwa kinabubuja maji kama kwamba pameingizwa umeme pale, hakuna umeme lakini maji yalikuwa yanabubujika mpaka kulikuwa na mto fulani pale ulikuwa haukai maji kutokana na maji yale yanayotoka katika kisima.

Mhe. Mwenyekiti, lakini kwa masikitiko makubwa kisima hichi baada ya kuingiza kokoto au changarawe kwa jina jengine na kisima hichi kikafikishiwa umeme na kusambazwa maji kwa wananchi, karibu kipindi cha wiki mbili tatu kisima hichi kilikufa kabisa.

Mhe. Mwenyekiti, hii kwa kweli ilitupa mtikisiko mkubwa wa nafsi zetu watu wa Chambani, kwa sababu kisima hichi kilikuwa ni tegemeo. Inasemekana kuwa wachimbaji wa visima hivi, kile kilikuwa ni miongoni mwa kisima kilichokuwa bora katika visima vyote vilivyochimbwa zaidi ya visima arobaini, kilikuwa ni miongoni mwa visima bora. Sasa inasemekana hapa kwamba wataalamu walioshusha yale mabomba hawakuyashusha kwa umakini wakati zilipoingizwa kokoto ziliingia ndani ya kisima, na ile mashine au mchikichi uliokuwemo mule ukakosa kufanya kazi.

Mhe. Mwenyekiti, hili ni tatizo na niseme kwamba utaalamu uliotumika hapa ulikuwa ni mdogo, lakini hizi ni dhana za wananchi. Nimuulize Mhe. Waziri kwamba kisima kile sababu gani za msingi zilizofanya kisima kile kufa.

Jengine Mhe. Mwenyekiti, waliamua kuchimba kisima kando ya kisima hichi ambacho kimekufa, lakini kisima hichi kimechimbwa katika wakati mgumu sana kwa sababu ni wakati wa mvua za Masika. Sijui mafanikio yake yamefikia vipi, kwa sababu kisima hichi kilichimbwa wakati wa Masika ninafikiri ukichimba mita tano au sita tu maji yanakuwa mengi.

Kwa hivyo nimuulize Mhe. Waziri kisima kilichokufa kile ambacho kilikuwa na maji endelevu, kitafanyiwa utaratibu gani ili kukiendeleza, lakini kisima hichi kipya ambacho kimechimbwa katika kipindi hichi cha mvua nyingi sijui kitakuwa na matumaini gani ya wananchi kutokana na suala hili.

Mhe. Mwenyekiti, vile vile ningemuuliza Mhe. Waziri pamoja na kupatikana kwa kisima hichi kipya ambacho bado hakisambazi maji yake, kuna utaratibu gani wa

kujenga tangi la kuhifadhia maji kwenye Mji huu wa Chambani ambao una wakaazi wengi na mwendo wa umeme, yaani kuendesha umeme masaa yote gharama inakuwa kubwa zaidi kuliko kuyakusanya maji katika tanki moja.

Mhe. Mwenyekiti, nikiendelea na mchango wangu niende katika kisima kilichochimbwa katika Shehia ya Ukutini. Mhe. Mwenyekiti, pale pamechimbwa kisima lakini kisima kile mpaka leo bado maji yake hayajasambazwa. Ni lini kisima hichi kitasambaziwa maji ili wananchi hawa na wao wapate maji ambayo yanakuwa salama.

Kipo kisima cha zamani ambacho kinapatisha maji katika mji ule wa Ukutini lakini maji yake si safi na muda mrefu hayajasafishwa. Kwa hivyo ni lini kisima hichi cha watu wa Shehia ya Ukutini kitapata kusambazwa maji katika mji wa Ukutini.

Mhe. Mwenyekiti, nikiendelea na mchango wangu niende kwenye ukurasa wa 36 kuhusiana na masuala ya umeme.

Mhe. Mwenyekiti, nishati ya umeme ni nishati muhimu. Ninapongeza Serikali kwamba watu wa Jimbo la Chambani, katika Shehia ya Chambani na Shehia nyengine zimepatiwa umeme, lakini umeme wa Shehia ya Chambani ulikuwa ni usambazaji wa umeme vijijini. (*Makofi*).

Mhe. Mwenyekiti, lakini kwa masikitiko makubwa kuna vijiji kadhaa vya Chambani havikufika umeme. Sasa mara nyingi huwa tunapiga kelele kwamba vijiji hivi vifikishwe umeme, kwa sababu ni aibu kwamba kuna vijiji vipo katikati vimezungukwa na vijiji vyengine ambavyo vina umeme, lakini vijiji vyengine vimekosa umeme. Kwa mfano, kuna Kijiji tunakiita Wani, Shangini, Dongoni, Mafuweni, vijiji hivi vyote vipo katikati ya Mji wa Chambani, vimezungukwa na vijiji vyenye umeme lakini vijiji hivi bado haujafika umeme.

Mhe. Mwenyekiti, kwa kuwa umeme umeshafika katika eneo hili, nimuombe Mhe. Waziri kwa makusudi vijiji hivi vimo ndani ya mji uliofika umeme watusambazie umeme ili wananchi na wao wapate angalau matumizi ya nishati hii ya umeme.

Mhe. Mwenyekiti, mimi kwa mchango wangu huu, nimuombe Mhe. Waziri ayafuatilie yale yote ambayo nilimuomba kuyafuatilia, na niunge mkono hoja ya kitabu hichi kwa asilimia mia moja.

Mhe. Mwenyekiti, ahsante sana. (*Makofi*).

**Mhe. Mwenyekiti:** Ahsante sana Mhe. Mohammed Mbwana kwa mchango wako. Sasa nafasi tunampa Mhe. Hamza Hassan Juma.

**Mhe. Hamza Hassan Juma:** Mhe. Mwenyekiti, na mimi ninakushukuru kunipa nafasi hii nikaweza kutia tia nyalio ili Mhe. Waziri bajeti yake hii tuweze kumpitishia, aweze kwenda kutufanyia kazi kuwahudumia wananchi wetu.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nataka nianze na mambo mawili kwanza ili nimuachie Mhe. Waziri akayafanyie kazi, halafu baadae nije na maoni na ushauri wangu kwenye Kamati au kwenye hotuba ya Mhe. Waziri.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nina kadhia mbili ambazo ni za wananchi, nitaomba tu nimkabidhi Mhe. Waziri ili *hansard* iweke sawa, nilikuwa tu nataka aje anipe ufafanuzi.

Mhe. Mwenyekiti, kuna hawa wananchi ambao mimi Kamati yangu ililisimamia sana suala hili, hawa vijana wetu waliokuwepo Maruhubi pale waanikaji madagaa. Eneo lile kwa kweli Mhe. Mwenyekiti, limetoa ajira nyingi sana kwa vijana. Kwa bahati ajira hii ya uanikaji wa madagaa, sasa hivi imekuwa ni sekta ambayo Serikali inatakiwa iwe karibu nayo sana, kwa sababu ni sekta ambayo inatoa maslahi makubwa sana kwa wananchi wetu.

Sasa tukisema tunawaondoa lakini tunashindwa kuwapatia pahala pa uhakika ambapo hapana matatizo, yaani pa kudumu. Kwa kweli wananchi wale tutawavunja moyo, na kwa sababu idadi ya viti vyetu maofisini; yaani Serikalini vimeshajaa, sasa na wao kwenda serikalini kutafuta ajira, kwa kweli itakuwa ni mtihani.

Sasa mimi kwanza ninashukuru sana; ninamshukuru sana Katibu Mkuu pamoja na Mkurugenzi wa Ardhi kwamba ule ushauri wa Kamati kwa kweli waliutekeleza, lakini katika utekelezaji wake kidogo kumejitokeza changamoto ndiyo hii ambayo nataka Mhe. Waziri aifanyie kazi.

Vijana wale tulipopata taarifa kwamba Serikali lile eneo linataka kufanywa shughuli ya maendeleo, yaani ujenzi wa bandari ya kisasa kabisa ambayo itabadilisha hata uchumi wa Zanzibar.

Sisi kimsingi tuliridhika lakini wale vijana na siyo vijana tu, kwa sababu mpaka watu wazima ambao wengine mimi wananizaa wapo pale ambao wanafanya shughuli zao za kutafuta maisha.

Sasa kwa taarifa niliyoipata vijana hawa wamepatiwa eneo katika eneo la Mangapwani, lakini hilo eneo ambalo walilopatiwa kuna mwananchi amekuja na

waraka wake ambao huku nyuma nilivyoangalia kuna saini ya Muasisi wetu Mzee Karume. Kwa hivyo huu waraka inaonekana ni waraka halali.

Sasa mimi nitaomba tu Mhe. Mwenyekiti, kwa Mhe. Waziri, basi nikishamaliza kukaa kitako hapa nimkabidhi waraka huu ili wajaribu kuangalia hilo eneo ambalo vijana wetu au wananchi wetu wanaotaka kuwekwa kwa ajili ya kutafutia rizki lionekane uhalali lakini vile vile lisilete athari kwa watu wengine.

Sasa hili nilisema nianze nalo kwa sababu ninahitaji Mhe. Waziri alifanyie kazi, kwa sababu naweza nikaja nikazuia programu fulani hapa kwa ajili ya kupata maelezo ya kutosha. Kwa hivyo sitaki hasa nilikuwa sikusudii hasa kuzuia kifungu katika bajeti hii, kwa sababu Mhe. Waziri kwa kweli hii Wizara ameimudu sana. Kabla ya kuingia yeye hii Wizara Mhe. Mwenyekiti, kila mtu alikuwa anasubiri Wizara ya Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati lakini sasa hivi hakuna hata mtu mmoja anayepoteza muda wake kusikiliza Wizara ya Ardhi kuna nini, kwa sababu mambo yote Mhe. Waziri ameweka sawa na tumeridhika sana. Sasa hili tu kidogo nilikuwa nataka baadae alifanyie kazi.

Jengine Mhe. Mwenyekiti, nilikuwa na *document* nyengine hapa ambayo pia nitamuomba Mhe. Waziri baadae na timu yake aifanyie kazi.

Nina maamuzi ya Mahakama hapa lakini kwa bahati mbaya haya maamuzi ya Mahakama haya, sijui labda tubadilishe sheria maana yake yameandikwa kwa lugha ya kigeni na mimi ni mwenyeji. Lakini nitajaribu kumpa hii *document* ambayo ni *Civil Appeal No.37* ya *2012 from original case number* hiyo hapo, *original Court at Vuga*. Hii naizungumza hapa kwa sababu maamuzi tayari yalikwishakutoka. Kesi hii inahusu *appelant* kuna Muungano *Cooperative* Zanzibar na mwengine ni Suleiman Neyyan vs Ushirika wa Urafiki Mwema, na wa pili Mkurugenzi wa Idara ya Nyumba na Maendeleo. Hawa ndio *respondents*.

Sasa inasema; *date of last order* ilikuwa tarehe 7 Novemba, 2012 na *date of judgement* ilikuwa ni tarehe 13 Februari, 2013. Sasa hii *judgement* ni ndefu, kwa sababu ina kurasa karibu 4, kwa hivyo nikiamua kuisoma hapa Mhe. Mwenyekiti, nitachukua muda wako mwingi, na nitashindwa kupata nafasi ya kushauri katika taasisi zake nyengine Mhe. Waziri.

Sasa haya nilikuwa naomba ayafanyie kazi, kwa sababu hapa kuna maamuzi ya Mahakama, kuna wananchi hawa ambao walilalamika dhidi ya Ushirika wa Urafiki Mwema na Mkurugenzi wa Idara ya Nyumba, na Mahakama ilitoa amri kwamba warejeshewe hawa eneo lao, na kwa sababu vile vile lina historia kubwa nyuma, lakini mpaka leo bado hawajarejeshewa.

Kwa hivyo, mimi naamini kwamba Mhe. Waziri ni mtu ambaye ni mtulivu sana, ni mtu ambaye anafanya maamuzi yake kwa uhakika, na kama ni maamuzi ya Mahakama yameshapita, basi naamini Mhe. Waziri hatoweza kupingana na maamuzi ya Mahakama. Sasa haya Mhe. Mwenyekiti, nilisema niyaanzie, kwa haya ambayo nitayahitaji Mhe. Waziri akayafanyie kazi, halafu baadaye nitakuja katika mchango wangu binafsi.

Mhe. Mwenyekiti, nataka nianze na Mamlaka ya Maji. Mhe. Mwenyekiti, mimi nataka nimpongeze sana Mhe. Waziri, pamoja na watendaji wake hawa wa Mamlaka ya Maji. Kimsingi huko nyuma tuliwasema sana, na tuliwasema sio kwamba tulikuwa tunawachukia, hapana. Tuliwasema sana kwa sababu kwa kweli huduma ya maji ilikuwa hairidhishi. Lakini tunashukuru sasa hivi *alhamdulillah* maji yanaendelea kupatikana, ingawa kuna baadhi ya maeneo yanakuwa na matatizo kidogo kidogo, lakini matatizo yakiisha kabisa basi Mamlaka ya Maji watakuwa hawana kazi. Kwa hivyo, matatizo ni sehemu ya kazi zao. Kwa hivyo, tunaomba waendelee na jitihada zao hizo.

Mhe. Mwenyekiti, hapa kidogo wananchi wangu wa Jimbo la Kwamtipura hapa roho zao kidogo ziko shingo upande, kwa sababu sisi bomba la maji lile kubwa linalotoka Welezo, linapita katikati ya Jimbo la Kwamtipura. Lakini bahati mbaya bado sisi hatupati maji kama vile inavyostahiki.

Mhe. Mwenyekiti, kutokana na kilio chetu kusikiwa na serikali, tunashukuru kwamba tumepata fedha za mfuko wa jimbo na tumeweza kuchimba visima vingi tu ndani ya jimbo letu.

Mhe. Mwenyekiti, tunamshukuru Mwenyezi Mungu sasa hivi visima hivi vinatoka maji na wananchi wetu wanaweka zamu, angalau kuweza kupata huduma ya maji. Kwa nini nikasema wananchi wa Kwamtipura wanaweka shingo upande.

Mhe. Waziri alizungumza hapa kwamba, nafikiri ilipokuwa bajeti kuu ya serikali kwamba serikali itabeba dhima ya kulipia umeme katika visima vya maji, vile ambavyo ni vya ZAWA. Lakini sasa sisi visima vyetu sio vya ZAWA, visima vyetu sisi ni vya WAZAWA. Maana yake kuna ZAWA na WAZAWA. Sasa sisi wenye majimbo ni WAZAWA, tumechimba visima ambavyo moja kwa moja vinawahudumia wananchi wetu, lakini bado tunaendelea kulipia umeme.

Kwa hivyo, ina maana ile *offer* wanapewa wale ambao hawakuchimba visima, sisi tuliochimba visima *offer* ile hatujaipata. Sasa naomba huruma hiyo kwa wananchi wangu wa Kwamtipura. Kazi kubwa kwa kweli wanafanya, mpaka saa 8:00 za usiku wanaamka wanawafungulia maji watu kwa zamu. Kwa hivyo, ina maana hata ule ugomvi wa maji sasa hivi Kwamtipura kwa kiasi fulani umepungua.

Jengine nilikuwa naomba Mhe. Mwenyekiti, kwa kupitia kwako Mamlaka ya Maji, naomba walikague lile bomba lililotoka Welezo, lile la asili sijui kama ni la saruji au sijui la chuma. Lakini kama sikosei nafikiri ni la saruji, lakini saruji ile ya zamani ya kikoloni.

Lile bomba sasa hivi kuna baadhi ya sehemu nyingi zimeanza kufanya *leakage*, na sijui kama *spare* ya mabomba yale yanapatikana katika hivyo viwanda vilivyotengeneza yale mabomba. Sasa nilikuwa naomba yafanyiwe ukaguzi, kwa sababu kuna baadhi ya maeneo yale kwa kupitia Mboriborini, Shauri Moyo huku, kuna baadhi ya sehemu zinakuwa na *leakage,* kwa hivyo maji mengi yanapotea.

Pia nataka nimuulize Mhe. Waziri, sijui kama mfano itakuja kutokezea, ile aliyoizungumza rafiki yangu hapa, swahibu wangu Mhe Raza, ikija ikitokezea gharika yoyote lile bomba tuseme likipasuka kabisa, njia gani mbadala itaweza kufanywa.

Halafu ile *last time* yale mabomba sijui ipo katika *record* kwamba mabomba yale yametakiwa yakae pale ardhini kwa muda wa miaka mingapi. Lakini kwa nini nikasema yafanyiwe ukaguzi.

Kwa sababu tunaona sasa kuna ujenzi mkubwa, maana yake ule ujenzi wa zamani katika vile vijumba vyetu vile vya Kwamtipura, angalau unaweza ukaja kidogo ukasema bomba limepasuka vunja ukuta huu. Lakini sasa hivi kumeanza kujengwa majengo ya kisasa ya ghorofa, katika *line* ya bomba kubwa ya maji.

Kwa hapa hebu Mhe. Waziri naomba, na nafikiri hii bajeti itapita Jumatatu, kwa hivyo naamini kesho Jumamosi na Jumapili wataweza kwenda kufanya *survey* wakaliangalia hasa lile bomba limepita wapi na wapi, na ujenzi unaoendelea sasa hivi, kama hautoweza kuja kuathiri miundombinu yetu hii ya maji kwa upande wa Zanzibar.

Lakini kikubwa zaidi nilikuwa nataka niwapongeze, kwa sababu nilikuwa nawasikiliza baadhi ya Waheshimiwa Wajumbe wenzangu wa majimbo ya vijijini, walivyokuwa wanaishukuru serikali kwa kupitia Mamlaka ya Maji namna wanavyopata maji. Kwa hivyo, sasa hivi tunashukuru mpaka vijijini sasa hivi *alhamdulillah* wananchi wetu wanakunywa maji ya bomba, au ya mfereji. Maana yake wenzetu wanaita bomba, lakini sisi tunaita maji ya mfereji.

Mhe. Mwenyekiti jengine ambalo nilikuwa nataka nilizungumzie ni suala la Shirika la Nyumba. Mhe. Mwenyekiti, moja katika kumuenzi Mzee Karume ni hili Shirika la Nyumba ufanyaji wake wa kazi. Mwenzangu Mhe. Mjumbe wa Matemwe hapa amezungumza, kwamba Mzee Karume alianza *land use plan*, na

alijenga majengo katika maeneo mbali mbali majengo makubwa, lakini vile vile na yale majengo ya chini katika maeneo mbali mbali, sina haja ya kuyataja kwa sababu nyumba za maendeleo mule zilimo tunaziona.

Sasa tumepitisha sheria ya Shirika la Nyumba, na kwa kuwa tumepitisha sheria ya Shirika la Nyumba, tunamuomba sana Mhe. Waziri, amshauri vizuri sana Mhe. Rais, asifanye papara, asifanye haraka, atafute ili tupate mtu *competent* hapa ambaye ataweza kuja kuibadilisha sura ya Zanzibar. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, masuala ya nyumba. Tumeshatembea sana sisi tunamshukuru sana Mhe. Spika, wetu, ametusafirisha sana. Leo ukienda China kila *province*, kila mji unajitegemea kwa majengo yake yenyewe, ile inatokana na yale Mashirika ya Nyumba katika mamlaka zile yanafanya kazi vizuri. Miradi hii ya *Real Estate* Mhe. Mwenyekiti.

Leo tunaanza kupiga kelele, aah! Zanzibar watu wengi. Hapa bado watu hawajaja. Mhe. Mwenyekiti, hapa watu watakuja. Kwa sababu hii nchi tunategemea sio muda mrefu itakuwa na uchumi mkubwa wa kutosha, rasilimali ambazo tutakazokuwa nazo zitawavutia wawekezaji, zitawavutia ma- *investors* wakubwa, ambao hao wakija basi lazima idadi ya watu wataongezeka. Kwa sababu watu watakuja kufanya kazi, pataanzishwa viwanda vingi sana hapa Zanzibar kwa uchumi ambao tunautegemea hapo baadaye.

Kwa hivyo, hivi sasa Zanzibar hatujawa na viwanda vikubwa ambavyo vinachukua wafanyakazi wengi. Leo tunajenga mpaka kwenye mabonde ya mpunga. Je, hapo Zanzibar itakapofunguka kiuchumi hao watu watakuja kukaa wapi, tutakuja kushindwa na hata pa kulima. Lakini mkombozi wa suala hili ni Shirika la Nyumba la Zanzibar.

Mhe. Mwenyekiti, tumeona wenzetu, mfano mdogo tu Tanzania Bara. Tanzania Bara Mhe. Rais kuna baadhi ya taasisi alipoona anataka kuziboresha, basi aliwachungulia wataalamu wake wa ndani, lakini vile vile akaona hebu nijaribu ku-*import*, akawachukua wataalamu wa Kitanzania, lakini waliofanya kazi nje ya Tanzania. Kwa kweli tumeanza kuona maboresho makubwa kabisa. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, kuhusu *TRA* kuna Rished Bade pale. Baada ya kuitwa yule na kuingia pale, mapato yameongezeka sana, ni kwa sababu gani. Amechukua utaalamu kutoka nje ameuleta ndani, umeweza ku- *boost* mapato ya uchumi wa nchi yetu.

Vile vile Mhe. Mwenyekiti, kuna hii *project* mpya kule wanaita *Big Results Now*, ambayo kuna ndugu Omar pale. Yaani ule mradi sasa hivi ukiangalia kuna

programu nyingi, zile za skuli za sekondari, sijui kuna miradi gani mingi sasa hivi imeanza kuonekana ile *impact* yake. Lakini Mhe. Mwenyekiti, hata ile *Treasury Registrar* kule Dar es Salaam. Vile vile kuna ndugu yetu Mahfoudh, kazi kubwa sana ameweza kuifanya.

Kwa hivyo, tusilazimishe lazima sisi. Tunao wenzetu hawa ambao ni Wazanzibari na Watanzania ambao wanaofanya kazi nje ya nchi. Wameshafanya kazi katika Mashirika ya Kimataifa, katika makampuni makubwa duniani. Kwa hivyo, ndio maana tukasema Mhe. Rais asifanye haraka, Mhe. Waziri akae aumize kichwa, akae na Mhe. Rais washauriane vizuri.

Mhe. Mwenyekiti, tena sasa hivi kwa bahati nzuri wenzetu kwa kupitia Ofisi ya Rais Ikulu pale, ile Idara ya Diaspora. Sasa hivi tayari wameanza kutayarisha *database* ya Wanzanzibari wataalamu waliokuwepo nchi za nje ambao wanaweza kuja kusaidia maendeleo ya nchi yetu. Lakini hata hapa Zanzibar *SUZA* pale, tunaye Profesa Idrissa Ahmada Rai tumemuona, baada ya kuja yeye pale basi ameweza kubadilisha sasa hivi taaluma, kwa kweli Zanzibar sasa hivi inaanza kuonekana katika mradi huu.

Mhe. Mwenyekiti, kwa bahati tulipokuwa tunapitisha ile sheria ya *PPP*, tulimshauri sana Mhe. Dkt. Mwinyihaji, Waziri wa Nchi, Mipango, ambapo ile sheria ya *PPP* iko kwake.

Tulimshauri tukamwambia katika hiki kipengele cha huyu Mkurugenzi au Kamishna, Rais apewe mamlaka ya kufanya maamuzi ambayo anahisi yanatosha. Yaani yule Mkurugenzi wa *PPP* asilazimishwe, kwa sababu katika ile sheria kulikuwa kuna kipengele kinasema lazima awe *Senior Public Officer*. *Senior Public Officerl* ni lazima mtu awe amefanyakazi ndani ya serikali kwa muda mrefu. Lakini je, kama tuna mtu ambaye yuko makini, na Wazanzibari wapo wengi tu ambao tunawajua wana uwezo mkubwa sana nje ya nchi.

Sasa kwa bahati ile sheria ilipopitishwa mimi nilikuwa safarini kidogo, lakini sijui kama iliangaliwa vizuri. Mwanasheria Mkuu anapiga kofi pale anaonesha alizingatia hili. Kwa hivyo, tulikuwa tunalenga maeneo kama haya, kwamba lazima tuangalie hapa tukimweka huyu, je, ataweza kubadilisha vipi taasisi yetu. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, sasa hivi ukiangalia China pamoja na wingi wao basi ni Bara la Afrika mara moja na nusu, wako karibu bilioni 1,400,000,000. Sisi tuko karibu milioni 800 tu Afrika sasa hivi. Lakini sasa hivi ukienda pale utaukuta ule mji wao jinsi walivyoujenga, ile *land use plan* walivyoiweka. Wanavunja nyumba hizi za chini chafu chafu, wanawapelekea mji wanawaambia hapa tunataka kuondoa

nyumba zenu tunataka kujenga mji kama huu. Wanajengewa majumba ya ghorofa marefu sana. Mtu kama amevunjiwa nyumba moja anapewa nyumba mbili, tena wala huna haja ya kumlipa fidia, kwa sababu umechukua ardhi yake.

Kwa hivyo, mimi naomba hili Shirika la Nyumba waanze kuangalia utaratibu, wataanza kujenga mji kutoka katika maeneo gani. Tuliwahi kupendekeza, waliwahi kuja makampuni kuna kipindi. Kuna kampuni moja walitaka kufungua eneo lote la Makadara lile wajenge majengo yale sisi wa Kwamtipura wote tungenyonywa kule Makadara. Yaani hii Wilaya ya Magharibi mpya hii sijui Magharibi A au B wala zisingekuwepo, kwa sababu watu wote wangekuwa wameshakusanywa katika mji wamewekewa soko, wamewekewa *super market* na kila kitu, hayo ndio mambo ya kileo yanavyokwenda.

Sasa katika kujiandaa na uchumi mpya Zanzibar, Shirika la Nyumba lazima linatakiwa lije lifanye kazi ya kutosha, ambayo itaweza kuja kusaidia kuboresha mji wetu.

Mhe. Spika, aah! Mhe. Mwenyekiti. Itikia Amina. Kuna mifano mingi na mimi Mhe. Mwenyekiti, nilikushauri nilipokuwa nachangia kwenye bajeti kuu ya serikali. Nilikushauri Mhe. Mwenyekiti, hizi kamati za Baraza tusifanye kazi Unguja na Pemba tu, Dar es Salaam na Tanzania Bara, hebu tutokeni nje! *(Makofi)* Mhe. Mwenyekiti, sasa hivi na ninaomba bado muda upo, kamati yako ingeondoka na huyu Mkurugenzi aliyekuwepo sasa hivi, mngelikwenda Ethiopia. Mhe. Waziri hebu angalia kwenye kapu yako hiki kilichobakia, waende kamati hii Ethiopia wakaangalie.

Mhe. Mwenyekiti, Ethiopia zamani ikitajwa ulikuwa unafikiria mifupa, watu wamekonda. Ethiopia ya sasa hivi ni tofauti.

Ethiopia sasa hivi inajengwa na inabadilika sana. Wale wenzetu Shirika la Nyumba pale Ethiopia kitu walichokifanya ni kwamba wafanyakazi wameandaliwa utaratibu maalum wa kupatiwa makaazi, serikali inatafuta *fund* ina- *compensate* pale.

Kwa hivyo, mwananchi analipa *fee* ambayo ni ndogo sana, lakini vile vile anakuwa ni mtiifu ndani ya serikali. Kwa hivyo, lazima Mamlaka ya Nyumba au Shirika la Nyumba liangalie serikalini, lakini vile vile katika mifuko mingine kuchangia ili kuweza kujenga hizi nyumba za kisasa.

Mhe. Mwenyekiti, najua nachukua muda wako, lakini kwa kuwa tunaishauri serikali, na unajua sasa hivi mpango wetu tunakwenda na *PBB. PBB* kuna vitu

vyengine vilikuwa havimo, lakini Shirika likiundwa wanaweza wakapanga mipango yao kama hiyo niliyoweza kuishauri.

Mhe. Mwenyekiti, nilikuwa nataka kuja katika Shirika la Umeme, kama nilivyosema mwanzo. Mhe. Waziri mwanzo mlikuwa hamtuelewi, tulilisema sana Shirika la Umeme. Lakini kwa kuwa Mhe. Waziri wewe ni msikivu, ulikuwa unachukua maoni yetu unayafanyia kazi, kwa kweli tunashukuru sana. Huduma za umeme sasa hivi zimeendelea kuboreka siku hadi siku. Lakini kama walivyosema wenzangu Shirika la Umeme unalipa mzigo mkubwa.

Mhe. Mwenyekiti, sasa hivi *TANESCO* wanatudai pesa nyingi sana. Leo kuna Mjumbe mwenzangu hapa Mhe. Abdalla Mohamed amesema, kila siku tunakuja na mipango mipya. Tuna programu sijui umeme wa upepo, sijui umeme wa jua, umeme wa *biogas*, umeme wa taka, umeme wa Mhe. Makame Mshimba sijui yuko wapi. Lakini Mhe. Mwenyekiti, sisi Wazanzibari ni watu wa kushangaza sana, tunapiga kelele wakati kitu tunacho.

Mwalimu Nyerere alitutolea mfano, alisema Watanzania uchumi tunao lakini tumeukalia. Sasa watu wakashtuka, wakasema aah! Mwalimu Nyerere siku hizi unaanza kubadilika, unasema uchumi tunao lakini tumeukalia, wakaambiwa hivyo sivyo, tuna rasilimali tunashindwa kuzitumia na leo imeanza kujidhihirisha.

Mhe. Mwenyekiti, tunapiga kelele *research,* kila *research* inafanywa kwa ajili ya kutafuta umeme mbadala. Umeme mbadala Mhe. Mwenyekiti, ipo njia rahisi tena ya mkato tutafika mara moja, umeme wa gesi.

Leo huko Tanzania Bara kwa kupitia *TANESCO* tunakonunua umeme. Kila siku *bill* ya umeme ilikuwa inaongezeka kwa sababu walikuwa wanatumia nini ile *hydro electric power*, ule umeme ambao unatumia maji, lakini leo Mhe. Mwenyekiti, ukiangalia mvua zenyewe ndio hivyo, zinaweza zikaja kidogo na zinaweza zikaja nyingi sana.

Kwa hivyo, wenzetu sasa hivi wameanza kutumia umeme wa gesi. Mhe. Mwenyekiti, umeme wa gesi ndio umeme wenye gharama ndogo sana. Sasa Zanzibar tukiweza kuchimba gesi ina maana ni *source* ya uzalishaji wa umeme, kwa hivyo ina maana tutakatisha kununua umeme kutoka *TANESCO*, umeme utapatikana hapa hapa Zanzibar, sasa tuna tatizo gani. Mhe. Raza rafiki yangu sasa hivi amezungumza, amesema Fungu Mbaraka kuna meli tumeiona kama hatukuwa makini tutaziona nyingi, kama hatukuwa makini meli tutaziona nyingi, watavuna sisi tunatumbua macho!

Mhe. Mwenyekiti, leo Maalim Rama Mhe. Waziri hata *TPDC* ameshasaini mkataba eneo lile siku nyingi tu, na kwa sababu suala la mafuta na gesi mpaka sasa hivi ni suala la Muungano, tukitaka tusitake Katiba ndio inavyosema, sasa ndio yale niliyosema Mwalimu Nyerere alisema Watanzania uchumi tunao lakini tumeukalia, sasa tuinuke ili uchumi uje juu isiwe sisi tuko juu uchumi tumeukalia. Kwa hivyo nawashauri na nawashawishi wenzangu *the only solution* iliyobakia ni kubadilisha Katiba, na sasa hivi *draft* imeshapangwa Katiba Mpya tuipigie kura Katiba inayopendekezwa ili sasa Mhe. Waziri akachimbe yeye hiyo gesi.

Leo kuna watu wanasema aa maana yake hiyo gesi Zanzibar sijui haipo, nani alikwambieni, Zanzibar gesi ipo, tena ya kutosha! Kuna *research* chungu nzima zimeshafanywa, wengine wanasema aa maana yake hiyo gesi ya miaka minane, kakwambieni nani. Hapa hapa mimi niliwahi kuzungumza siku moja nikatoa *document*, niliitoa kwenye mtandao Waziri Mkuu Pinda yuko wapi Korea, amekwenda kukagua meli ya kufanya utafiti wa mafuta na gesi, meli ya kampuni ya Brazil, haikuchukua hata miaka mitatu ngoma ile pale sasa hivi Mtwara.

Mhe. Mwenyekiti, Mtwara katika eneo lililokuwa mkoa masikini katika Tanzania Mtwara ilikuwa moja, leo nenda Mtwara kiwanja hukipati, kile kiwanja kile ukitaka *square metre* sijui ngapi hukipati baada ya kupatikana gesi.

Mheshimiwa Mwenyekiti ili tumpe nguvu Mhe. Waziri lile alilolizungumza Mhe. Raza katika suala la utafiti unaotaka kufanywa katika eneo la Fungu Mbaraka tumpe nguvu sasa Mhe. Waziri, awe na mamlaka ile gesi sasa baada ya kuja meli tukaanza kufukuzana nazo tupeleke meli yetu sisi tukachimbe. Na yapo makampuni mengi tu Mhe. Waziri ukitaka kesho nitakuletea Mhe. Mshimba anayo lakini mimi ninayo mengi kuliko Mhe. Mshimba.

Mhe. Mwenyekiti yapo makampuni ambayo yako tayari kuja kuchimba rasilimali ya gesi, na SMZ Mhe. Waziri hutoi hata shilingi moja shughuli yote itafanywa na wewe mwenyewe unajua, na yeye mwenyewe Mhe. Waziri anajua, lakini atafanya nini, tumpe zana tu.

Mhe. Mwenyekiti, umeme tunaouziwa sisi tulifanyiwa semina hapa na watu wa Shirika la Umeme hapa ukumbi wa juu sote hapa, umeme sisi bei tunayouziwa Shirika linakula hasara hauwezi kujiendesha, kwamba deni lililokuweko kule walipe na *running costs* za Shirika la Umeme haziendi Pemba kule. Sijui huo umeme uliopelekwa Pemba kama angalau wananchi wameshafikia kiwango kile cha kuutumia na kuweza kulipa, labda Mhe. Waziri uje utupe takwimu umeme tulioupeleka Pemba *running costs* za Pemba na wananchi wanavyolipa, je, ule umeme unalipa au Serikali inafidia.

Sasa Mhe. Mwenyekiti haya yote yanaweza yakarekebishika tukianza kuchimba rasilimali yetu ya gesi sisi wenyewe. Umeme utakuwa bei ya chini, uwekezaji utaongezeka na uchumi wa nchi utakua.

Leo pato letu bajeti tunayopitisha sasa hivi karibu bilioni mia nane na kumi na ngapi sijui, leo tukichimba gesi ina maana yale ni mapato *extra* ambayo yalikuwa hayamo katika bajeti yetu. Sasa tusimgonganishe kichwa Mhe. Waziri kwenda kutafuta meli ya kufukuzana nayo, tumpe nyenzo, tumpe uhuru, tumpe nafasi na sisi ndio wenye kazi, ndio watu wa kuweza kufanya kazi hiyo.

Mhe. Mwenyekiti, najua unaniangalia sana lakini nataka nijaribu kumalizia malizia nakuja Mahakama ya Ardhi, ingawa sasa hivi kidogo malalamiko mengi katika masuala ya ardhi tunavyohisi yamepungua, kwa sababu zamani kila ukikaa unapigiwa simu unaletewa *document*, lakini siku hizi mambo yamekuwa shwari.

Mahakama za Ardhi nimetaarifiwa kwamba zinashushwa mpaka katika Wilaya lakini bado hawa Mahakimu kuna upungufu mkubwa pamoja na nyenzo za kufanyia kazi. Sasa naomba sana Mheshimiwa Mwenyekiti aangalie sana, kwa sababu unajua ardhi hizi kama zikikaa muda mrefu hazijafanyiwa maamuzi kuna wengine watakuwa wanafaidika, kwa sababu mtu ameikalia ardhi ya watu, lakini kuna wengine wanakuwa wanaumia kwa sababu ardhi yake ndio rasilimali yake mtu anashindwa kuitumia. Na wakati mwengine kuna watu wana uwezo wao na mapesa yao wanakalia ardhi za wanyonge. Ssasa kama hizi Mahakama za Ardhi zinachukua muda mrefu kufika kutoa maamuzi, wale wanyonge wanazidi kuendelea kuwa wanyonge.

Mhe. Mwenyekiti, la kumalizia kabisa kabisa juzi tulipata taarifa kwamba yale yale majenereta mnataka kuyauza, sasa hebu twambieni mnataka kuyauza kwa utaratibu gani? Kwa mnada, kwa *tender* au vipi.

Vile vile kuna ukuta ambao mnaujenga sasa hivi wa kuhifadhi lakini naona kwanza ule ukubwa wake ukuta ule ni mdogo. Mimi ushauri wangu mngelizungurusha ukuta sehemu yote ili mkawa mmehifadhi vizuri ile rasilimali. Unajua nchi yetu hii imekaa kama mvua za vuli, mara mvua mara jua, kwa hivyo mkiweza kujenga ule ukuta mtaweza kuhifadhi vizuri ili kulinda rasilimali za wananchi wetu.

Mhe. Mwenyekiti baada ya hayo machache nafikiri Mhe. Waziri amenisikiliza vizuri na hoja zangu kubwa katika bajeti yake hii zilikuwa ni hizi mbili, haya mengine yote yalikuwa ni ushauri. Tunawaombea kila la kheri watendaji wetu katika kazi zao njema, lakini na sisi Mhe. Waziri wewe mwenyewe pamoja na watendaji wako mtuombee dua maana yake sasa hivi tuko magharibi, tuko lala salama, haya tuliyowashauri basi tuje tuyasimamie.

Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru naunga mkono hotuba hii kwa asilimia mia moja. Ahsante sana. (Makofi)

**Mhe. Mwenyekiti:** Ahsante Mhe. Hamza kwa mchango wako mzuri wa kumalizia kwa siku ya leo. Waheshimiwa Wajumbe kwa vile muda tuliobakiwa nao ni dakika kumi na tano za ziada, na tuna wachangiaji hapa wanne wamebakia; kwanza Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa, Mhe. Waziri Haroun Ali Suleiman, Mhe. Naibu Waziri na hatimaye tumkaribishe Mhe. Waziri mwenyewe kwa ajili ya kufanya majumuisho, naomba watu hao wajitayarishe hadi siku ya Jumatatu watamalizia haya.

Baada ya hayo sasa nichukue fursa vile vile kukushukuruni sana kwa mashirikiano ambayo mumenipatia tokea nimeanza na mwenzangu Mwenyekiti mwenza, ambaye alianza nanyi asubuhi na hatimaye sasa hivi kufikia hapa tulipofika.

Naomba niahirishe shughuli yetu hii hadi siku ya Jumatatu Saa 3:00 za asubuhi tarehe 15/06/2015, naomba kuahirisha.

*(Saa 1:32 Usiku Baraza liliahirishwa hadi*
*tarehe 15/06/2015 Saa 3:00 Asubuhi)*